# UCHANGANUZI WA PROPOSISHENI KATIKA KISWAHILI: NADHARIA YA UHUSIANO


NA

CAROLINE WAWIRA NJUE


TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI


KATIKA

CHUO KIKUU CHA NAIROBI


2010

## IKIRARI

TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJAWAHI KUTOLEWA NA MTU YEYOTE KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU KINGINE

Wawira                                                    1/11/2010

CAROLINE WAWIRA NJUE                                                    TAREHE

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTATHMINIWA KWA IDHINI YETU KAMA WASIMAMIZI WA KAZI HII KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

MSIMAMIZI: DKT. OLALI TOM

2/11/2010

SAHIHI                                                    TAREHE

MSIMAMIZI: MADAM MWALIWA HANAH

Mwaliwa                                                    2/11/2010

SAHIHI                                                    TAREHE

## TABARUKU

Safari hii imekuwa ndefu na ngumu sana. Ili kufika kwenye ukingo wako ilibidi kujizatiti kwa kutia bidii za mchwa ajengaye kichuguu kwa mate. Safari iliponiwia ngumu sana kuna washauri walio nihimiza na kunitia moyo kuwa nitaendelea hadi tamati. Ari zao hazikuambulia patupu kwani nilitia shime zaidi. Wasaidizi wangu wandani wangu walionisaidia sana ni wazazi wangu Viginia Njeri na Nazareno Njue ambao walinilea, wakanielimisha na wakahakikisha kuwa watazidi kunitia shime ili nitimize ninayoyapenda maishani, wakachangia kwa kunipa msaada hasa wa kifedha niliouhitaji kuifanya kazi hii.

Vilevile, namtabarukia mwanangu kwa kuvumilia kuwa mda wangu naye ulikuwa nadra sana, aliyaelewa yote kuhusu usomi wangu. Kwa dhati, ninamtabarukia binti yangu mpenzi na rafiki wa karibu sana Eve Philippa Nyakio. Asante kwa uvumilivu, kunihimiza na uelewa wako. Mara nyingi nilikuacha na kuzama kwenye bahari la usomi huku ukinitia moyo wa kuendelea na kunitakia heri. Ulivumilia change moto ya kuwa na mama msomi. Uliyaelewa haya yote barabara na ukawa name hadi mwisho. Mola akubariki, akuizdishie baraka nyingi na akuinue hadi viwango vya juu zaidi na vya kustaajabisha. Sitausahau wema wako daima.

## SHUKRANI

Furaha niliyo nayo moyoni ni tele. Shukrani zangu za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha toka mwanzo hadi tamati kuhitimu katika shahada hii ya uzamili. Wema wake ni wa daima na milele kwani amenipa afya na fursa ya kushuhudia neema zake. Ninawashukuru wasimamizi wangu Madam Mwaliwa na Daktari Olali Tom. Mmenisaidia sana kwa kuhakikisha kuwa nimefikia tamati. Mmenishauri, mmenielekeza na kunihimiza katika kazi hii. Ninayo furaha moyoni kwa sababu ya ushauri wenu wa dhati. Naomba Mwenyezi Mungu awabariki na kuwapa neema katika maisha yenu.

Namshukuru Madam Mwaliwa kwa uvumilivu wake na kujitolea kwake kwa dhati. Ulipokuwa katika likizo yako ulijitolea mhanga na kuja chuoni kukutana nami kwa ushauri na kunielekeza. Asante sana. Vilevile, nakushukuru kwa kuyavumilia makosa yangu na hukuchoka kunikosoa. Daima nitakumbuka ushauri wako. Mola akuzidishie na uendelee na moyo huo huo, ulikuwa mshauri kweli.

Namshukuru Daktari Olali Tom kwa msaada wake na kujitolea hata katika wakati wake wa mapumziko. Ulikuwa mshauri kweli. Ulinitia shime na kuyavumilia yote niliyoyakosea. Nimenufaika sana kwa ushauri wako, hukuchoka kunielekeza na kunihimiza. Asante sana. Ulikuwa mshauri mwema. Daima nitakumbuka ushauri wako. Mola akuzidishie na uendelee na moyo huohuo.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Daktari Habwe John. Msaada wako umenifaa hasa ushauri na vitabu ulivyoniazima ili kufanikisha kazi hii. Asante sana kwa ushauri na msaada wako na mola akubariki. Pia, shukrani zangu za dhati ni kwa Daktari Helga Schroeder kwa msaada wake hasa wa vitabu na majarida aliyoniazima. Vilevile, alikuwa mshauri mwema. Nawashukuru wahadhiri

wote wa idara ya isimu na lugha, haswa wale ambao wamenifunza somo la Kiswahili. Mlijaa moyo wa wema na hekima. Mlikuwa katika msitari wa mbele kuhakikisha kuwa tumepata elimu ifaayo. Asante kwa kazi yenu njema. Ni dhahiri kwamba mlitufaa pakubwa. Nawashukuru wote waliotufaa katika masomo yetu ambao ni pamoja na Profesa Abdulaziz, Profesa Kithaka wa Mberia, Daktari Mwenda Mbatia, Daktari Zaja Ombaga, Daktari Kineene wa Mutiso, Daktari Habwe John, Daktari Buregea Alfred, Bwana Mungania na wengineo.

Wenzangu ambao tulizama kwenye bahari la usomi pamoja pia nawashukuru. Tumepitia mengi ya kututia shime na vilevile ya kutushusha moyo, lakini tulihimizana na kusaidiana kwa hali na mali ili kukamilisha safari hii kwa pamoja. Hongera kwa bidii zetu na kujizatiti hadi tamati. Tuliokuwa nao katika darasa la Kiswahili ni pamoja na: Veronica Wanjiku, Jacinta Nasimiyu, Walter Makokha, Abraham Walubengo, Francis Kareithi, John Kapufi. Wote walioshiriki katika kupiga chapa kazi hii pia nawashukuru. Mola awabariki.

Nawashukuru ndugu zangu Alex Njeru na JohnMark Mutugi pamoja na mkewe Carol kilee na bintiye Tamar Talia Makena, kwa kunihimiza katika masomo haya. Walitia bidii kunipa msaada wowote niliouhitaji katika safari hii. Mola awabariki na kuwazidishia neema zake kuu. Shukrani tele kwenu.

Shukrani za dhati pia ni kwa tume ya kuwaajiri walimu (TSC) kwa kuniruhu kuendelea na masomo haya kwa muda wa miaka miwili kwa kunipa likizo

Nakishukuru pia Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuniruhusu kujiunga nacho kwa masomo ya shahada ya kwanza na pia katika shahada ya uzamili. Kweli Chuo Kikuu kiliniwezeza kukamilisha masomo yangu. Mipango yake kabambe imeniwezesha kukamilisha masomo yangu kwa muda uliowekwa. Shukrani tele. Mungu awabariki na kuwazidishia neema zake.

## MUHTASARI

Utafiti huu umeshugulikia uchanganuzi wa proposisheni katika Kiswahili. Tumetumia Nadharia ya Uhusiano ya Sperber, D na Wilson, D. (2003), haswa vipengee vyake ambavyo ni; kanuni ya mawasiliano katika uhusiano na kanuni ya utambuzi katika uhusiano.

Madhumuni ya utafiti huu ni kubainisha kuwa dhana hii ya proposisheni ina maana katika pragmatiki kwa sababu proposisheni imechunguzwa katika nyanja za semantiki. Vilevile, proposisheni hubainika na kueleweka vyema hasa inapohusishwa na muktadha. Hivyo basi, tumebainisha ufahamu huu kwa kutumia miktadha tofauti.

Katika sura ya kwanza, tumeeleza kwa kifupi kuhusu proposisheni kwa jumla. Tumeeleza tatizo la utafiti na kuorodhesha madhumuni na nadharia tete za utafiti huu. Sura hii pia imeshugulikia sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka katika utafiti, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada hii na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumeshugulikia dhana ya proposisheni katika undani, aina tofauti za proposisheni, ishara za proposisheni nzuri. Vilevile, katika sura hii tumejihusisha na maana ya kiproposisheni iliyoko katika sentensi na proposisheni katika sentensi mbalimbali.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia proposisheni na istilahi nyingine, proposisheni katika vitendo usemi; lokusheni, ilokusheni na palokusheni. Vilevile, katika sura hii tumejihusisha na proposisheni katika chukulizi na umaanisho, proposisheni katika miktadha tofauti na proposisheni katika semantiki na pragmatiki.

Katika sura ya nne, tumejihusisha na uchanganuzi wa data, mfanyiko uliopo katika kuufasiri ujumbe, uzalizaji wa proposisheni. Pia, katika sura hii tumejihusisha na jukumu la muktadha kwa

kufahamu proposisheni katika mazungumzo anuwai, matarajio katika uhusiano baina ya msemaji na msikilizaji. Mwishowe katika sura hii, tumewalinganisha Wilson na Sperber dhidi ya Grice kwa kulinganisha dhana za kimsingi na kanuni baina yao.

Katika sura ya mwisho ambayo ni ya tano, tumeshugulikia muhtasari, mahitimo na mapendekezo. Tumeutoa muhtasari wa yote tuliyoyajadili katika utafiti huu kutoka sura ya kwanza hadi sura ya tano, kisha kutoa mapendekezo katika utafiti kwa wakati ujao.

## YALIYOMO

Mada........................................................................................ i

Ikrari........................................................................................ ii

Tabaruku........................................................................................ iii

Shukrani........................................................................................ iv

Muhtasari........................................................................................ vi

**SURA YA KWANZA........................................................................................ 1**

Proposisheni........................................................................................ 1

1.0 Utangulizi........................................................................................ 1

1.1 Tatizo la Utafiti........................................................................................ 3

1.2 Madhumuni ya Utafiti........................................................................................ 6

1.3 Nadharia Tete........................................................................................ 7

1.4 Sababu za kuchagua Mada........................................................................................ 7

1.5 Upeo na Mipaka........................................................................................ 8

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia na Mada........................................................................................ 8

7 Msingi wa Nadharia........................................................................................ 15

..8 Mbinu za Utafiti........................................................................................ 20

1.9. Ukusanyaji Data........................................................................................ 20

1.9.1 Uchanganuzi wa Data........................................................................................ 21

1.9.2 Umuhimu wa Utafiti........................................................................................ 21

**SURA YA PILI** .......... **23**

Dhana za Kimsingi .......... 23

2.0 Utangulizi .......... 23

2.1 Dhana ya Proposisheni .......... 23

2.2 Aina za Proposisheni .......... 32

2.2.1 Proposisheni ya Hakika .......... 32

2.2.2 Proposisheni ya Thamani .......... 33

2.2.3 Proposisheni ya Sera .......... 34

2.3. Ishara ya Proposisheni nzuri .......... 35

2.3.1 Proposisheni nzuri yapaswa Kujadilika .......... 36

2.3.2 Proposisheni nzuri yapswa Kuthibitika .......... 36

2.4 Proposisheni katika misingi ya kweli au uongo .......... 39

2.5 Aina za Kauli .......... 40

2.5.1 Maana katika Sentensi .......... 49

2.6 Proposisheni katika sentensi: Maagizo, Maswali, Kuamuru, Uyaakinifu, na Ukanushi .......... 55

2.6.1 Maagizo .......... 56

2.6.2 Maswali .......... 59

2.6.3 Kuamuru .......... 60

2.6.4 Uyakinifu .......... 61

2.6.5 Ukanushi .......... 61

2.7 Hitimisho .......... 62

**SURA YA TATU** ........................................ **64**

Proposisheni na Istilahi Nyingine ........................................ 64

3.0 Utangulizi ........................................ 64

3.1 Proposisheni katika Vitendo Usemi:Lokusheni, Ilokusheni, Palokusheni ........................................ 64

3.2 Proposisheni katika Chukulizi na Umaanisho ........................................ 69

3.2.1 Proposisheni katika Chukulizi ........................................ 69

3.2.2 Proposisheni katika Umaanisho ........................................ 78

3.3 Hitimisho ........................................ 83

**SURA YA NNE** ........................................ **84**

Uchanganuzi wa Data ........................................ 84

4.0 Utangulizi ........................................ 84

4.1 Data kuhusu Proposisheni ........................................ 85

4.2 Mfanyiko wa Ufasiri ujumbe ........................................ 88

4.3 Uzalizaji Proposisheni ........................................ 90

4.4 Jukumu la Muktadha ........................................ 92

4.5 Matarajio katika Uhusiano ........................................ 96

4.6 Kuwanganisho Sperber na Wilson Dhidi ya Grice ........................................ 98

4.6.1 Dhana za Kimsingi ........................................ 99

4.6.2 Kanuni zao ........................................ 100

4.7 Proposisheni katika Miktadha Tofauti ........................................ 101

4.8 Proposisheni katika Semantiki na Pragmatiki ........................................ 106

4.9 Hitimisho ........................................ 109

SURA YA TANO........................................................................................................ 111

Muhtasari, Mahitimisho na Mapendekezo........................................................................ 111

5.0 Utangulizi........................................................................................................ 111

5.1 Mihtasari na Mahitimisho.................................................................................... 111

5.2 Mapendekezo...................................................................................................... 118

MAREJELEO.............................................................................................................. 119

# SURA YA KWANZA

# PROPOSISHENI

## 1.0 UTANGULIZI

Fleming (1988:53-57) anasema kuwa proposisheni ni usemi ambao hukubali au kukataa jambo na ni usemi wa kweli au uongo. Proposisheni ni sehemu ya maana ya kishazi au sentensi ambayo ni imara au isiyobadilika licha ya mabadiliko katika sauti au msukomo wa kiilokusheni wa kishazi. Proposisheni yaweza kutolewa kwa kusudi la kukubaliwa au kukataliwa kama pendekezo. Proposisheni yaweza kuhusiana na vitengo vingine vya aina yake kupitia kwa uhusiano wa muda na wenye mantiki.

Kulingana na Crystal (2003: 377) proposisheni ni istilahi kutoka kwa falsafa, ambapo hadhi yake husababisha ubishi na mara kwa mara hutumika katika isimu kama sehemu ya uchanganuzi wa lugha na semantiki. Hutatua maana kwa kurejelea hisi zinazoibuka katika sentensi yenye azimio kwa kusudi la kueleza jambo lililolengwa, kuwepo kwa utata ambapo maana si dhahiri kwa mfano; "Anampenda Maria John " haifahamiki wazi ni nani anayempenda mwingine, pia kutokua na udhahiri na usonde, ili kuwa na thamani ya ukweli ulio na hakika. Kisemantiki proposisheni yaweza kuwa pana katika maana zake. Katika isimu, maumbo ya kiisimu yaliyo tofauti yanaweza kudhihirisha proposisheni moja.

Kwa mfano: 1.1: '*Paka alikula nyama.*'

'*Nyama ililiwa na paka.*'

Proposisheni hizi zina maana sawa. Tofauti ni kuwa katika kauli ya kwanza suala kuu ni kumhusu alichokifanya paka, imo katika kauli ya kutenda. Kauli ya pili yahusu kilichofanyiwa nyama, imo katika kauli tendwa. Umbo la kiisimu ambalo ni kitenzi *kula* limebainishwa katika kauli ya kutenda na kauli tendwa. Umbo moja la kiisimu laweza pia kuchanganuliwa na kuwa proposisheni kadha. Kwa mfano: 1.2: '*Tufaha zile nzuri na nyekundu ni ghali*'. Kauli hii yaeleza proposisheni kuwa:

1) **Tufaha ni za bei ya juu**.
2) **Tufaha ni nzuri**.
3) **Tufaha ni nyekundu.**

Dhana ya proposisheni ni asili ya lugha fulani kwani kila lugha huwa na kauli zake ambazo huzua maana kulingana na ujumbe kutoka kwa msikilizaji hadi kwa mzungumzaji, na hutumika kama visehemu vya sentensi kwa sababu kila sehemu hubeba maana yake. Kila proposisheni huchanganuliwa kwa misingi ya kiarifu kwa sababu hutoa maelezo kuhusu kitu au jambo fulani. Kuna tofauti kati ya maana ya kiproposisheni katika sentensi na matumizi ya sentensi. Kwa mfano: Katika vitendo usemi kuna **kanuni ya ushirikiano** ambayo huwa na kanuni ***nne*** kuu kulingana na Grice (1975, 1978) ambazo ni: **Kanuni ya idadi, kanuni ya ukweli**, **kanuni ya uhusiano** na **kanuni ya namna**. Kanuni hizi zitaelezwa kwa kina baadaye katika sehemu ya yaliyoandikwa kuhusu nadharia. Mtazamo wa kiproposisheni huchanganuliwa kama mahusiano ambayo mtu binafsi anaweza kuamua kuwa ni proposisheni. Uamuzi huu utategemea namna msikilizaji alivyoufahamu na kuufasiri ujumbe alioupokea kutoka kwa msemaji. Hivyo basi msikilizaji anaweza kuwa na mtazamo fulani kuhusu jambo alilolipokea.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa proposisheni katika Kiswahili kwa kuihusisha na Pragmatiki. Proposisheni ni kipengee cha semantiki na vilevile ni kipengee cha pragmatiki. Watu wengi kama vile Atichi (2004), Kamau (2008) wameshughulikia Proposisheni pasipo kuihusisha na pragmatiki.

Katika tasnifu ya Atichi (2004) proposisheni imechunguzwa katika misingi ya semantiki ambayo hueleza maana katika lugha. Utafiti wetu basi utachunguza proposisheni katika misingi ya pragmantiki ambayo hueleza maana inavyoelezwa kulingana na matumizi, kwa kuzingatia uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Pia, anasema kuwa maana ya neno ili kuelezeka hutegemea uhusiano wake na maneno mengine. Kwa mfano: 1.3: *Kuokoka* ni neno lenye maana kadha kama vile:

1) Ni kitenzi kinachomaanisha kuwa mtu ameokolewa kutoka kwa hali nzito au ya hatari, kama vile: '*Ningeanguka mtihani lakini mambo aliyoyaandika yaliniokoa.'*

2) Kutubu dhambi na kumuamini *Yesu Kristo kama Mwokozi.*

Hivyo basi, kitenzi hiki cha *kuokoka* kimo katika muktadha wa kisemantiki kulingana naye Atichi (2004). Hata hivyo, katika pragmatiki kuna maana ya kina kulingana na wazungumzaji, ambapo kwa kurejelea maana ya kitenzi *kuokoka*, katika 1.3; tutapata proposisheni kuwa:

1) **'Aliponea chupuchupu kuanguka mtihani.'**

**'Anayezungumziwa kumhusu alikuwa ameandika.'**

**'Aliyasoma maandishi ya aliyeandika.'**

**'Hakuanguka mtihani.'**

2) **'Hakuwa ameokoka hapo awali.'**

**'Sasa ameokoka.'**

**'Sasa ni mkristo.'**

Kamau (2008) ametafiti kuhusu masharti ya ukweli na proposisheni imo ndani yake. Anaeleza kuwa masharti ya ukweli ni muhimu katika maana kwani kauli yapaswa kuwa ya kweli au uongo kwa kuelezwa ikizingatia sheria fulani. Mbali na masharti ya ukweli, proposisheni huhusisha nyanja nyingine kama vile: Chukulizi, vitendo usemi na umaanisho. Nyanja hizi tutazizungumzia kwa undani katika sura zifuatazo hasa ile ya tatu.

Greenbaum na wenzake (1985: 1437-1438) wanasema kuwa uhusiano uliopo katika sehemu tofauti za matini hutumika kwa kuhusisha mambo yanayoshirikisha maana kama kuhusisha pragmatiki na semantiki katika usemi. Kwa mfano: 1.4: "*Umeliona gazeti*? *Kuna ajali ya ndege*."

Fasiri yake yategemea gazeti la kila siku kwa kuchukulia gazeti maalum. Hii ni kwa sababu kuna aina tofauti za gazeti ambazo huandikwa kila siku lakini kuna gazeti maalum ambalo liliangazia habari hii na magazeti mengine hayakuandika kuhusu habari hii. Uwiano kati ya sentensi hizi mbili zilizopo hapa juu wategemea:

1) Kuwa swali larejelea kitu chenye shauku maalum ambayo msemaji ataka izingatiwe.

2) Usemi huu ni muhtasari wa habari ambazo msemaji amesoma katika gazeti.

Kwingineko kama sehemu ya pili ingeendelea hivi '*...ambayo haijashughulikiwa kamwe.*' Sehemu hii iliyoendelea yadhihirisha kuwa kuna jambo la ziada ambalo msemaji ahisi kuwa ni la dharura kwani huenda ikawa hakuna waokoaji waliotumwa mahali pale na serikali au hata shirika la msalaba mwekundu halikushiriki katika shughuli zozote za uokoaji.

Basi kuhusishwa kwake kungekuwa tofauti kabisa, kwani kungezua maana kuwa msemaji ana habari zaidi kuhusu ajali hiyo.

Vilevile katika mfano mwingine kuna ufafanuzi wa maana kwa kina. Kwa mfano: 1.5:

> '*Bwana Costello aliendesha gari lake kwenda London ili kujihusisha katika maandamano dhidi ya mashambulizi ya kinuklia.*'

Kauli hii yamaanisha kuwa alijihusisha na maandamano. Vilevile kama usemi huu ungeendelea:

> '*...alihisi kuwa amefanya jambo kuhusiana na amani.*' Tunapata habari kuhusu hisia zake. Pia usemi huu kama ungeendelea;

> '*...akiwa njiani mkewe alipendekeza kuwa waende katika onyesho la maua badala yake.*'

Hivyo basi kauli yenyewe ingezidi kueleza kuwa bado alielekea London na kufika pale, lakini tunaona kuna uwezekano kuwa atafanya shughuli tofauti, kwa kwenda katika onyesho la maua badala ya kushiriki katika maandamano. Badala yake usemi huu pia ungeendelea:

> '*...mwishowe walikwenda kwa shughuli ya ununuzi katika barabara ya Regent street.*'

Hatimaye walitupilia mbali kusudi lao la awali la kwenda London na kufanya shughuli tofauti kabisa.

Utafiti huu utaonyesha umuhimu wa muktadha katika uchanganuzi wa proposisheni hasa katika misingi ya pragmatiki. Kama tunavyofahamu hakuna utafiti unaohusu semantiki na pragmatiki ambao umeshughulikia proposisheni ili kusuluhisha utata wa maana tofauti katika miktadha mbalimbali. Tutasuluhisha tatizo lililopo kwa maswali kama:

i) Je, dhana ya proposisheni ina maana katika misingi ya pragmatiki?

ii) Je, kuna umuhimu wa muktadha katika uelewa wa proposisheni?

iii) Je, proposisheni imo katika pragmatiki, semantiki au ni katika vipengee vyote viwili?

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu utaongozwa na madhumuni yafuatayo:

1) Kueleza jinsi dhana ya proposisheni ina maana katika pragmatiki.
2) Kuonyesha umuhimu wa muktadha katika uelewa wa dhana ya proposisheni.
3) Kubainisha kama proposisheni imo katika pragmatiki au semantiki ama ni katika pragmantiki na semantiki kwa pamoja.

## 1.4 NADHARIA TETE

Nadharia tete zitakazotathminiwa katika utafiti huu ni:

1) Dhana ya proposisheni ina maana katika pragmatiki.
2) Kuna umuhimu wa muktadha katika uelewa wa dhana ya proposisheni.

3) Proposisheni imo katika pragmatiki na semantiki.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Suala la maana huleta utata kwa sababu ipo maana katika lugha na vilevile ipo maana katika watumizi kulingana na jinsi msikilizaji na mzungumzaji wanavyohusiana. Proposisheni kama kitengo cha maana huzua utata baina ya maana hizi mbili. Jambo hili lilichangia kuwepo kwa ari katika kuchagua mada hii, kwani maana katika pragmatiki na semantiki ndicho kiini hasa katika mawasiliano. Kwingineko, dhana ya proposisheni kwa misingi ya nadharia ya uhusiano na katika pragmatiki kama tunavyofahamu haijashughulikiwa katika utafiti na kama tulivyoona hapo awali proposisheni ina maana zake anuwai. Hivyo basi, ni muhimu kuwepo na uelewa bora wa proposisheni ili kufahamu na kufasiri maana ipasavyo.

Utafiti huu utachangia katika nyanja za pragmatiki na semantiki kwa kueleza zaidi kuhusiana na maana ya mambo yaliyowasilishwa kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji. Vilevile utafiti huu utatumika kurejelea katika mada zinazohusiana na maana hasa kwa kubainisha tofauti iliyopo kati ya maana katika jambo na maana kulingana na uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umejikita tu katika uchanganuzi wa proposisheni katika Kiswahili. Hivyo basi, hatutajishughulisha na mambo kama: Majukumu na aina ya semantiki na pragmatiki. Pia hatutajishughulisha kwa semantiki na pragmatiki katika lugha ya Kiswahili, bali shughuli yetu yahusu uchanganuzi wa proposisheni. Vilevile katika utafiti huu, hatuna kusudi la

kuangazia masuala yote ya nadharia ya uhusiano. Utafiti huu umejikita katika mifanyiko na kanuni za nadharia ya uhusiano ambazo zinahusiana na proposisheni. Mifano itatumika kutoka lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kufafanua maelezo.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU NADHARIA NA MADA

Sehemu hii inahusu utafiti uliofanywa hapo awali na wasomi na hata wanaisimu tofauti kwa kurejerea proposisheni pamoja na nadharia ya uhusiano ambayo tunaihusisha katika utafiti wetu.

Katz (1977:50-51) anasema kuwa maana ya sentensi huwepo kwa sababu ya uhusiano uliopo baina ya nadharia ya vitendo usemi na nadharia ya semantiki. Nadharia ya vitendo usemi ya John R. Searcle na John L.Austin yahusu vitendo. Nadharia ya semantiki yahusu muundo wa sarufi katika lugha. Hivyo tutaweza kubainisha ujumbe wa kisemantiki na ujumbe wa kipragmatiki, kisha kutumia kanuni za vitendo usemi zinazohitajika katika semantiki na pragmatiki. Vilevile tunaweza kuunda ujumbe unaowakilishwa na msukumo wa kiilokusheni katika sarufi ambapo ni muhimu kubainisha pragmatiki na sarufi. Hakujihusisha na nadharia ya uhusiano lakini ametumia vitendo usemi ambavyo pia tutavichanganua katika utafiti wetu.

Griffin (1991:29-30) anamnukuu Osgood (1984) katika nadharia yake patanishi ambapo aliunda mbinu za kutofautisha semantiki ili kulinganisha maana tofauti zilizomo katika maneno ya watu tofauti. Hisia za watu zitakuwa tofauti. Kwa mfano: 1.6: "*Mngurumo wa radi*". Watu tofauti watakuwa na hisia tofauti, wengi watashtuka na kuna wale hawatababaika kamwe. Nadharia yake yahusiana na nadharia tutakayoitumia kwa sababu yahusu maana hasa katika wazungumzaji.

Wilson na Sperber (2002: 2004) wanasema mifanyiko ya kipragmatiki katika ufahamu wa kauli hutendwa na mfumo maalum katika akili ambao hutegemea nyanja tofauti katika tabia za binadamu. Mifanyiko hii ina kanuni na taratibu zake ambazo huchanganua tabia za watu katika mawasiliano. Kanuni hizi ni; **kanuni ya utambuzi** na **kanuni ya mawasiliano.** Kwingineko, Wilson na Sperber (1995:51) wanasema kuwa kanuni ya mawasiliano katika uhusiano yahusu kauli ambazo huibua chukulizi zenye upeo wa juu katika uhusiano. Kauli yoyote ile yaweza kuchukuliwa kuwa:

a) **Yenye kuhusika vya kutosha ili mpokezi ujumbe apate juhudi fulani za kufasiri ujumbe.**
b) **Yenye kuhusika zaidi na kuafikiana na hali iliyopo katika maarifa ya mzungumzaji pamoja na mapendeleo na malengo yake.**

Nadharia ya uhusiano huhusika na kanuni mbili kuu, ambazo: Kwanza, ni **kanuni ya utambuzi** ambapo utambuzi wa binadamu hutegemea uhusiano wa kiwango cha juu baina yake na anayewasiliana naye. Pili, ni **kanuni ya mawasiliano** ambapo kauli humpa binadamu matumaini ya upeo wa juu. Grice (1989) anasema kuwa mwasilishaji ujumbe hufahamu ujumbe ambao hufasiriwa na mpokezi wa ujumbe na hupata maana ya kiisimu iliyokusudiwa. Mfanyiko wa kipragmatiki huibua chukulizi za muktadha katika masharti ya kweli. Jukumu kuu la kanuni hizi tulizozitaja hapo awali limo katika kufafanua kauli za kitamathali, zinazohusisha semi na methali katika ukweli wake. Uhusiano huwa na asili yake katika mawazo, kumbukumbu na ufahamu.

Proposisheni huhusishwa na kauli na hukidhi mahitaji ya uhusiano kupitia kwa yaliyosemwa. Wanaoshiriki huelewana na kufasiri vyema ujumbe kutoka kwa kila mmoja wao katika mazungumzo yao. Kwa mfano: 1.7: *Peter* : "*John alikulipa deni lako?*"

*Mary* : "*Alisahau kwenda benki.*"

Hivyo basi Mary anaposema "*alisahau kwenda benki*", Peter anamaanisha kuwa John hakuweza kumlipa Mary deni lake kwa sababu alisahau kwenda benki. Vilevile, huenda John atamlipa Mary deni lake wakati atakapokwenda benki.

Paul Grice (1975, 1978), katika nadharia yake ya umaanisho ambayo ni ya kiisimu, anaeleza jinsi watu katika mawasiliano hufahamu kauli tofauti ambazo hazihusiani katika diskosi na kuzifasiri kama zilivyokusudiwa. Msikilizaji huwa na uwezo wa kufasiri na kuratibu ujumbe wa kiisimu na usio wa kiisimu katika ufahamu wake. Vilevile, kuna kanuni ya ushirikiano, ambapo umaanisho umo ndani ya ushirikiano. Ushirikiano huzua umaanisho wa jambo lililomaanishwa na kauli tofauti kisha jambo hilo lieleweke na kufasiriwa ipasavyo na msikilizaji. Hivyo basi kuna ushirikiano baina ya dhana ya umaanisho na ile ya ushirikiano ambazo zitajadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Kanuni nne ambazo huzingatiwa katika kanuni hii ya ushirikiano kwenye mazungumzo huwa ni:

**1)Kanuni ya idadi**: Kusema mambo yanayotosheleza katika mazungumzo. Yaani, usizidishe wala kupunguza. Kama vile; 'Mazungumzo baina ya mzazi na mwalimu. Mzazi anataka kujua maendeleo ya mwanawe katika masomo. Mwalimu anamwambia ni mzuri katika spoti. Mzazi hakupata jibu aliliotarajia kuhusu masomo ya mwanawe bali alielezwa kuhusu spoti.'

**2) Kanuni ya ukweli**: Kuhakikisha kuwa wasema ukweli unaouamini na kuujua ili mawasiliano yasitatizwe. Kama vile: 'Rais wa Kenya ni mwanamume. Huu ni ukweli unaofahamika.'

**3)Kanuni ya uhusiano**: Mambo yatakayosemwa yahusu kisemwacho. Kama vile: 'Mambo ya kijinsia yakizungumzwa katika kongamano la lugha hayatakuwa na uhusiano wowote na kongamano hilo.'

**4)Kanuni ya namna**: Mambo yazungumzwe kwa jinsi iliyo wazi wala sio kwa kificho. Kama vile: 'Mtu akiagiza apewe kikombe hawezi kupewa kitu kingine kama kisu au kijiko. Lazima atapewa kikombe alichokiagiza.'

Schroeder (2005:69) anasema kuwa mwingiliano wa watu kutoka jamii tofauti husababisha utata katika mawasiliano. Jambo hili laweza kusababisha msikilizaji kuwa na uhusishi usiofaa katika ujumbe, kisha kutoelewa ujumbe huo. Utata huu ni kwa sababu jamii tofauti huwa na chukulizi tofauti. Anaendelea kueleza kuwa ufahamu wa jambo hukwama kwani kanuni ya uhusiano hupata ujumbe usio sahihi na kuupeleka kwa mpokezi bila usahihi unaofaa. Basi ni muhimu kwa wanaoshiriki katika mawasiliano kuelewana vyema. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu unahusisha maana na ufahamu wake kulingana na uhusiano uliopo baina ya msikilizaji na mzungumzaji ambalo ni jambo mojawapo la kimsingi katika utafiti wetu.

Atoh (2001) anachanganua hadhi ya kisemantiki katika baadhi ya nomino za Kidholuo, wakati ambapo nomino hizi hutokea katika nyanja tofauti na jinsi zinavyohusiana katika



UNIVERSITY OF NAIROBI
LOWER KABETE LIBRARY

nyanja hizo. Katika utafiti wake baadhi ya nomino hupata maana, kwa jinsi zinavyohusiana na nomino nyingine. Utafiti wake wahusu nomino, lakini utafiti wetu utahusu sentensi na kauli tofauti ambazo hujumuisha nomino pia. Utafiti wake unatupa mwelekeo muhimu hasa wa kisemantiki katika kuangazia suala la maana.

Atichi (2004) amechanganua mifanyiko ambayo husababisha maneno kubadilisha maana na kujadili mambo ambayo husababisha kubadilika kwa maana katika Kiingereza cha Kenya. Utafiti wake unaeleza kuwa sababu ambazo zasabisha maana hii kubadika ni anuwai kulingana na umuhimu wa mambo ya kijamii ambayo huamua matumizi ya lugha yatakuwa vipi. Utafiti wake unahusu maana katika maneno na mabadiliko yake. Utafiti wake ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu maana ndio hasa jambo la kimsingi katika utafiti wetu.

Ogola (2006) ameshughulikia mawasiliano ya kiisimu kwa kuyahusisha na muktadha wa kitamaduni katika matamshi na kuchambua mawazo ya uhusiano pamoja na mawazo katika nadharia ya uhusiano. Vilevile amejihusisha na uchambuzi wa baadhi ya dhana tofauti za nadharia ya uhusiano ambayo tutaitumia katika utafiti wetu. Hata hivyo hatutajihusisha na dhana zote za nadharia hii bali tutazitumia tu zile zinazohusiana na proposisheni. Utafiti huu unatuhusu kwa sababu umeshughulikia muktadha kwa kuuhusisha na nadharia ya uhusiano ambayo itasuluhisha tatizo letu la utafiti.

Njeri (2007) amefanya utafiti wa kipragmatiki kuhusiana na miiko katika lugha ya Gikuyu katika mazungumzo kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Ameeleza kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo ni miiko kuyazungumzia katika jamii ya Gikuyu hasa yanayohusu masuala nyeti

kama ugonjwa huu wa ukimwi. Vilevile anahusisha kanuni za Grice ambazo ni muhimu kuzizingatia katika mazungumzo ili mzungumzaji na msikilizaji washirikiane na kufahamiana ipasavyo. Utafiti huu utatufaa hasa katika nadharia aliyoitumia ya Neo-Grice ya umaanisho, ambayo pia itatuhusu kwa kuzingatia kanuni zake. Kanuni hizi tutazieleza zaidi baadaye hasa katika sura ya tatu.

Kamau (2008) ameonyesha umuhimu wa muktadha katika masharti ya kweli na hivyo basi anahusisha semantiki na pragmatiki kwa pamoja. Kulingana na utafiti wake proposisheni yahushwa na hakuihusisha katika nyanja zake tofauti. Hata hivyo, hajashughulikia mtagusano baina ya semantiki na pragmatiki ambao ni muhimu katika kubainisha maana zake. Utafiti huu wetu utahusisha proposisheni katika semantiki na pragmatiki. Utafiti wake utatufaa kwa sababu masharti ya kweli ni jambo la kimsingi katika uchanganuzi wa proposisheni.

Munga (2008) katika uchanganuzi wake ameonyesha kuwa miktadha tofauti kama ya kitamaduni, ya diskosi, ya kijamii, ya kitambuzi na ya ufahamu wa jambo lililotajwa au kuelezwa hapo awali ni muhimu ili kuelewa uhusiano uliopo wa kimaana katika Gikuyu. Hili hasa ni katika hali ambapo neno huwa na maana zaidi ya moja, hivyo kurejelea mambo tofauti. Baadhi ya maneno hubadilisha maana katika miktadha tofauti. Utafiti huu utatufaa kwa sababu miktadha mbalimbali itaibua maana tofauti za proposisheni.

Ndung'u (2009) ameeleza kuwa sarufi hutoa njia tofautitofauti za kuelezea kauli moja, yaani taarifa moja yaweza kuelezwa kwa kutumia kauli mbalimbali. Anaendelea kusema kuwa uchanganuzi katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili sanifu umeegemea katika kiwango cha sentensi katika muktadha wa diskosi. Muktadha huu utashirikisha

mazungumzo baina ya watu tofauti na maana zilizopo katika kauli zao. Utafiti huu utatufaa kwani tutajihusisha na maana katika kauli tofauti na miktadha tofauti katika sentensi ili kuchambua maana katika proposisheni.

## 1.8 MSINGI WA NADHARIA

Nadharia ya uhusiano ni ya mawasiliano, inayohusu mzungumzaji na msikilizaji. Mawasiliano haya huhakikisha kuwa msikilizaji huufasiri ujumbe na kisha kuibua chukulizi kadha akilini mwake. Nadharia ya uhusiano huhusishwa na sematiki na pragmatiki lakini inajikita zaidi katika pragmatiki. Kulingana na nadharia ya uhusiano usemi wafaa kuwa na umuhimu ama uhusiano kwa msikilizaji na vilivile kupunguza juhudi katika kuufasiri ujumbe. Nadharia ya uhusiano ni maelezo ya nadharia ya umaanisho ya Paul Grice (1975, 1978). Kanuni ya ushirikiano ya Grice yasisitiza na kumzingatia msemaji. Kwa mfano; Msemaji anafaa kusema idadi ya maneno inayotosheleza, asipunguze wala kuzidisha na aseme ukweli anaoujua yeye. Vivyohivyo katika utafiti huu tutawalinganisha Wilson na Sperber (2002,2004) wanao jadili kuhusu nadharia ya uhusiano dhidi ya Grice (1975,1978) anayejadili kanuni za ushirikiano kwani maoni yana ukuruba kwa kiasi fulani.

Nadharia ya uhusiano inalenga kuchanganua jinsi mifanyiko mbalimbali ya kiakili inavyohusika ili msikilizaji aweze kufasiri maana lengwa. Nadharia hii ina vipengee vyake ambavyo ni:

a) **Kanuni ya mawasiliano katika uhusiano.**

b) **Kanuni ya utambuzi katika uhusiano.**

Vilevile kuna vipengee vinginevyo vinavyohusishwa na nadharia ya uhusiano kama;

a) **Uhusiano na ufahamu.**

b) **Athari za kiutambuzi.**

c) **Juhudi zinazohitajika katika uchanganuzi.**

Deirdre Wilson na Dan Sperber (2003:3) wanasema kuwa katika mawasiliano binadamu huwa makini katika jambo lililo muhimu na lililo na uhusiano. Uhusiano ni jambo la kimsingi katika utambuzi wa binadamu.

Kwa mfano: 1.8:

a) *'Maria na Jane wamo katika mazingira mamoja ya utambuzi.'*

b) *'Redio yaanza kucheza muziki.'*

Kauli hizi zaeleza chukulizi kuwa;

1. **'Inatambulika kwa Jane na Maria, kuwa redio inacheza muziki.'**
2. **'Inatambulika kwa Jane na kwa Maria, kuwa kila mmoja wao anafahamu kuwa mwenzake anatambua kuwa redio inacheza muziki.'**

Chukulizi hizi zaweza kueleza proposisheni zilizopo kuwa za kweli au uongo. Kama kuna redio ambayo imefunguliwa basi itakuwa ni kweli. Kama kuna redio ambayo haijafunguliwa au hamna hata redio, basi itakuwa ni uongo.

Hofman (1993:7) anasema kuwa proposisheni ni mawazo yaliyokamilika na yenye kutosheleza katika kuwa kweli au uongo. Hivyo basi proposisheni haiwezi kuwa ya kweli au uongo kwa wakati mmoja.

Chukulizi katika 1.8; zahakikisha proposisheni kuwa;

1) **'Mahali walipo Jane na Maria kuna redio.'**

2) **'Redio yenyewe imefunguliwa.'**

3) **'Redio yenyewe inacheza muziki.'**

Hivyo basi, tunafahamishwa kuwa kuna uhusiano uliopo kati ya Jane na Maria kwa wote wanafahamu fika kuwa kila mmoja wao ameisikia sauti kutoka kwa redio. Vivyo hivyo, kila mmoja wao anao uwezo wa kufamu kuwa redio iaucheza muziki.

Kimsingi, uhusiano ni mfanyiko wa kufikiria ukiongozwa na masharti kuwa utambuzi wa binadamu huelekezwa kufikia kiwango cha juu cha athari za kiutambuzi. Athari hizi husababisha tofauti za jinsi mtu binafsi anavyopata elimu na anavyokumbuka, anavyotatua matatizo na matumizi yake ya lugha. Kila mtu huwa na tofauti zake katika kutimiza mambo haya, kulingana na anavyoyakumbuka mambo aliyoyahifadhi akilini mwake.

Kanuni ya mawasiliano yahusisha msikilizaji na mzungumzaji. Mawasiliano huafikiwa kama msikilizaji atakuwa makini wakati msemaji anapozungumza. Ujumbe wa msemaji utakuwa muhimu na wenye uhusiano uliotosheleka katika thamani ya umakinifu wa msikilizaji.

Kwa mfano: 1.9: '*Maria na Jane wanatazama mazingira fulani ya kuvutia, na Maria ametambua kuwa kuna kanisa linaloonekana kwa mbali, Anamwambia Jane.*' "*Nimewahi kuwa ndani ya kanisa.*" Kabla ya kauli hii Maria hakutafakari kama Jane amelitambua jengo lile na kama Jane anachukulia kuwa ameliona au kama Jane anafahamu kama Maria anakisia kuwa ni kanisa. Kwake Maria anajua kuwa ni jambo la kawaida kuwa Jane ana uwezo wa kulifahamu jengo la kanisa. Hivyo basi chukulizi katika 1.9; yadhihirisha proposisheni kuwa;

1. **Maria amewahi kuwa ndani ya kanisa.**
2. **Maria ana uwezo wa kufahamu jengo la kanisa akiliona kwa mbali.**
3. **Jane vilevile ana uwezo wa kulifahamu jengo la kanisa akiliona kwa mbali.**

Maria aliweza kuwasilisha ujumbe wake aliokusudia kwa Jane. Proposisheni hizi basi zitakuwa ni za kweli kama Maria aliona na kufahamu jengo la kanisa. Zitakuwa za uongo kama aliona jengo lile kuwa ni kasri au kitu kisicho jengo la kanisa au kama hakuona chochote.

Wilson na Sperber (2003) wanasema kuwa semi zaweza kuongeza, kuondoa au kuunganisha juhudi pamoja na chukulizi zilizopo ili kuleta maana ya kimuktadha. Umuhimu wa ujumbe utachangia katika ufasiri wa ujumbe. Chukulizi haitakuwa na athari yoyote katika muktadha kama haihusiki na muktadha wenyewe, badala ya kuongezwa juhudi, utaondolewa. Kuwepo kimuktadha kwa habari katika muktadha ni jambo muhimu katika uhusiano.

Kwa mfano: 1.10: *kumuona mtu ambaye unamwona kama ni punguani kwa jinsi alivyovalia. Baadaye kumuona mtu yuyu huyu akihudhuria mihadhara darasani utastaajabu kwa jambo hilo.* Ujumbe uliokuwa umeufasiri hapo awali utapungua kwani umelifasiri jambo jipya baada ya kumuona akihudhuria mihadhara. Kwingineko katika mfano mwingine; *kumuona mtu anayezungumza pweke kisha baadaye upate kufahamu kuwa mtu yule ni akili punguani.* Hivyo basi, fasiri uliyokuwa nayo hapo awali wa akilini huongezeka kwa sababu umehakikisha kuwa ni punguani.

Katz (1977:50-51) anamnukuu Zeno Vendler (1972) katika nadharia yake ambayo yahusu mawazo katika binadamu anasema kuwa **kufahamu**, **kuamini**, **kukataa** na **vitenzi vingine vya mtazamo wa kiproposisheni katika sentensi iliyonominishwa hasa nomino,** hueleza proposisheni na huzua mfanyiko wa matendo.

Kwa mfano: 1.11: "*Nasikiza kuimba kwake.*" Sentensi hii ina proposisheni kuwa:

1) **Inanirejelea mimi.**

2) **Kuna mtu anayeimba.**

3) **Mimi namsikiza mtu anayeimba.**

Vilevile katika kitenzi tunaweza kupata proposisheni anuwai.

Kwa mfano: 1.12: Kitenzi; *Teua*

1) **"Nimekuteua ili uwe Rais."**

2) **"Nimekuteua kuwa Rais."**

3) **"Nimekuteua kuwa kwenye Shirika la Urais."**

Sentensi hizi zinaeleza neno *Teua* kama kitenzi tendaji kwa kukihusisha katika sentensi tofauti ambazo zinafafanua proposisheni moja kwa njia tofauti na kupata maana mbalimbali zinazoeleza wadhfa wa kuwa Rais.

Abraham (1966:38-39) anasema kuwa nadharia yafaa kujibu maswali kikamilifu, yapaswa kuonyesha kama sentensi ina mantiki au la. Kwa mfano: 1.13: 1) " *Analima kiisimu.*"

2) "*Analima polepole.*"

Kauli ya kwanza haina mantiki kwani kulima hakuna uhusiano wowote na isimu, ilhali ya pili ina mantiki kwa sababu yaeleza jinsi alivyolima. Sentensi yenye mantiki yaweza kuwa na maana tofautitofauti. Hivyo basi nadharia yapaswa kudhihirisha maana hizi.

Kwa mfano: 1.14: "*Mvulana aliupiga mpira.*"

"*Peter anacheza na ndugu yake.*"

Kila mojawapo ya sentensi hizi ina maana zaidi ya moja. Sentensi ya kwanza ina maana kuwa; mvulana aliupiga mpira ili kucheza, mvulana aliupiga mpira kwa sababu alikuwa na hasira. Sentensi ya pili ina maana kuwa Peter na ndugu yake wanacheza pamoja, Peter anamchezea ndugu yake ambaye hataki kucheza. Maelezo haya ya Abraham yatatufaa katika utafiti wetu kwa sababu maana iliyo na mantiki ni muhimu ili ujumbe ueleweke kwa udhahiri na pia kubainisha maana halisi iliyopo katika kauli zenye maana zaidi ya moja.

Hivyo basi, tutaitumia nadharia hii ya uhusiano kwa kuzichanganua sentensi tofauti kwa kuzingatia kanuni mbili kuu zake ambazo ni; kanuni ya mawasiliano katika uhusiano na kanuni ya utambuzi katika uhusiano, ili kueleza maana inayozuka katika proposisheni.

## .9 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii yahusu ukusanyaji data na uchanganuzi wa data hiyo. Data itakayokusanywa itarejelea proposisheni katika kategoria zake tofauti kwa jinsi zitakavyojitokeza kwenye kauli mbalimbali katika Kiswahili.

### .9.1 UKUSANYAJI DATA

Utafiti wa kina ni katika maktaba ili kupata yaliyoandikwa na yaliyo muhimu katika utafiti huu. Sentensi tofauti zitakazoeleza proposisheni zitachanganuliwa. Habari za mtandao pia zitatumika hasa itakapobidi kufanya hivyo. Sentensi hizi ambazo zitaeleza kuhusu proposisheni zitatumiwa kama data ambayo itafafanua na kubanisha bayana proposisheni na jinsi huundwa na kufahamika kisha kufasirika ipasavyo na msikilizaji kutoka kwa msemaji. Mtafiti pia ataongeza data kwa kutumia mifano kadha ili kupambanua zaidi maana itakayoelezwa.

### 1.9.2 UCHANGANUZI WA DATA

Data itakayokusanywa itachanganuliwa katika misingi ya nadharia ya uhusiano ili kuhakikisha kuwa madhumuni ya utafiti yametimia. Sentensi zitakazotumika katika data zitapangwa na kuainishwa katika maana zake tofauti za proposisheni. Maelezo ya kisemantiki katika sentensi tofauti yatabainishwa kisha mawasiliano ya sentensi hizo kwa kuihusisha na muktadha wa kipragmatiki kulingana na watumizi lugha. Vilevile, katika sehemu hii tutajihusisha na utaratibu unaozingatiwa katika kuibua maana mbalimbali za proposisheni mara tu zinapotamkwa kama kauli zenye lengo fulani. Pia, data itaonyesha mfanyiko unaohusika katika kuufasiri ujumbe na kudhihirisha umuhimu uliopo katika muktadha kwa jumla. Kwingineko data yetu itawalinganisha wanafalsafa Wilson na Sperber (2002,2004), wanaojadili nadharia ya uhusiano dhidi ya mwanafalsafa Grice (1975,1978), anaye jadili dhana kuhusu kanuni za ushirikiano, katika kueleza jinsi ambavyo mawasiliano hutimia.

### 1.9.3 UMUHIMU WA UTAFITI

Utafiti huu ni muhimu hasa katika nyakati hizi ambapo mawasiliano ni jambo linalozua utata baina ya watu wengi. Watu wengi huwasiliana vyema kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Jambo hili lahitaji kuwepo kwa uelewa bora wa maana ili kuwa na mawasiliano mwafaka zaidi kati ya watu wa tabaka mbalimbali. Kwa mfano: Watalii wengi huzuru nchi yetu na hutumia Kiswahili kama lugha ya taifa nchini mwetu. Shughuli kama za kortini ambapo watu wanaohusika katika kesi ni wa makabila tofauti na labda kuna wale hawazifahamu lugha za wenzao, basi itakuwa muhimu kutumia lugha itakayoeleweka na kufasirika vyema kwa wote. Wengi wa watalii hawa hutaka kujifunza lugha ya Kiswahili. Vilevile Kiswahili hutumika

katika shughuli za kitaifa kama sherehe za taifa. Matokeo ya utafiti huu yatazua mwelekeo mpya wa kutafiti maana katika pragmatiki na semantiki kwa kutumia nadharia ya uhusiano.

# SURA YA PILI

## DHANA ZA KIMSINGI

### 2.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia dhana ya proposisheni, aina za proposisheni, proposisheni katika misingi ya kweli au uongo na vilevile, proposisheni katika sentensi. Vilevile, inajihusisha na maagizo, maswali, kuamuru, uyakinifu na ukanushi.

### 2.1 DHANA YA PROPOSISHENI

Katie Wales (2001), anasema kuwa proposisheni ni neno lililoazimwa kutoka kwa elimu ya falsafa. Maana kiproposisheni katika kauli au sentensi ndio ya kimsingi akilini na wakati huohuo maana katika proposisheni ni ya kidhahania ambayo huhusisha kiima na kiarifu. Proposisheni hufanana na vitendo usemi vya kauli. Hulingana kisarufi na sentensi arifu ambayo huwa na kiima na kiarifu. Hata hivyo, kuna tofauti baina ya viwango tofauti vya sarufi na maana. Kama vile, sentensi katika kauli tendaji na katika kauli tendwa zaweza kueleza proposisheni ambayo yaonekana kuwa moja hata kama zina kiima na kiarifu tofauti. Kwa mfano: 2.1: *Mpira ulichezwa na watoto.*

*Watoto waliucheza mpira.*

Vilevile, proposisheni yaweza kuwa na maana zaidi ya moja, kama ina utata.

Kwa mfano: 2.2: *Joy amepigia Judy mpira.*

# SURA YA PILI

## DHANA ZA KIMSINGI

### 2.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia dhana ya proposisheni, aina za proposisheni, proposisheni katika misingi ya kweli au uongo na vilevile, proposisheni katika sentensi. Vilevile, inajihusisha na maagizo, maswali, kuamuru, uyakinifu na ukanushi.

### 2.1 DHANA YA PROPOSISHENI

Katie Wales (2001), anasema kuwa proposisheni ni neno lililoazimwa kutoka kwa elimu ya falsafa. Maana kiproposisheni katika kauli au sentensi ndio ya kimsingi akilini na wakati huohuo maana katika proposisheni ni ya kidhahania ambayo huhusisha kiima na kiarifu. Proposisheni hufanana na vitendo usemi vya kauli. Hulingana kisarufi na sentensi arifu ambayo huwa na kiima na kiarifu. Hata hivyo, kuna tofauti baina ya viwango tofauti vya sarufi na maana. Kama vile, sentensi katika kauli tendaji na katika kauli tendwa zaweza kueleza proposisheni ambayo yaonekana kuwa moja hata kama zina kiima na kiarifu tofauti. Kwa mfano: 2.1: *Mpira ulichezwa na watoto.*

*Watoto waliucheza mpira.*

Vilevile, proposisheni yaweza kuwa na maana zaidi ya moja, kama ina utata.

Kwa mfano: 2.2: *Joy amepigia Judy mpira.*

Maelezo katika mfano 2.2, yana maana kuwa labda Joy alimpiga Judy kwa sababu ya Mpira au pengine alimpigia mpira ili wacheze pamoja, vilevile huenda ikawa Joy aliupiga mpira kwa niaba ya Judy. Hivyo basi, proposisheni katika sentensi hii tabainika kama msemaji ataeleza bayana maana aliyoikusudia katika kutamka kauli hii.

Kulingana na Halliday (1985), proposisheni hukubaliwa au kukataliwa. Hii ina maana kuwa kama ni ya ukweli ambao unaweza kuthibitika, basi itabidi washiriki katika mazungumzo kuikubali na kuamini jambo lililomo katika proposisheni hiyo. Kwingineko, kama itakuwa haina ukweli ambao unaweza kuthibiti, basi washiriki katika mazungumzo wataikataa na kutoiamini kuwa ya kweli. Hivyo basi, ni lazima proposisheni ithibitiwe katika misingi ya kweli au uongo.

Kwa mfano: 2.3: '*Nchi ya Kenya ni huru.*'

Proposisheni katika kauli hii itakubalika kwa sababu ni jambo lililo wazi na kila mtu anafahamu kuwa ni nchi yetu ilijinyakulia uhuru na kujikomboa kutoka kwa utawala wa wakoloni.

Larson (1984:89 -197), anasema kuwa proposisheni ni mkusanyiko wa dhana katika kundi la watu ambalo huwasiliana. Hivi anamaanisha kuwa Proposisheni hutegemea uhusiano uliopo baina ya dhana zilizomo.

Kwa mfano: 2.4: *John, Peter, alimpiga.*

Kama John ndiye aliyetenda kitendo cha kumpiga Peter, basi proposisheni itakuwa: **John alimpiga Peter**. Vivyo hivyo, Kama Peter ndiye aliyetenda kitendo cha

kumpiga John, basi proposisheni itakuwa: **Peter alimpiga John**. Muundo wa semantiki katika proposisheni waweza kuonyeshwa kwa njia zifuatazo tunazoziangazia hapa chini.

Kwa mfano: Proposisheni katika 2.4;

1)**Mtenda** : *John ...* **kitendo** : *kumpiga ...* **mwathiriwa** : *Peter*

2)**Mtenda** : *Peter ...* **kitendo** : *kumpiga ...* ***mwathiriwa*** : *John*

Mfuatano wa maneno katika sarufi utabainisha ni nani aliyempiga mwingine. Proposisheni yaweza kuzua maana kadha.

Kwa mfano: 2.5:

1) *John alimpiga Peter.*
2) *Peter alipigwa na John.*
3) *Kupigwa kwa Peter kulifanywa na John.*
4) *Peter ndiye alipigwa na John.*
5) *John ambaye alimpiga Peter.*

Kuna proposisheni za matukio ambazo hubainishwa kwa dhana ambazo huwakilishwa na maneno tofauti. Kama vile:

Uhalifu wa mji ulipangwa vyema.

↓ Tukio ↓ kitu ↓ tukio ↓ matokeo

Sentensi iliyo hapo juu kwanza itachanganuliwa kwa kutambua dhana ambazo huwakilishwa na maneno tofauti. Kisha, sentensi hii ya kisarufi kuelezwa kama proposisheni ambapo matukio yatakuwa msingi wa proposisheni hizo. Hivyo basi, matukio hayo yatakuwa; **kuharibu** na **kupanga**.

Proposisheni zitakuwa: **Mtu aliharibu mji.**

**Mtu alipanga vyema.**

Proposisheni huelezwa kwa kujumlisha wahusika. Nomino **Mtu** imetumika katika proposisheni hizi kuwakilisha mtenda ambaye alitenda kitendo.

Kwa mfano: 2.6: '*John alikataa ahadi ya Peter.*'

Matukio *basi ni **kukataa*** na ***ahadi*** kisha Wahusika ni ***John*** na ***Peter***.

Hivyo basi, John alikataa naye Peter alikuwa ameahidi kufanya kitu fulani na Peter aliahidi kabla ya John kukataa. Hatimaye tunafahamu kuwa tukio la kuahidi lilifanyika kabla ya tukio la kukataa.

Proposisheni ndicho kitengo kidogo zaidi katika mawasiliano. Dhana moja hutokea pamoja na dhana zingine ili kuwepo na mawasiliano yenye maana. Kila tukio huwakilisha proposisheni. Kwa mfano: 2.7: '*Joy aliruka ukuta, alikimbia na kutumbukia ndani ya ziwa'*.

Sentensi 2.7; ina proposisheni tatu ambazo ni:

1) **Joy aliruka ukuta.**

2) **Joy alikimbia.**

3) **Joy alitumbukia ziwani.**

Matini chanzi katika lugha yoyote yaweza kuwa proposisheni. Kwa mfano: 2.8:

1) Lugha chanzi: *Kutotii husababisha kuteseka sana.*

Proposisheni: **Mtu hukosa kutii.**

**Mtu huteseka.**

2) Lugha chanzi: *Sifa hiyo ilipokelewa vyema na Maria.*

Proposisheni: **Mtu alimsifu Maria.**

**Maria aliitikia vyema.**

3) Lugha chanzi: *Watu wanaofikiria kuwania kiti cha Urais, wataanzisha kampeni zao hivi karibuni.*

Proposisheni: **Kuna watu wanaolifikiria tendo.**

**Wanataka kuwa Rais.**

**Watafanya kampeni hivi karibuni.**

Tukio laweza kuwa; **tendo, tajriba** au **mfanyiko.**

Kwa mfano: 2.9: **Tendo:** *Wavulana walikimbia.*

*Paul alikula.*

**Tajriba:** *Maria alisikia filimbi.*

*John aliona ng'ombe.*

**Mfanyiko:** *Barafu iliyeyuka.*

*Paka alikufa.*

Kuna proposisheni za hali ambazo kitu au matokeo ndio msingi wake. Proposisheni ya hali huwa na sehemu mbili kuu: Sehemu hizo ni **mada** na **maoni**. Tukianza na **mada,** hii ni dhana itakayozungumziwa, ilhali **maoni** yahusu kitu au matokeo katika kueleza mada na uhusiano katika hali yake.

Kwa mfano: 2.10: '*Kitabu ni cha Peter.*'

Mada ni **kitabu** na chahusishwa na dhana **Peter** kwa uhusiano wa kuwa **Peter** anakimiliki **kitabu** kile. Kwa mintarafu hii Peter ndiye mwenye kitabu.

Proposisheni za hali huelezwa kwa kitenzi cha kuwa ***ni.*** Kama vile:

| ***Proposisheni ya hali;*** | ***Maelezo;*** |
|---|---|
| **Gari** ...*umiliki*... **mimi** | *gari ni langu.* |
| **Mbwa** ...*jina*... **fido** | *Jina la mbwa ni fido.* |
| **Msimamizi** ...*kitambulisho*... **Bwana John** | *Msimamizi ni Bwana John.* |
| **John** ...*mahali* ...**nyumba** | *John yumo nyumbani.* |
| **John** .. *maelezo*...**mkubwa** | *John ndiye mkubwa.* |

Maana ya proposisheni yaweza kuwa katika matumizi. Mzungumzaji anaweza kuuliza swali, kutoa arifa au kuamrisha. Proposisheni huwa ni moja lakini matumizi tofauti.

Kwa mfano: 2.11:

**Maana elekezi :** *John* ... **mtenda** ... *aliupiga* ... **mwathiriwa** ... *mpira*

**Arifa :** *John alipiga mpira.*

**Swali :** *Je, John alipiga mpira?*

**Amri :** *John, piga mpira!*

Maana elekezi haibadiliki lakini matumizi huwa ni tofauti katika kila proposisheni. Matumizi hayo yapo katika proposisheni za matukio na vilevile katika proposisheni za hali, ambayo hujulikana kama misukumo ya kiilokusheni katika proposisheni. Sentensi sahihi, mfuatano wa maneno na uakifishaji ni mambo ambayo huonyesha msukumo wa kiilokusheni katika proposisheni. Mara nyingi kiimbo huonyesha msukumo wa kiilokusheni katika mazungumzo.

Kwa mfano: 2.12:

1) Proposisheni ya hali ambayo inaamrisha: **Uwe hapa karibu!**
2) Proposisheni ya hali ambayo yauliza: **Je, Maria ni dadake?**
3) Proposisheni ya hali ambayo yaarifu: **Mbwa yumo katika chumba chake.**
4) Proposisheni ya tukio ambayo yauliza swali katika kufanyika: **Je, maziwa yaliganda?**
5) Proposisheni ya tukio ambayo yaonyesha tendo la kuamrisha: **Wewe, kimbia haraka!**
6) Proposisheni ya tukio ambayo yatoa arifa katika tajriba: **Tulisikia sauti.**

Msukumo wa kiilokusheni waweza kuonyeshwa kwa mfuatano wa maneno, viambishi au maneno na huibuka hasa kupitia kwa dhamira. Matumizi ya proposisheni ni muhimu katika kuleta maana kwa sababu mtu huenda asifahamu maana iliyokusudiwa na msemaji.

Kwa mfano: 2.13:

**Tukio** – *kula*, **mtenda** – *chui*, **mwathiriwa** – *msafiri* .

Katika mfano 2.13; maana haiwezi kueleweka ila msemaji afafanue lile jambo analolitamka kuwa sentensi yenyewe ni Arifa: Kama vile; **Kauli:** '*Chui alimla msafiri*' au ni sentensi ya kutaka kuhakikishiwa jambo: Kama vile; **Swali:** '*Je, chui alimla msafiri*?'

Jinsi msemaji anavyosema jambo huchangia katika kuelewa maana. Kuna wakati ambapo msemaji hutaja msukumo wa kiilokusheni.

Kwa mfano: 2.14: **Nenda** – *Nakuamrisha uende*! ***Amri***.

**Alikwenda** – *Nasema kuwa alikwenda*: ***Arifa***.

**Kwa nini alikwenda**? – *Nauliza ni kwa nini alikwenda?*: ***Swali***.

Arifa hukusudia kumpa msikilizaji ujumbe. Swali hukusudia kumpa msikilizaji ujumbe kutoka kwa msemaji, ilhali amri hukusudia kutoa sheria itakayofuatwa na msikilizaji. Kama vile: **Nakuamrisha**, **nasema** na **nauliza** ni proposisheni tendaji kwa sababu huonyesha kitendo kinachofanyika, yaani ni maana iliyopo katika proposisheni, ili mawasiliano yaweze kufaulu.

Maana ya proposisheini hujumlisha maana kadiri ya vitendo katika kishazi.

Kwa mfano: 2.15: "*Jengo refu ambalo ni adhimu lilianguka*". Yadhihirisha proposisheni kuwa:

1) **Jengo ni refu**.
2) **Jengo ni adhimu**.
3) **Jengo lilianguka**.

Katika Kiswahili, kila mojawapo ya kauli hizi zifuatazo ni proposisheni.

Kwa mfano: 2.16: '*Alex alikula ndizi*.'

'*Ndizi ililiwa na Alex*.'

'*Je, Alex, alikula ndizi*?'

Matamshi yaliyo katika 2.16, yaweza kuchanganuliwa kuwa na kiarifu kinachotaja kundi au hali na mijadala kadha na wahusika katika tukio au hali fulani. Shughuli ni ya kula. **Mtenda** ni *Alex*. **Mtendwa** ni *ndizi*.

Proposisheni ya uhusiano huzua maana ya umaanisho kati ya proposisheni mbili au makundi ya proposisheni ambayo yahusiana katika mwingiliano wa kiproposisheni ulipo katika kauli. Huleta uamuzi na mshikamano mkubwa kuhusu yaliyozugumzwa.

Kwa mfano: 2.17: "*Nina njaa. Twende Westlands*". Kauli hii ina proposisheni kuwa:

1) **Msemaji anahisi njaa.**

2) **Msemaji anaonelea waende Westlands wapate chakula.**

Uhuasiano wa proposisheni hizi mbili ni kuwa kuna suluhisho la njaa na jinsi ya kusuluhisha. '*Kwenda kwetu Westlands*' ni sehemu ya suluhisho la tatizo langu kuwa '*naona njaa*'.

Leech (1974:18-23), anasema kuwa hisia za mtu binafsi huwepo kama zinazomhusu mtu anayepokea ujumbe au kuhusu kitu fulani zitabainika wazi. Maana hisivu yaweza kuibushwa na proposisheni.

Kwa mfano: 2.18: "*Samahani kwa kuwakatiza mazungumzo yenu lakini, ni vyema kama mngepunguza sauti zenu*".

Msemaji wa kauli hii alikuwa ana hasira kwa sababu ya kelele kutoka kwao, kisha alijaribu kuwa mpole katika kuwaambia kuwa sauti zao za juu hazimfurahishi kamwe. Vilevile, proposisheni yaweza kuzua maana katika dhamira. Jinsi mzungumzaji anavyoupanga ujumbe wake katika mpangilio wake wa maneno na kusisitiza jambo.

Kwa mfano: 2.19: (A)

1) *'Bi Smith alifadhili tuzo la kwanza'*.

2) *'Tuzo la kwanza lilifadhiliwa na Bi. Smith'*.

Sentensi ya kwanza ni katika kauli tendi ilhali sentensi ya pili ni katika kauli tendwa.

Kwa mfano: 2.20: (B)

1) *'Ndugu yangu amemiliki duka lililo kubwa zaidi mjini Nairobi'*.

2) *'Duka lililo kubwa zaidi katika mji* wa *Nairobi limemilikiwa na ndugu yangu'*.

Maana ni tofauti kulingana na kauli zilizotumika, kulingana na mpangilio wa maneno na msisitizo. Mfano 2.20; (A), sentensi ya kwanza ina proposisheni kuwa Bi.Smith ni mtu mabaye ni muhimu sana ili ufadhili wa tuzo la kwanza uwepo, sentensi ya pili ina proposisheni kuwa tuzo la kwanza ni lenye umuhimu na sio lazima lifadhiliwe na Bi. Smith, mbali pia mtu mwingine yeyote anaweza kufadhili. Mfano 2.20; (B), sentensi ya kwanza ina proposisheni kuwa ni ndugu yangu aliye na uwezo wa kumiliki lile duka kubwa zaidi mjini Nairobi, ilhali katika sentensi ya pili mtu mwingine yeyote isipokuwa ndugu yangu hana uwezo wa kumiliki duka kubwa zaidi mjini Nairobi.

## 2.2 AINA ZA PROPOSISHENI

Fleming (1988:53-57) anasema kuwa proposisheni ni za aina tatu ambazo ni: **Proposisheni ya hakika, proposisheni ya thamani** na **proposisheni** ya **sera**. Sehemu hii inadhamiria ama kuorodhesha aina za proposisheni. Inafuatwa na mjadala kuhusu aina hizi za proposisheni na hatimaye tutatoa mifano kwa kila mojawapo. Proposisheni ambazo tutazichanganua ni kama zifuatavyo:

### 2.2.1 PROPOSISHENI YA HAKIKA

Proposisheni hii ni tamko ambalo hulenga hasa katika imani ya msikilizaji, kama ni ya kweli ama ni ya uongo. Jinsi itakavyojadiliwa ndivyo itakavyoibua namna msikilizaji atakavyoichukulia kuwa ni ya kweli au uongo. Mfano huu hapa chini utatoa mwangaza zaidi.

Kwa mfano: 2.21: '*Vyuo vikuu vyote hupatikana mjini*'.

Tamko hili litategemea jinsi msemaji atakavyoinshawishi msikilizaji. Kama msikilizaji hana mfano wowote wa Chuo Kikuu anachokijua kuwa mjini, basi atakubali kuwa proposisheni hii ni ya kweli, lakini kama anakijua Chuo Kikuu chochote ambacho hakimo mjini basi kwake proposisheni hii itakuwa ni ya uongo. Proposisheni katika 2.21, ni:

1) **Msemaji anamaanisha kuwa vyuo vikuu havipo mahali pengine ila katika miji tu.**
2) **Huenda ikawa msemaji anataka kumsawishi msikilizaji kuwa kauli hii ni ya kweli.**
3) **Labda msikilizaji hana ufahamu wa kutosha kuhusu vyuo vikuu.**

Vilevile, katika mfano mwingine unaoafikiana na huu.

Kwa mfano: 2.22: '*Wanaume wote ni wabaya*'.

Kauli kama hii itategemea mtazamo wa watu mbalimbali. Kuna wale wanao amini ilhali wengine wanakataa. Pia itategemea ushawishi kutoka kwa msemaji kuhusu tajriba yake ikilinganishwa na tajriba aliyonayo msikilizaji kuwahusu wanaume, kisha ataweza kuamua kauli kama hii ina jambo ambalo ni la kweli au la ni jambo la uongo. Huenda ikawa msemaji amekabiliwa na janga fulani lililo sababishwa na mwanamume ilhali, msemaji hajawahi kupatwa na jambo lolote baya kutoka kwa mwanamume yeyote.

Proposisheni katika 2.22, ni kuwa:

1)**Msemaji anajumlisha wanaume wote kuwa ni wabaya.**

2)**Msemaji labda ana sababu ya kusema jambo hili.**

**3)Msemaji anonekana kuwa na hasira.**

## 2.2.2 PROPOSISHENI YA THAMANI

Proposisheni hii ni tamko ambalo msemaji hutoa ili kutaka kupata maoni ya kutathmini kama tamko lake ni nzuri kimaadili au la, ni sawa au si sawa. Msikilizaji hasa hulinganisha vitu viwili na kuuliza ni kipi kilicho bora zaidi.

Kwa mfano: 2.23: '*Kuna mwanafunzi anayekula darasani, ilhali wengine wanamsikiliza mwalimu'*.

Proposisheni katika 2.23, ni kuwa:

1) **Kuna wanafunzi walio darasani.**

2) **Kuna mwalimu ambaye anafunza katika darasa hilo.**

3) **Mwalimu anapofunza kuna mwanafunzi mmoja ambaye yuala katika darasa hilo.**

Kauli hii itategemea maoni ya msikilizaji ambaye katika proposisheni anayoifahamu ni maadili mema kumsikiliza mwalimu darasani badala ya kula. Mwanafunzi anafahamu kuwa si sawa kula darasani kama mwalimu anafundisha, lakini labda analifanya jambo hili kwa kusudi fulani. Hivyo basi, wasikilizaji wataamua ni jambo lipi lililo bora zaidi ya lingine. Vilevile, mfano mwingine wenye kueleza jambo lililo sawa na hili.

Kwa mfano: 2.24: '*Kuna mtu anayepiga gumzo kanisani ilhali Padre anahubiri.*'

Proposisheni katika 2.24, ni kuwa:

1) **Kuna wakristo walio kanisani kwa ibada.**

2) **Kuna mtu mmoja ambaye anazungumza ndani ya kanisa.**

3) **Padre anaendelea na shughuli ya ibada huku mtu fulani akipiga gumzo.**

Vilevile kauli kama hii itategemea maoni ya washiriki katika mjadala kama huu. Watu wasio mcha Mwenyezi Mungu hawataliona kuwa ni jambo baya kufanya kitendo kama hiki. Kwingineko, wanaomheshimu Mwenyezi Mungu watachukulia kuwa ni dhambi. Hivyo basi, ubora wa tendo kama hili utategemea mitazamo ya watu walio na tajriba tofauti kuhusu maisha.

### 2.2.3 PROPOSISHENI YA SERA

Proposisheni hii ni tamko ambalo hutoa mawazo kuhusu jambo litakalofanywa kama hatua ifaayo. Msikilizaji hupaswa kupitisha sera mwafaka au kujitolea kwa tendo maalum.

Kwa mfano: 2.25: '*Mtu yeyote atakayepoteza kitabu alichokiazima atanunua kingine*'.

Kauli hii ni kulingana na sera iliyopangwa na wahusika. Hivyo basi, kauli 2.25, ina proposisheni kuwa:

1) **Kila mmoja wao amekubali tendo maalum la kununua kitabu atakachokipoteza.**
2) **Kuna vitabu ambavyo huazimwa mahali pale.**
3) **Kuna masharti fulani ambayo ni lazima yazingatiwe kuhusu kitabu kilichoazimwa.**

Vilevile, hakuna mtu yeyote ambaye ataepuka hatua hii kwa sababu yajumlisha watu wote. Kwingineko, katika mfano : 2.26: '*Mwanafunzi yeyote atakayechelewa kuwasili shuleni atarudi nyumbani.*'

Proposisheni katika 2.26, ni kuwa:

1) **Mahali pale ni shuleni.**
2) **Kuna wanafunzi ambao huhudhuria shule ile.**
3) **Kuna sheria fulani ambazo lazima zizingatiwe kuhusu kuchelewa shuleni.**

Sera iliyopo katika shule hii na baadhi ya shule ni kuwa mwanafunzi yeyote anapaswa kuwasili shuleni kabla ya wakati uliowekwa kama sheria au mara tu wakati huo unapowadia. Atakayefanya kinyume na haya basi ataadhibiwa kwa kuambiwa arudi nyumbani ilhali, wenzake wataendelea na masomo siku hiyo. Hakuna mwanafunzi yeyote ambaye ni bora zaidi ya wengine kuwa hataadhibiwa.

## 2.3 ISHARA ZA PROPOSISHENI NZURI

Proposisheni nzuri yapaswa **kujadilika** na vilevile **kuthibitika**. Ili proposisheni itambulike kuwa bora, basi yapaswa kutimiza mambo haya mawili. Kujadiliwa au kukubaliwa kwa proposisheni ni jambo ambalo litakalotegemea maoni ya watu tofauti tofauti na msukumo walio nao hasa wa kimamlaka, kulihusu jambo hilo na uwezo wao wa kuwasawishi wasikilizaji. Pia proposisheni nzuri yapaswa kuwa na masharti ya kweli au uongo, kisha thamani iliyopo katika proposisheni hiyo ili ifahamike kama ni nzuri au la.

### 2.3.1 PROPOSISHENI NZURI YAPASWA KUJADILIKA

Mjadala wake ni muhimu ili mambo husika yakubalike au yakatalike katika proposisheni. Msemaji humhimiza msikilizaji katika mjadala dhidi ya proposisheni. Proposisheni kama zitakataliwa au kukubaliwa, ukweli utakubalika hata kama hautathibitika na wanaoshiriki katika mazungumzo. Kwingineko uongo utabaki kuwa si kweli hata kama tutasawishika kuukubali.

Kwa mfano: 2.27: '*Nchi ya Kenya ni yenye ufisadi*'.



UNIVERSITY OF NAIROBI
LOWER KABETE LIBRARY

Kauli 2.27, ina proposisheni kuwa:

**1) Kuna nchi fulani iitwayo Kenya.**

**2) Nchi hiyo huwa na ufisadi.**

Ufisadi wa Kenya ni suala linaloweza kujadiliwa kisha likakubaliwa au kukataliwa. Kwingineko, wanaoshiriki katika ufisadi watashikilia msimamo kuwa hakuna hatia yoyote katika ufisadi kwani ni njia mojawapo ya kujisaidia katika umiliki mali kwa kuwanyanyasa wengine. Kisha, wanaonyanyaswa kupitia kwa ufisadi watahisi kuwa ni jambo ovu na wanapaswa kukabiliana nalo ili kulimaliza haraka iwezekanavyo. Huenda ikawa walio na uwezo watazidi kuwanyanyasa walio wanyonge.

### 2.3.2 PROPOSISHENI NZURI YAPASWA KUTHIBITIKA

Ukweli wa kauli ni muhimu ili kuthibitisha ukweli wa proposisheni ipasavyo. Uongo wa proposisheni kama hauwezi kuthibitishwa basi vilevile, hata ukweli wake hauwezi kuthibitishwa.

Kwa mfano: 2.28: '*Kunanyesha'*.

Kauli ya 2.28, ina proposisheni kuwa:

**1) Msemaji huenda ikawa ametazama nje na kuona kuwa kunanyesha.**

**2) Pengine kuna mingurumo ya radi na matone ya mvua yanayoanguka.**

Ni jambo ambalo laweza kuthibitishwa kuwa ni kweli au ni uongo, kwa kutazama nje au kwa kuzingatia yaliyotajwa na wanaotangaza kuhusu hali ya anga. Mfano mwingine ni kuwa: 2.29: '*Yesu Kristu atarudi tena'*. Proposisheni katika 2.29, ni kuwa:

**1) Msemaji ni muumini wa dini ya kikristo.**

**2)Msemaji huyasikiliza mahubiri ya injili.**

**3)Msemaji ana imani kwa Yesu Kristo.**

**4)Msemaji anaamini kuwa Yesu Kristo atarudi.**

Kauli kama 2.29; haiwezi kuthibitika kuwa ni ya ukweli au uongo kwa sababu yategemea imani ya watu hasa kutoka dini tofauti. Hivyo basi, ni vigumu kuthibitisha kuwa ni ya kweli au si ya kweli.

Akmajian na wenzake (2004: 254) wanasema kuna proposisheni ambayo huelcza jambo moja maalum na pia kuna proposisheni ambayo huelezwa kwa ujumla wake. Proposisheni ya jumla yaweza kufanywa ya kweli na mambo tofauti.

Kwa mfano: 2.30: '*Nakuahidi kuwa nitafika.*'

Proposisheni hii itakuwa ya kweli kama nitatimiza ahadi yangu na kufika. Itakuwa ya kweli pia kama ni mimi nitakaye timiza jambo hilo na wala sitamtuma mtu mwingine. Proposisheni inayoeleza jambo moja maalum, hulenga jambo mahususi na mtu fulani mahususi.

Kwa mfano: 2.31: '*Neil Armstrong ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kufika katika maeneo ya mwezi*'.

Proposisheni hii ni ya kweli kwani ni jambo linalojulikana kuwa lilitendeka na limo katika hifadhi.

Leech (1969:39-40), anasema kuwa kuna proposisheni mbili maarufu kama; **mzunguko** na **ukinzani**. **Mzunguko** ni aina ya proposisheni ambayo ni ya kweli kulingana na yanayojadiliwa katika jambo linalodokezwa.

Kwa mfano: 2.32: '*Wavulana hukimbia shuleni'*.

Proposisheni katika 2.32, yadokeza kuwa:

1) **Wavulana huenda shuleni.**

2) **Hivyo basi inathibitika kuwa wao hukimbia kuelekea shuleni.**

3) **Wavulana ambao hukimbia shuleni huenda shuleni.**

Ina maana kuwa ni wavulana wote, wala sio baadhi yao au mmoja maalum. Proposisheni nyingine huwa na madai ambayo yamefanana, nyingine madai yaliyopatana kwa jinsi mambo fulani yaliyofasiriwa na nyingine huwa na madai yanayofuata mantiki ili kupata wazo la ujumla au pia muungano.

Kwa mfano: 2.33:

1) *'Watu ambao wana bahati wana bahati'*. – **kufanana.**

2) *'Wenye magari humiliki magari'*. - **Yafuata mantiki.**

3) *'Mawazo yanayofaa watu huwafaidi wanasayansi'*. - **Yafuata ufasiri wa jambo.**

4) *'Tufaha hupendwa na watoto ambao ni wa matajiri'*. – **Yafuata mantiki pamoja na ufasiri wa jambo.**

**Ukinzani** ni aina ya proposisheni ambayo ni ya uongo kulingana na yanayodaiwa katika jambo lililodokezwa.

Kwa mfano: 2.34:

1) *'Kunanyesha na hakunyeshi'*.

2) *'Nduguye John mdogo ni mkubwa kwake kwa umri'*.

Proposisheni hizi zina ukinzani kwa sababu haiwezekani kuwa jambo moja litatendeka na kinyume chake kwa pamoja. Maana ya umbo la kimantiki italingana na mfumo wa mantiki utakaoshughulikiwa. Vilevile, proposisheni hizi zikielezwa kwa upana zaidi zitarejelea

maeneo tofauti. Kwa mfano: 2.35: '*Kunanyesha Embu na hakunyeshi Nairobi'*. Hivyo basi' itakuwa hakuna ukinzani tena. Katika proposisheni kuna ukweli ulio na mantiki ambao pia ni ukweli ulio changanuzi ambao ukweli wake hutegemea maana yake.

Kwa mfano: 2.36:

1) '*Kapera huyu hajaoa'*. - **mzunguko.**
2) '*Kapera huyu ameoa'*. – **ukinzani.**

## 2.4 PROPOSISHENI KATIKA MISINGI YA KWELI AU UONGO

Cambridge (2008: 1563-1564), wanasema kuwa ukweli ni jinsi ya ubora uliopo katika jambo lililo la kweli. Ni uhakika uliopo kuhusu hali, tukio au mtu. Husisitiza kuwa jambo ni la kweli, au ni hali ya kuwa katika ukweli. Cambridge (2008: 509), wanaendelea kusema kuwa uongo ni jambo lisilo halisi lakini hufanywa kuonekana kuwa kweli ili kuhadaa watu. Vilevile, kusema uongo kuhusu jambo, ni sawa na kusema jambo lisilo sahihi, lililo kataliwa au lisilo aminika.

Wilson (1967: 76-79) anasema kuwa proposisheni ni ya kweli kama itatimiza mambo yafuatayo:

1) **Mtu anafahamu maana ya jambo liliosemwa.**
2) **Mtu awe na njia mwafaka ya kuthibitisha jambo lililopo katika proposisheni.**
3) **Mtu awe na ushahidi unaofaa ili aweze kuliamini jambo hilo.**

Kwa mfano: 2.37: '*Ni kweli kuwa dunia ni mviringo'*.

Kama mtu hafahamu maana katika kauli hivyo basi, hawezi kuthibitisha kuwa ni ya kweli au la. Vilevile, kama mtu hana ushahidi wa kutosha kuhusu jambo, basi itakuwa vigumu

kuthibitisha kuwa kauli hii ni ya kweli. Ni bora kuhakikisha kuwa kila mtu anafahamu maana ya kauli hii na njia mwafaka ya kuthibitisha kisha wanasayansi watafanya utafiti wao ili kuwa na ushahidi thabiti.

Kauli za aina tofauti hueleza mambo kadha kuhusiana na ukweli au uongo wa jambo fulani. Kama vile:

1) **Kauli za kuamuru na za mtazamo.**

2) **Kauli chambuzi.**

3) **Kauli za thamani.**

4) **Kauli dhanifu.**

## 2.5 AINA ZA KAULI

Fleming (1988:59-63) anasema kuwa kuna aina nne za kauli. Aina hizi ni kama zifuatazo: **Kuamuru** na **mtazamo, chambuzi, thamani** na **dhanifu.** Kauli hizi tutazijadili kwa kuzieleza maana zake kisha kuzitolea mifano mwafaka kwa kila mojawapo ya aina hizi, ambayo itafafanua zaidi lengo la kauli zenyewe katika mawasiliano. Madhumuni ya kauli hizi hasa ni kumpa msikilizaji athari fulani baada ya kuzisikiza na mwishowe kuzifasiri kama ilivyo kusudiwa.

Kwanza, kauli za **kuamuru** na **mtazamo** ni zile ambazo hutoa amri au hueleza mambo yanayomhusu msemaji kama; ***matumaini*** au ***analolitamani***.

Kwa mfano: 2.38:

1) '*Tumikia Mungu na umheshimu Mfalme.*'

2) '*Tupendane sote kama ndugu.*'

Kauli kama za 2.38, hazina kusudi la kuwa ni za kweli au uongo kwani hasa zaeleza mitazamo ya watu kuhusu mambo fulani. Hivyo basi, mtu anaweza kugairi na kukosa kumtumikia Mungu na kutomheshimu vilevile. Pia, ana hiari ya kutopenda wengine kama ndugu. Kauli hizi hueleza jambo kuhusiana na mtazamo wa mzungumzaji na wala sio jambo la hakika.

Kwa mfano: 2.39: '*Wanaume wote ni sawa.*'

'*Wanaume wote ni huru.*'

Ili kuthibitisha kauli hizi, itabidi kutazama mambo yote ya kijumla katika wanaume, kama vile; ***urefu*** na **werevu** kisha kuchunguza mambo haya kama ni sawa. Vivyohivyo, ni jambo ni bora kubainisha ni jambo lipi litakalosababisha wao kuwa huru. Kama, mwanamume amepewa hadhi ya juu katika jamii, kuwa yeye ndiye atakayefanya uamuzi wa mambo yote katika familia basi, mwanaume atkuwa anao uhuru wa kufanya lolote alitakalo. Ujumbe waweza kupashwa kupitia kwa kauli ambapo itakuwa muhimu kufahamu ujumbe wenyewe ni wa aina ipi, na jinsi ya kuweza kutambua na kuwa na ushahidi kama jambo ni la kweli au la. Kwa mfano: 2.40: '*Mungu ni Baba yetu anaye tupenda.*'

Kauli kama hii yaweza kuwa ni ya mtazamo ambayo itamaanisha kuwa:

**1) Tunapaswa kupendana sote kama ndugu.**

**2) Tushukuru kwa mambo mema katika maisha yetu.**

Kauli 2.40, hatuwezi kuithibitisha kuwa ni ya kweli au ya uongo, kwa sababu ukweli wake au uongo wake utategemea mtazamo wa mtu binafsi. Kauli za majaribio ni zile ambazo huwa na ujumbe kuhusu dunia kwa misingi ya tajriba za watu tofautitofauti katika dunia.

Kwa mfano: 2.41: 1) '*Mji wa London umo nchini Uingereza.*'

2) '*Dunia huzunguka jua.*'

Jambo lenye uhakika huelezwa kwa kauli hizi na tunaweza kuamua kuwa ni za kweli au za uongo. Kunao uhakika wa kauli.

Kwa mfano: 2.42: '*Jua litachomoza miale yake kesho.*'

Uwezekano uliopo ni kuwa watabiri wa hali ya anga walitabiri kuwa siku itakayofuata kutakuwa na jua. Vilevile, huenda jua likose kuchomoza, kwani Labda hali ya anga yaweza kubadilika. Kwingineko, tunaweza kuwa na jambo ambalo laweza kuhakikishwa.

Kwa mfano: 2.43: '*Wanaume wote ni binadamu*'. Hii ni kauli ya kweli kabisa kwa sababu jina **mwanaume** ni la kiumbe ambaye ni binadamu. Hata hivyo hili ni jambo linalojulikana wazi na watu wote kuwa wanaume wote ni binadamu. Tunapaswa kufanya uchunguzi fulani, ili kuthibitisha baadhi ya kauli.

kwa mfano: 2.44:

**1)** '*Kutanyesha kesho.*'

**2)** '*Shangazi ni mgonjwa.*'

Katika kauli ya kwanza, kipimahewa chaweza kutumika ili kuthibitisha jambo hilo kuwa kutanyesha kesho. Katika kauli ya pili, shangazi atafanyiwa uchunguzi wa maabara hospitalini ili kuthibitisha ugonjwa wake ni upi. Kabla ya kuthibitisha kauli za 2.44, kupitia kwa uchunguzi, basi zitakuwa tu ni kauli zenye uwezekano wa kuwa kweli na baadaye zitathminiwe kuwa ni za kweli au za uongo.

Pili, kauli **chambuzi** ni zile ambazo baada ya kutathminiwa huwa za zingatia kanuni fulani za kimantiki. Kauli hizi hazina ujumbe kuhusu mambo ya ulimwengu na wala haziwezi kuthibitishwa kupitia kwa tajriba ya mtu.

Kwa mfano: 2.45: '*Chochote ambacho ni chekundu kina rangi.*'

Kauli yenyewe yaeleza kuhusu **wekundu**, kuwa ishara ya rangi nyekundu kama itatumika basi itabidi kutumia rangi ambayo ni nyekundu kwa kuerejelea kifaa kilekile kimoja.

Kwa mfano: 2.46: '*Taa za trafiki huwa ni rangi nyekundu, rangi ya machungwa* na *rangi* ya *kijani kibichi'*.

Hivyo basi, katika kuzichora rangi mwafaka zitatumika katika kuwakilisha kila rangi. Vilevile' katika mfano mwingine: 2.47:

1) '*Kuanguka kwa kitu fulani humaanisha kuelekea chini, kama kitu kitaanguka kuelekea juu, basi jambo hilo haliwezekani kamwe, kwani* ni *jambo ambalo ni kinyume cha kawaida ya mambo.*'

2) '*Nina tufaha mbili katika mkono wa kulia na tufaha mbili katika mkono wa kushoto.*'

Kauli ya kwanza katika 2.47, ina habari za kisanyansi ambazo zimetafitiwa na kuthibitishwa kuwa kila kitu huanguka kuelekea chini. Kauli ya pili katika 2.47, yatufahamisha kuwa ninazo tufaha nne, kwani tunafahamu kuwa katika majaribio, mbili kuongeza mbili ni nne.

Tatu, kauli za **thamani** ni zile ambazo hutumia maneno kwa sababu ya kutathmini au kuependekeza jambo fulani.

Kwa mfano: 2.48:

1) '*Ni mtu mzuri.*'

2) '*Haupaswi kufanya hivyo.*'

3) '*Ni sawa kuwaua wauaji.*'

Vigezo vya kutathmini vitategemea uamuzi wa mtu binafsi kuwa kitu ni chenye thamani au la. Uamuzi huu utategemea vigezo kama mtu ni mwaminifu, mkarimu, mwenye ujasiri, mwenye uwazi katika kusema na kutenda mambo.

Kwa mfano: 2.49: '*Maria ni mwanamke mzuri.*'

Mtu fulani kumpendekeza Maria kuwa ni mzuri labda vigezo vilivyo hapo juu vilitathminiwa na kuwa vimo katika tabia za Maria. Tunapata mtazamo kuwa yeye ni mwanamke mzuri.

Ithibati katika kauli za thamani itategemea tajriba za watu au maarifa kuhusu uhakika wa jambo na vilevile vigezo vya thamani.

Kwa mfano: 2.50: '*Kuna wale watakaokuwa na vigezo tofauti vya kumtathmini Maria na kwa wao Maria atakuwa mwanamke mbaya.*'

Huenda hawakuuona ubora wowote katika tabia za Maria, hivyo kupingana na kauli kuwa Maria ni mzuri. Kwingineko, katika kueleza mifano mingine inayoafikiana na iliyopo hapo juu ni kuwa: 2.51: '*Serikali yetu ni nzuri.*'

Kauli hii pia italenga vigezo ambavyo vitatumika kuitathmini serikali yetu, kama vile: '**Ukarabati wa barabara, elimu ya bure kwa shule za msingi na za upili.**' Vigezo hivi vikitumika, basi tutaipa serikali yetu thamani kwa mtazmo wa kuisifu, na kama vigezo tofauti vitazingatiwa, kama vile: '**Ufisadi** na **unyanyasaji wa wafanyikazi,**' tutapata kuwa tunaipa serikali yetu kashfa na kukosa thamani ya kuisifu.

Nne, kauli **dhanifu** ni zile ambazo uthabiti wake utategemea mambo ambayo yatachukuliwa kuwa ni ya kufaa. Mambo haya ni yale ambayo hayajakubaliwa lakini yanaweza kujadiliwa kuwa yatakubaliwa au la. Hueleza mambo ambayo si ya kawaida katika ulimwengu na ambayo ni ya kumiujiza. Kauli nyingi dhanifu hupatikana katika mambo ya kidini. Hata hivyo, kuna kauli dhanifu ambazo hazina uhusiano na mambo ya kidini na hasa zimo katika **mambo kamilifu**, kama vile: **Haki**, **urembo**, na **ukweli**. Pia, kauli za **ubinafsi** na **hiari**.

Kwa mfano: 2.52: '*Mungu atawaokoa walio waadilifu.*'

Watu watajadili kuwa kauli hii ni sawa au si sawa, ni kweli au ni uongo. Kauli dhanifu inapaswa kukubalika kimaana na kudhibitiwa ili kuwasiliana kuhusu mambo yaliyomo katika ulimwengu wa kawaida na usio wa kawaida.

Kwa mfano: 2.53: '*Ni jukumu la mtu binafsi kulichagua alitakalo maishani.*'

Kauli hii yaeleza kuwa binadamu ana hiari ya kulichagua jambo alipendalo kulizingatia yeye bila kushurutishwa na mtu yeyote kulifanya asilolitaka.

Kwa mfano: 2.54: '*Kila mzazi anapaswa kumwelimisha mwanawe.*'

Kulingana na kauli hii ni haki ya kila mtoto kupata elimu ambapo kila mzazi anapaswa kugharamia kwa kulipa karo na mahitaji mengine ya kielimu.

Cornford (1957: 287- 290) anamnukuu Plato na kusema kuwa kulingana naye, chochote kilicho halisi hakina budi kuwa kweli, kwani si kitu kingine chochote bali ni kitu maalum kilicho halisi, kama vile: '**Mwendo kama kitu ambacho ni halisi.**' Kauli hii ina maana kuwa **mwendo** ni kusonga kwa kitu kutoka mahali kilipokuwa na kupiga hatua fulani hadi mahali pengine. Hivyo basi, kwa kuzingatia kauli hii kuhusu mwendo tutatoa mifano kuwa:

2.55: 1) '*Mwendo ni kitu ambacho hakipo.*'

2) '*Mwendo ni kitu ambacho kipo.*'

Kulingana na kauli za 2.55, ya kwanza si ya kweli kwa sababu mwendo ni kitu ambacho kipo ilhali kauli ya pili ni kweli kwani yasema kuwa kipo, ni jambo la kweli na hutendeka. Msemaji anatafakari kuhusu kauli ambazo ni za uongo kama zina maana yoyote. Ni vigumu kwa mtu kuzungumza mambo ambayo hayapo na ambayo mtu hana uhakika nayo. Hivyo basi, kauli zote ambazo si za kweli hazina maana yoyote.

Kwa mfano: 2.56:

1) '*Chuo* Kikuu *cha Nairobi kimo mjini Dar es salaam.*'

2) '*Rais wa Marekani ni mwanamke.*'

Kauli katika 2.56, ni za uongo kwa sababu, kama tunavyofahamu proposisheni tunazozipata kutoka kwa kauli hizi si kweli, kwani katika kauli ya kwanza, Chuo Kikuu cha Nairobi kimo mjini Nairobi nchini Kenya. Dar es salaam ni mji uliopo nchini Tanzania. Kauli ya pili, si ya kweli vilevile kwani Rais wa Marekani anayetawala kwa wakati huu ni mwanamume na wala si mwanamke.

Kauli ambazo ni za kweli huwa na:

1) **Jambo ambalo ni la kimsingi katika kauli hiyo.**

2) **Kitendo kinachoelezwa na kitenzi.**

3) **Mfumo wote unaohusika na kauli hiyo.**

Ni bora basi kuzungumza mambo yaliyohalisi na yaliyopo. Kauli ya kweli na ya uongo, vile vile huwa na kiima na kiarifu chake. Hivyo basi sio kwamba kauli ya uongo haizungumzii chochote hata kama haina maana yoyote, kwani ina kiima chake na kiarifu chake kama vile kauli ya kweli ilivyo. Uamuzi baina ya wanaowasilisha ujumbe na wanaopokea ujumbe ni

muhimu kwa sababu wanaweza kuamua kuhakikisha jambo lisilo la kweli likawa la kweli. Watafanya hivyo kwa kusisitiza kuwa ni kweli, ilhali wanajua kuwa ni uongo.

Linsky (1952:15-16) anasema kuwa ukweli katika sentensi wahusu ukubalifu wake katika uhalisi. Sentensi ni ya kweli kama itaweza kuthitibisha hali ya mambo yaliyopo kuwa ni ya kweli.

Kwa mfano: 2.57: '*Theluji ni nyeupe.*'

Tunapaswa kutafakari ni katika masharti yapi ambapo kauli hii ni ya kweli au ni uongo. Proposisheni hii basi ni ya kweli kama theluji ni nyeupe na ni ya uongo kama theluji si nyeupe. Hata hivyo, tunafahamu wazi kuwa ni kauli ya kweli kwa sababu sote tunajua kuwa theluji ni nyeupe. Ili kupata maelezo mwafaka ya ukweli ni vyema kuhusisha mawazo ya kisemantiki, kama vile; kukidhi mahitaji.

Kwa mfano: 2.58: '*Nchini mwetu elimu imetiliwa maana na asasi za mambo ya kielimu kuongezeka, ili kukidhi mahitaji ya kielimu.*'

Tumeelezwa hapo awali kuwa jukumu la kukidhi mahitaji ni muhimu katika semantiki. Hivyo basi mfano 2.58, unaeleza kuwa ni mahitaji ya kielimu ambayo hutimiza uchu wa binadamu kwani hutaka kupata elimu zaidi wakati wote. Kauli katika 2.58, ni ya kweli kwani yaeleza proposisheni kuwa:

**1) Elimu ni muhimu nchini mwetu.**

**2) Asasi za kielimu nchini zimeongezeka.**

Vilevile kauli 2.58, inakidhi mahitaji ya kielimu ambayo wananchi wengi nchini mwetu wanazidi kuyahitaji.

Kempson (1975: 33-34) anasema kuwa kauli yenye maana katika lugha asili ni kauli yenye masharti ya ukweli katika sentensi za lugha hiyo.

Kwa mfano: 2.59: '*Mtoto alikimbilia mamake.*'

Kauli 2.59, ina proposisheni kuwa:

1) **Aliyekimbia ni binadamu mwenye umri mdogo.**
2) **Amefanya kitendo cha kukimbia.**
3) **Ameelekea kwa mzazi wake ambaye ni wa kike.**

Hata hivyo, kauli hii yapaswa kutimiza masharti ili kudai ukweli uliopo katika kauli hiyo. Kauli ambayo inaeleza maana hubainisha kuwa kuna uwezekano wa sentensi hiyo kuwa ya kweli. Katika sinoniminia ambapo sentensi au maneno tofauti yatakuwa na maana sawa, basi masharti yake ya ukweli yatakuwa sawa, kwa hivyo kama sentensi moja ni ya ukweli, vilevile nyingine basi itakuwa ni kweli.

Kwa mfano: 2.60:

1) '*Msichana huyu ni mrembo.*'
2) '*Banati huyu ni mrembo.*'

Kauli hizi zina maana sawa kwa sababu msichana pia anaitwa Banati, kauli ya kwanza ni ya kweli, na ya pili vilevile ni ya kweli. Proposisheni zinazotokana na kauli hizi ni za kweli ambazo ni:

1) **Kuna msichana ambaye yumo mahali fulani.**
2) **Msichana mwenyewe ni mrembo.**
3) **Msichana kwa jina lingine pia huitwa banati.**

### 2.5.1 MAANA KATIKA SENTENSI

Fodor (1977:27-28) anasema kuwa ili kueleza maana ya sentensi ni vyema kuainisha uwezo wake katika ilokusheni na proposisheni zake. Hali za kauli tofauti huwa za kweli au za uongo. Mtu anapotoa kauli hujihusisha na ukweli uliopo katika proposisheni ili aweze kudai kuwa ni ya kweli. Vilevile, mtu anapofahamu kauli huelewa kuwa mzungumzaji anadai kuwa kitu ni cha kweli na kisha kukifahamu ni kitu kipi anachokidai kuwa ni cha kweli.

Kwa mfano: 2.61:

'*Kitabu hiki kitakufaa kwa marejeleo.*'

'*Sherehe hiyo ilikuwa nzuri sana.*'

Proposisheni katika 2.61, ni za kweli kama:

1) **Kitabu ni cha marejeleo wala sio cha kuandikia.**
2) **Kitabu chenyewe kina ujumbe hasa ninaohitaji kurejelea.**
3) **Sherehe ilikuwepo.**
4) **Sherehe yenyewe ilinipendeza mimi.**

Kama proposisheni zitakuwa hazitimizi mambo haya yanayodaiwa na kauli hizi, basi zitakuwa ni za uongo. Proposisheni katika sentensi mara nyingi hurejelea masharti ya ukweli katika kauli.

Palmer (1981:196) anasema kuwa chukulizi ya kimsingi katika sentensi au proposisheni huwa ni za kweli au uongo, lakini ukweli au uongo wake hutegemea mtazamo wa mtu binafsi. Sentensi ya kweli hueleza jambo kinagaubaga kama lilivyo.

Kwa mfano: 2.62: '*John anampenda Mary.*'

Kauli hii ni ya kweli ikiwa John anampenda Mary. Sentensi hii ina proposisheni kuwa :

1) **Kunaye msichana kwa jina Mary.**

**2) Kunaye mvulana kwa jina John.**

**3) Mvulana anampenda Msichana.**

Vilevile katika mfano mwingine unaoafikiana na huu:

2.63: '*Barafu huwa baridi.*'

Kauli 2.63, ni ya kweli kwa sababu sote tunajua kuwa barafu ni baridi kwa kuigusa na kuhisi kuwa ina baridi.

Kauli 2.63 ina proposisheni kuwa:

1) **Kuna kitu kwa jina barafu.**

2) **Barafu yenyewe huwa ni baridi daima.**

Proposisheni yapaswa kutimiza masharti fulani ili iwe ya kweli.

Kwa mfano: 2.64: '*Nguruwe wana mabawa.*'

Kauli hii ni ya uongo kwa sababu, sisi sote tunafahamu kuwa nguruwe hawana mabawa. Nguruwe ni aina ya mnyama na kawaida ya wanyama ni kuwa hawana mabawa. Hatahivyo, kuna Popo ambaye tunafahamu kuwa si ndege wala myama kwani ana mabawa hivyo kanafanana na ndege ilhali hujifungua wana kama mnyama. Hivyo basi, proposisheni katika kauli hii si ya kweli hasa kama inamrejelea Nguruwe aliyetajwa katika mfano. Kwa kiasi fulani kuna ukweli kuwa nguruwe ni mnyama, lakini kwa upande mwingine kuna uongo kusema kuwa nguruwe wana mabawa kwani hawana.

Kamau (2008:50-51), anasema kuwa masharti ya ukweli hutegemea muktadha wake katika matumizi. Mawasiliano hutumika na kueleweka hasa kupitia kwa proposisheni zake. Mtu akitumia lugha bila kuzingatia baadhi ya sheria za lugha hiyo, mawasiliano hayana matatizo.

Kwa vile; matamshi yanapaswa kuwa sawa na mpangilio wa maneno uwe na mantiki. Anaendelea kusema kuwa kulingana na wanaisimu masharti ya ukweli yanaweza kubainisha uhusiano uliopo baina ya sentensi yoyote ile na proposisheni yenye mantiki.

Kwa mfano: 2.65: 1) *'Karanja ni mrefu zaidi ya Kimani.'*

2) *'Kimani ni mrefu zaidi ya Maina.'*

Hivyo basi, ni wazi kuwa Karanja ni mrefu zaidi ya Maina kwa sababu Karanja mwenyewe ni mrefu zaidi ya Kimani ambaye pia ni mrefu zaidi ya Maina. Basi ni kweli kabisa kusema kuwa Karanja ni mrefu zaidi ya Maina.

Vilevile, katika mfano mwingine unaoafikiana na huu wa 2.65.

Kwa mfano: 2.66: 1) *'Njoki ni mrembo.'*

2) 'Utamuoa Njoki.'

Hivyo basi, ni bayana kuwa Njoki ni mrembo na ndiye utakaye muoa wewe kwa sababu ni msichana ambaye ni mrembo. Basi ni kweli kusema kuwa msichana mrembo ambaye utamuoa ni Njoki.

Akimajian na wenzake (2004:243-244) wanasema kuwa kauli katika lugha huwa na maana halisi na hueleza mambo ya kweli au uongo.

kwa mfano: 2.67 *'Watu wote ambao ni wagonjwa ni watu.'*

*'Gari lile lina rangi nyekundu, hivyo basi ni lekundu.'*

*'Baadhi ya watu ambao ni wagonjwa si watu.'*

*'Gari lile ni lekundu lakini halina rangi.'*

Kauli katika 2.67, zina proposisheni za kweli na za uongo. Kauli ya kwanza na ya pili ni za kweli kwa sababu watu watabaki kuwa watu hata kama ni wagonjwa. Vilevile, kama gari ni

lekundu basi lina rangi. Kauli ya tatu na ya nne ni za uongo kwa sababu watu wakiwa wagonjwa hawabadiliki kamwe, bali huwa ni watu daima hata wakipata afueni. Vivyo hivyo, haiwezekani kuwa gari lekundu halina rangi kwani tayari imeelezwa kuwa gari lenyewe lina rangi nyekundu.

Mahusiano ya kweli huwa na tabia zake ambapo tabia ya kimsingi ni kuwezesha jambo lingine kutendeka. Sentensi moja husababisha sentensi nyingine kuwa ya kweli ikiwa ukweli wa sentensi ya kwanza umehakikishwa kuwa upo. Vilevile, sentensi moja husababisha sentensi nyingine kuwa ya uongo kama uongo wa sentensi ya kwanza umehakikishwa kuwa upo.

Kwa mfano: 2.68: 1) '*John ni kapera.*'

2) '*John hajaoa.*'

Proposisheni iliyo katika kauli ya kwanza 2.68, yasababisha kuwepo kwa proposisheni katika kauli ya pili. Kapera ina maana ya mwanamume ambaye yumo katika umri wa kuoa lakini hajaoa. Kauli 2.68 zina proposisheni kuwa:

**1)Kuna mtu anayejulikana kwa jina John.**

**2)John mwenyewe hajaoa.**

**3)Kutooa kwa John kunamfanya yeye kuwa kapera.**

Hivyo basi, proposisheni zilizopo juu ni za kweli kwani kama John ni kapera basi hajaoa. Katika mfano mwingine unao ambatana na huu.

Kwa mfano: 2.69:

1) '*Sindano ni fupi mno.*'

2) '*Sindano haina urefu wa kutosha.*'

Ukweli uliopo katika 2.69 kauli ya kwanza wahakikisha ukweli kuwepo katika kauli ya pili. Kauli hizi zina proposisheni kuwa kama sindano ni fupi mno ni kweli kuwa haina urefu wa kutosha.

Fasold (2006:142) anasema kuwa maana katika sentensi ni proposisheni. Proposisheni ni wazo lililotimia, ni kauli ambayo yaweza kuwa ya kweli au uongo. Proposisheni ni ya kweli kama kiarifu chake kinaeleza sawasawa kinachorejelewa na kiima.

Kwa mfano: 2.70: '*Catherine Ndereba alikimbia kwa kasi na kushinda mbio hizo.*'

Kauli 2.70 ina proposisheni kuwa:

**1)Kuna mwanariadha kwa jina Catherine Ndereba.**

**2)Mwanariadha mwenyewe alikimbia kwa kasi sana.**

**3)Mwanariadha huyo alijipatia ushindi katika mbio hizo alizoshiriki.**

Mwanariadha kwa jina la Catherine Ndereba ambaye alikimbia kwa kasi, kisha akawa mshindi katika mbio hizo alizoshiriki, itakuwa ni ya kauli ya kweli kama alishiriki katika mbio hizo na kushinda, ilhali itakuwa ni ya uongo kama hakushiriki kamwe katika mbio hizo. Masharti ya ukweli ni muhimu kwani huunganisha jambo analojifunza mtu na jambo linalosemwa, kwa sababu nikitoa kauli kama niliyoitaja hapo kumhusu Catherine Ndereba huna budi kuamini kuwa ni mwanariadha na aliwahi kuwa mshindi katika mbio alizoshiriki.

Fretheim (2000:39-40) anasema kuwa kauli hukusudia kumfahamisha msikilizaji ujumbe alio ukusudia msikilizaji na kuwa anao uhakika fulani kuhusu proposisheni itakayofahamika kupitia kwa kauli aliyoitamka. Maelezo tofauti hutumika kurejelea proposisheni moja ambayo huelezwa kwa kauli tofautitofauti.

Kwa mfano: 2.71:

1) '*Maria hawezi kumsaidia Piera kupata kazi.*'

2) '*Maria anasema kuwa hawezi kumsaidia Piera kupata kazi.*'

3) '*Maria anaamini kuwa hawezi kumsaidia Piera kupata kazi.*'

4) '*Maria anajuta kuwa hawezi kumsaidia Piera kupata kazi.*'

Kauli katika 2.71, ni za kweli kwani zaeleza hisia za Maria kumhusu Piera. Maria haoni uwezekano wowote kamwe wa kumsaidia Piera kupata kazi. Kauli hizi zina proposisheni ya Maria kutomsaidia Piera kupata kazi kamwe, ambapo jambo hili limeelezwa kwa njia anuwai.

## 2.6 PROPOSISHENI KATIKA SENTENSI: MAAGIZO, MASWALI, KUAMURU, UYAKINIFU NA UKANUSHI

Kulingana na Longman (1968:1060), wanasema kuwa sentensi ni fungu la maneno ambalo, **hueleza, huuliza, huamuru** au **kuonyesha mshangao** kuhusu kitu au jambo fulani. Sentensi ya kawaida huwa na kiima na kiarifu. Huanza kwa herufi kubwa. Pia sentensi huwa na ujumbe ulio muhimu na ulio kusudiwa na msemaji ili msikilizaji aweze kuufasiri, kisha aamue kama ataafikiana na msemaji au atayakana madai yaliyo semwa. Hivyo basi, ni muhimu kwa wanao shiriki katika mazungumzo kuelewana vyema.

Cambridge (2008:1300-1301), wanasema kuwa sentensi ni kundi au fungu la maneno ambalo hasa **huwa na vitenzi vinavyoeleza wazo kwa njia ya kauli, maswali, maagizo au mshangao.**

**Madai** yao hayatofautiani sana na yale ya Longmans (1968) kwani, kueleza wazo ni sawa na kufahamisha kuhusu jambo. Vivyohivyo, maagizo yanaafikiana na maelezo kuhusu jambo fulani. Hata hivyo, wana tofautiana kwani hawajatufahamisha kuhusu **amri**, kama Longmans (1968). Kwingineko, Cambridge (2008) wanasema kuwa mawazo huwa ni kwa njia ya **kauli** ambayo ni kuhusu yaliyotamkwa na msemaji kwa kumlenga msikilizaji.

Bussmann (1996:427) anasema kuwa sentensi ni kitengo cha usemi ambacho huundwa kulingana na sheria ambazo lugha hutegemea ili kuunda sentensi. Sheria hizi ni huru zikihusiana na yaliyomo katika lugha, muundo wa lugha na lafudhi. Anaendelea kusema kuwa mwana umuundo BloomField (1933) anatoa maelezo ya sentensi kama: "Umbo kubwa zaidi la kisintaksia lililo huru na ambalo haliwezi kuambatishwa katika mfumo mwingine wa kisintaksia kwa sheria yoyote ya lugha." Sentensi huanzia kwa kitengo kidogo zaidi ambacho ni **fonimu** kisha **mofimu**, **maneno** na hatimaye **kirai**, mwishowe **huwa ni sentensi**. Bussmann (1996) anaendelea kusema kuwa sentensi yaweza kuainishwa kulingana na sura zifuatazo:

**1)Nafasi ya kitenzi ambayo ni muhimu na huonyesha viulizi au amri.**

**2)Kurejelea uamilifu wa pragmatiki katika mawasiliano, mpangilio wa maneno, dhamira na lafudhi kwa kuonysha sentensi nne za kimsingi ambazo ni:** ***Sentensi za kauli*****,** ***sentensi ulizi***, ***sentensi za kuamuru*** na ***sentensi za masharti***.

## 2.6.1 MAAGIZO

Lyons (195:32-33) anasema kuwa lugha zote huwa na sentensi ambazo zina umbo na maana ya sentensi na hutegemea maana ya maneno yaliyoiunda sentensi hiyo. Vilevile, maana ya sentensi hueleweka kupitia kwa muundo wa sarufi yake. Sentensi mbili zaweza kuundwa kwa maneno

yaliyo sawa na kila neno kufasirika sawasawa na neno lingine lolote katika sentensi ya pili na kisha kuwa na maana tofauti.

Kwa mfano: 2.72: 1) '*Kulikuwa kunanyesha jana.*'

2) '*Jana kulikuwa kunanyesha?*'

Sentensi hizi zina maneno sawa na zimo katika umbo moja lakini zatofautiana kisarufi kwa sababu sentensi moja ni **yenye azimio** na nyingine ni **sentensi ulizi**. Sentensi zingine zenye muundo unaoafikiana na wa 2.72 lakini, zina maelezo tofauti.

Kwa mfano: 2.73: 1) '*John anampenda Mary.*'

2) '*Mary anampenda John.*'

Sentensi ya kwanza, John ndiye anayempenda Mary na katika sentensi ya pili, Mary ndiye anayempenda John.

Kilingana na sentensi za 2.72 na 2.73, basi tunapata proposisheni kuwa:

1) **Tumearifiwa kwamba mvua ilinyesha jana.**

2) **Hatuna uhakika kama mvua ilinyesha jana.**

3) **Tumearifiwa kuwa John ndiye mwenye kumpenda Mary.**

4) **Tumearifiwa pia kuwa Mary ndiye mwenye kumpenda John.**

Lyons (1995) anaendelea kusema kuwa sentensi yenye azimio ni sentensi ambayo muundo wake wa kisarufi umo katika sentensi ambazo hutumika kuundia kauli.

Kwa mfano : 2.74:

1) '*Mazoezi ni bora kwa afya.*'

2) '*Ningependa kunywa maji baridi.*'

Sentensi au kauli hizi zina proposisheni zake ambazo zatoa maagizo kuhusu mambo fulani ambayo msikilizaji anahimizwa na msemaji kuyafanya. Hivyo basi, katika kauli ya kwanza, anahimizwa kuwa ni bora kama atafanya mazoezi ili awe na afya bora. Katika kauli ya pili, anaagizwa kuwa msemaji anapendelea kunywa maji yaliyo baridi na wala sio maji moto.

Sentensi ulizi ni ile ambayo muundo wake wa kisarufi umo katika sentensi ambazo hutumika kuuliza maswali, kama; '**Je, mankuli yatakuwa saa ngapi**?' Kulingana na kauli hii tunapata proposisheni kuwa;

**1)Msemaji anataka kufahamishwa jambo.**

**2)Msemaji hajui maankuli yatakuwa ni saa ngapi.**

**3)Msemaji anataka afahamishwa maankuli yatakuwa ni saa ngapi.**

**4)Huenda ikawa msemaji amehisi njaa.**

Saeed (2003:12) anasema kuwa kauli huundwa kwa kuzungumza au kuandika katika lugha fulani.

Kwa mfano: 2.75: **Mtu wa kwanza**: "*Shakespeare ni mwandishi maarufu.*"

**Mtu wa pili**: "*Shakespeare ni mwandishi maarufu.*"

Mifano katika 2.75, ni kauli mbili japo zinafanana kwa sababu zimezungumzwa na watu wawili tofauti ingawa zimo katika lugha moja na proposisheni zake ni sawa. Hivyo basi, kila jambo linalozungumzwa na watu tofauti, hata kama ni kurudia yaliyosemwa na mwingine huwa ni kauli iliyohuru.

Sentensi ni kitengo cha sarufi ambacho huundwa kwa kauli na kwa jumla hutokana na matumizi katika lugha. Mtu wa tatu na wa nne, wakizitamka kauli zilizopo hapa juu tena tutasema kuwa

tuna kauli nne za sentensi moja. Maagizo ni aina za kauli ambazo msemaji hutumia kama anataka jambo fulani litimizwe na msikilizaji.

Kwa mfano: 2.76: "*Utakwenda kununua sukari, mkate na mayai.*"

Kauli 2.76, ina proposisheni kuwa:

**'Kuna mtu anayehitaji vitu kutoka dukani.'**

**'Kuna mtu atakayetumwa dukani kununua vitu vitakavyohitajika.'**

**'Mtu ambaye ametumwa dukani, amepewa maagizo kuhusu vitu vinavyohitajika.'**

Maagizo yanaweza kuwa katika usemi halisi.

Kwa mfano: 2.77: "*Utakwenda kununua sukari, mkate na mayai sita.*" Mama alimwambia Alex.

Proposisheni katika kauli 2.77, itakuwa sawa na kauli ya hapo awali, tofauti ni kuwa kauli ya kwanza ni katika **usemi wa taarifa** na kauli ya pili ni katika **usemi halisi**. Vilevile, maagizo yanaweza kuwepo katika mazungumzo ya kawaida.

Kwa mfano: 2.78: "*Tafadhali, ukirejea kutoka sokoni mtazame mama Anne kama yumo kwake, kisha umwambie kuwa namhitaji afike kwangu leo alasiri.*"

Proposisheni katika kauli 2.78 ni kuwa:

1) **Kuna mtu anayekwenda sokoni.**
2) **Anayekwenda sokoni ameombwa kupitia kwa mama Anne.**
3) **Anayetoa maagizo anamhitaji mama Anne afike kwake.**
4) **Anayetoa maagizo ni mnyenyekevu kwani ametumia neno la upole, '*tafadhali*'.**

### 2.6.2 MASWALI

Maswali ni aina za kauli ambazo msemaji hutumia kama anataka kufahamishwa jambo fulani na msikilizaji. Msemaji anaweza kuwa halifahamu jambo hilo kamwe au anataka kupewa uhakika kuhusu jambo alilo na tashwishi nalo.

Kwa mfano: 2.78:

1) "*Je, kitabu chake ki wapi*?"

2) "*Je, msichana yule ninayemwona kwa mbali ni bintiye Maria*?"

3) "*Umewahi kufika mji wa Nairobi*?"

Kauli ya kwanza, ina proposisheni: 1) **Msemaji hajakiona kitabu cha mtu yule.**

2) **Msemaji hana uhakika kilipo kitabu chake.**

3) **Mtu anayerejelewa ana kitabu.**

Kauli ya pili, anayeuliza ana tashwishi kuhusu jambo hilo, hivyo anataka kuhakikishiwa. Ina Proposisheni ni kuwa:

1) **Msemaji amemwona msichana kwa mbali.**
2) **Msemaji anataka hakikisho kama msichana aliyemwona ni binti wa Maria au la.**
3) **Maria ana binti.**
4) **Anayeuliza anafahamu kuwa Maria ana Binti.**

Kauli ya tatu, anayeuliza hafahamu jawabu.

Proposisheni ni kuwa:

1) **Msemaji ana jambo analotaka kulisema kuhusu mji wa Nairobi.**
2) **Msemaji hana uhakika kama msikilizaji amewahi kuwa mjini Nairobi au la.**

### 2.6.3 KUAMURU

Kauli za kuamuru ni ambazo msemaji hutumia katika kutoa amri kwa msikilizaji.

Kwa mfano: 2.79: '*Njoo hapa.*'

'*Simama.*'

'*Kimbia.*'

Mara nyingi, kauli za kuamuru huwa na maneno machache sana. Hata hivyo, kuna wakati ambapo huwa na maneno kadha.

Kwa mfano: 2.80: 1) "*Niletee kitabu chako mara moja.*"

2) "*Sitaki kumwona mtu yeyote hapa.*"

3) "*Lazima uzungumze sasa hivi.*"

Proposisheni katika mifano 2.79, ni kuwa; msemaji ametoa amri ambazo ni lazima zitimizwe mara moja na aliyeamrishwa kufanya hivyo. Mifano katika 2.80, ina proposisheni kuwa:

1) **Anayezungumziwa ana kitabu anachomiliki.**

**Ameamrishwa kukipeleka kitabu kile.**

2)**Msemaji hapendi kuwaona watu pale.**

**Ameamrisha kuwa yeyote asifike pale.**

3)**Anayezungumziwa lazima aseme.**

**Hawezi kusema baadaye ila ni sasa hivi.**

### 2.6.4 UYAKINIFU

Uyakinifu ni hali ya kukubaliana na jambo katika kauli au sentensi. Ni sentensi katika hali yake ya kawaida kama ilivyo semwa.

Kwa mfano: 2.81: 1) "*Ninataka kwenda nyumbani.*"

2) "*Watafika asubuhi.*"

*Utakila chakula hiki."*

Kauli za 2.81 zina proposisheni kuwa:

**1)Mimi nataka kufanya jambo.**

**Jambo ninalotaka kulifanya ni kwenda nyumbani.**

**2)Kuna watu wanaosafiri.**

**Huenda wametuarifu kuwa watafika asubuhi.**

**3)Kuna chakula kilichopikwa.**

**Chakula hicho kitaliwa na anayeambiwa.**

**2.6.5 UKANUSHI**

Ukanushi ni kinyume cha uyakinifu. Ni hali ya kukataa jambo katika kauli au sentensi. Ni sentesi au kauli katika hali ya kutokubaliana na yaliyosemwa.

Kwa mfano: 2.82:

1) "*Sitaki kwenda nyumbani.*"

2) "*Hawatafika asubuhi.*"

3) "*Hutakila chakula hiki.*"

Kulingana na kauli hizi, proposisheni ni kuwa:

1) **'Mimi sitaki kwenda.'**

**'Huenda nahitajika nyumbani.'**

2) **'Huenda wanaosafiri walichelewa kung'oa nanga.'**

**'Labda wametuarifu kuwa hawatafika asubuhi.'**

3) **'Kuna chakula kilichopikwa.'**

**'Anayezungumziwa hapaswi kula chakula hicho.'**

## 2.7 HITIMISHO

Sura hii imeshughulikia dhana tofautitofauti ambazo huhusiana na proposisheni. Dhana ya proposisheni imeelezwa kwa kina pamoja na aina zake kisha kuhusisha mifano mwafaka. Vilevile, imeeleza kuwa proposisheni huwa na misingi ya kweli na ya uongo ili kuweza kuthibitika na kukubaliwa. Kwingineko, proposisheni mbalimbali hujitokeza kupitia kwa sentensi ambazo hujumlisha maagizo, maswali, kuamuru, uyakinifu na ukanushi.

Vilevile imeshughulikia aina za proposisheni ambazo ni; proposisheni ya hakika, proposisheni ya thamani na proposisheni ya sera. Ubainishaji wa aina hizi za proposisheni hutegemea hasa maoni ya msikilizaji kuhusu ufaafu wa mambo yaliyoko katika proposisheni tofauti. Hivyo basi, huwa na jukumu la kutathmini mambo yaliyotamkwa na msemaji. Pia sura hii imejihusisha na ishara za proposisheni nzuri ambazo zadai kuwa; proposisheni nzuri yapaswa; kujadilika na kuthibitika. Wasemaji na wasikilizaji ndio hasa hujihusisha katika maswala kuhusu kujadilika na kuthibitika kwa proposisheni.

Vivyohivyo, sura hii pia imejadili proposisheni katika misingi ya ukweli au uongo wake kwani kauli iliyo tamkwa na msemaji yapaswa kuwa kweli ili ikubalike, kisha ieleze proposisheni yenye thamani ya ukweli. Ikiwa proposisheni ni ya uongo basi, huwa haina budi kukataliwa. Proposisheni katika sentensi za aina tofauti ni jambo ambalo pia limeshugulikiwa katika sura hii. Sentensi zenyewe ni kama vile; maagizo, maswali, kuamuru, uyakinifu na ukanushi. Tumeeleza kuwa sentensi ni fungu la maneno ya aina tofauti ambayo huambatanishwa pamoja ili kuunda kauli yenye maana na mantiki. Hivyo basi, kulingana na aina za sentensi tulizoziorodhesha ni kuwa kauli huwa na miundo ya aina mbalimbali kulingana na kusudi la msemaji kwa msikilizaji.

# SURA YA TATU

# PROPOSISHENI NA ISTILAHI NYINGINE

## 3.0 UTANGULIZI

Sura ya tatu itajadili proposisheni katika vitendo usemi ambavyo ndani yake huwa na lokusheni, ilokusheni na palokusheni. Pia itahusisha proposisheni katika chukulizi na umaanisho. Vilivile, itashughulikia proposisheni katika miktadha tofauti ambayo itazua maana tofauti kulingana na jinsi proposisheni itakavyoeleweka na kufasiriwa na msikilizaji kutoka kwa msemaji. Kisha itashughulika na proposisheni katika miktadha tofauti, kwa kuonyesha maana ambazo huwepo hasa katika mazungumzo ya watu na jinsi ambavyo washiriki katika mazungumzo hupaswa kuwa na maafikiano fulani ili waelewane.

## 3.1 PROPOSISHENI KATIKA VITENDO USEMI: LOKUSHENI, ILOKUSHENI, PALOKUSHENI

Baadhi ya wanaisimu wameeleza kuhusu dhana ya vitendo usemi kama vile Wales (1991:426-427) ambaye anasema kuwa nadharia ya vitendo usemi yahusishwa na kazi ya mwana falsafa Austin (1962) ambaye aliiendeleza zaidi. Nadharia hii yahusu vitendo vya kiisimu ambavyo huundwa wakati wa kuzungumza na huwa na kusudi la kijamii na mwingiliano baina ya watu tofauti katika jamii pamoja na athari zake za kipragmatiki. Austin (1962), alibuni:

1) **Kitendo cha kauli** ambacho alikiita kitendo cha lokusheni: Kama vile: *Aliniambia; "muue"*.
2) **Kitendo cha utendaji** katika kusema jambo: Kama; *kuahidi, kuapa, kuonya* ambacho alikiita kitendo cha ilokusheni. Kama vile: *Aliniomba nimuue.*

3) **Kitendo cha utendaji baada ya kusema jambo.** Kama; *kusihi* ambacho alikiita palokusheni. Kama vile: *Alinisihi nimuue.*

Vitendo hivi vya Austin (1962) hukamilika na kukubalika kama vitatimiza masharti fulani, ambayo yafaa katika kuibua maana mwafaka. Kama vile; kutambua kusudi la msemaji kuwa ana mamlaka yafaayo kufanya jambo kama; *kubatiza na kuteua* katika wadhifa fulani. Tendo la ilokusheni ndilo muhimu zaidi hasa kwa sababu za kusudi tofauti katika mawasiliano kupitia kwa kauli. Kama vile: "*naahidi kuwa nitakuwa mwema*". Vitendo usemi vinaweza kuwa katika usemi halisi au usemi usio halisi.

Kwa mfano:

3.1: "*Naahidi kuwa nitafika.*"

*3.2: "Musa aliahidi kuwa atafika.*"

Kauli ya kwanza imo katika usemi halisi na kauli ya pili imo katika usemi wa taarifa au usio halisi. Proposisheni katika kauli hizi ni kuwa:

1. **Mimi ndiye mwenye kutoa ahadi. Ninamwahidi mtu fulani kuwa nitafika.**
2. **Musa ndiye mwenye kutoa ahadi. Mimi ninaeleza jambo lililosemwa na Musa kuwa aliahidi kufika.**

Hivyo basi vitendo usemi ni kauli ambazo hutokana na mazungumzo baina ya watu tofauti kwa kusudi la msikilizaji kuufasiri ujumbe wa msemaji kama alivyonuia kisha, kuwasiliana na kuafikiana katika mazungumzo baina yao. Kila tendo katika vitendo usemi hubainishwa kwa jinsi lilivyotamkwa hasa kwa kuzingatia kiimbo kilichotumika. Kama vile; *tendo la*

*amri, tendo la kauli ya kawaida au tendo baada ya msikilizaji kupata athari fulani kutoka kwa kauli ya msemaji.*

Vilevile, kuna makundi matano ya vitendo vya ilokusheni ambayo yamehusishwa na sarufi kama yanavyoelezwa na vitendo usemi tofauti. Makundi hayo ni:

**1)Kauli wakilishi au tetezi.** Msemaji huahidi kuwa jambo ni la kweli katika proposisheni iliyoelezwa. Hivyo basi, *hudumisha, hubainisha, huripoti* au *hudai jambo fulani.*

Kwa mfano: 3.3: ***Kuripoti***: "*Rais wa Marekani atawasili nchini leo alasiri.*"

3.4: ***Kudai jambo***: "*Sina tashwishi kuwa jambo hilo ni la kweli.*"

**2)Maagizo au maelezo.** Msemaji humsawishi msikilizaji kuchukua mwelekeo fulani. Humbidi msemaji *kuamuru, kusihi* na *kutoa mawaidha.*

Kwa mfano: 3.5: ***Kuamuru***: "*Nenda!*"

3.6: ***Kusihi***: "*Tafadhali, usilifanye jambo hilo.*"

**3)Kauli za kujitolea.** Msemaji huchukua jukumu la kufanya kitendo katika wakati ujao, kama vile, *kuahidi* na *kutisha.*

Kwa mfano: 3.7: ***Kuahidi***: "*Nina hakika kuwa nitawasili.*"

3.8: ***Kutisha***: "*Leo utanitambua!*"

**4)Kauli elezi.** Msemaji hueleza mtazamo wa jambo kulingana na masharti fulani ya uaminifu katika hali inayoelezwa na proposisheni, kama vile, *kupongeza, kushukuru, kuomba udhuru* na *kutoa rambirambi.*

Kwa mfano:

3.9: ***Kupongeza***: "*Hongera kwa kazi yako nzuri.*"

3.10: ***Kuomba udhuru:*** "*Niwie radhi kwani sitaweza kuhudhuria mkutano wa kesho.*"

5)**Kauli za kuarifu.** Msemaji huangazia jambo halisi na kulihusisha na yaliyomo katika proposisheni kama vile, *kueleza*, *kutangaza azimio fulani* na *kusema kuwa mtu fulani ana hatia.* Kwa mfano:

3.11: ***Kutangaza azimio:*** *"Kusudi letu ni kuhakikisha kuwa haki za kila mwana nchi zimezingatiwa ipasavyo."*

3.12: ***Kueleza:*** *"Kitabu hiki kina mawaidha bora kwa wanaspoti wote."*

Kwa hivyo, tendo la ilokusheni tunapata kuwa ndilo muhimu zaidi kati ya matendo yote matatu kwani hasa ndilo humlenga msikilizaji. Hii ni kwa sababu huonyesha mambo ambayo binadamu huyatenda mara kwa mara katika mwingiliano baina yake na binadamu wenzake kwa njia ya mawasiliano. Maana iliyokusudiwa na msemaji kwa msikilizaji hufahamika na tendo linalotarajiwa kufanyika aidha kwa kukubali au kwa kukataa kauli ya msemaji, kulingana na jinsi msikilizaji atakavyo tathmini kauli kutoka kwa msemaji.

Vitendo usemi ni maarufu katika isimu na hutumika kurejelea nadharia ambayo huchanganua jukumu za kauli kwa kuzihusisha na tabia za msikilizaji na msemaji katika mawasiliano baina yao. Vitendo usemi kwanza, ni utendaji wa mawasiliano au tendo la lokusheni, pili, ni jambo ambalo hubainishwa kwa kurejelea kusudi la msemaji wakati anapozungumza au msukumo wa kiilokusheni katika kauli yake na tatu, ni athari ambazo hutimizwa kwa msikilizaji kupitia kwa yaliyosemwa au athari na palokusheni katika kauli ya msemaji. Vitenzi ambavyo hutumika ili kuthibitisha vitendo usemi vilivyokusudiwa na msemaji pia huitwa vitenzi tendaji. Vigezo ambayo hutoshelezwa ili vitendo usemi viwe na mafanikio hujulikana kama masharti ya usemi.

Maoni haya nakubaliana nayo kwani, hata hivyo humlenga pia msemaji kwa sababu anapaswa kuwa na matarajio fulani akilini mwake kutoka kwa msikilizaji ambaye anamtegemea kuliyafanya jambo baada ya mazungumzo baina yao. Msemaji huwa na mtazamo kuwa maoni yake yataafikiana na yale ya msikilizaji na hatarajii kunyume chake. Kwingineko, vitendo usemi vinapaswa kuibua proposisheni kadha kutegemea uelewa wa msikilizaji kuhusu yaliyotamkwa na msemaji.

Kurejelea utendaji uliopo hapo juu, kuna utendaji uliowazi na kuna utendaji unaoeleweka. Tofauti kati yake ni kuwa, kwanza, utendaji uliowazi unahusu maelezo yasiyo na utata na ambayo ni dhahiri kama vile; *naapa, naahidi.* Pili, utendaji unaoeleweka huhusisha kauli ambazo hutimiza utendaji uliokusudiwa.

Kwa mfano katika kauli zifuatazo: 3.13: "*Nakuamrisha uende.*" 3.14: "*Nenda.*"

Kauli ya kwanza yaeleza tendo la kuamrisha ilhali, kauli ya pili yaweza kueleza tendo la kuamrisha au kumpa mtu wosia. Tendo hili la vitendo usemi lahusisha matendo matatu yanayohusiana. Kwanza kuna ***tendo la lokusheni*** ambalo ni tendo la kimsingi katika kutamka au kauli ya kiisimu yenye maana.

Kwa mfano: 3.15: "*Nimepika chai ya kahawa sasa hivi.*"

Kauli huundwa ili iwe na jukumu fulani katika akili. Pili, kuna ***tendo la ilokusheni*** ambalo huundwa kwa msukumo wa kimawasiliano katika kauli, kama vile kauli 3.15, yaweza kutamkwa ili kueleza jambo, kujitolea kumpa mtu kitu au kwa kusudi lingine lolote la kuwasiliana. Vile vile, tendo hili hujulikana kama msukumo wa kiilokusheni ambalo ni kulingana na jinsi ya

utamkaji katika kauli yake. Tatu, kuna ***tendo la palokusheni*** ambalo msikilizaji atapata athari anazokusudiwa kuzipata kupitia kwa kauli ya msemaji. Kwa mfano: 3.16: ***kumfanya msikilizaji kunywa kahawa.*** Pia, tendo hili lajulikana kama athari za palokusheni. Kimsingi, vitendo usemi humaanisha kuwa ni msukumo wa kiilokusheni katika kauli.

## 3.2 PROPOSISHENI KATIKA CHUKULIZI NA UMAANISHO

Maana ya proposisheni hudhihirika katika chukulizi na umaanisho. Kila mojawapo ya istilahi hizi hueleza jinsi proposisheni hujitokeza katika nyanja tofauti kwa kuzihusisha katika kauli tofauti ambazo hufasirika kulingana na uelewa wa mpokezi ujumbe.

### 3.2.1 PROPOSISHENI KATIKA CHUKULIZI

Brown na Yule (1983:28-29) wanasema kuwa chukulizi ni jambo ambalo humpatanisha msemaji na msikilizaji katika mazungumzo. Msemaji ndiye chanzo cha chukulizi katika mawasiliano. Hii ina maana kuwa kama msemaji ana unafahamu wa hapo awali kuhusu hali ya msikilizaji na uhusiano walio nao, basi hahitaji kulisema jambo kwa ukamilifu kwani anayo hiari ya kuyaacha mambo mengine kwa sababu msikilizaji atunda chukulizi akiini mwake kuhusu mambo ambayo hayakutajwa. Msemaji huzua chukulizi kwa msikilizaji kwa kuwa yeye ndiye hutamka kauli ambazo msikiliza huzitafakari na kupata chukulizi mwafaka akilini mwake. Kwingineko, kuna akiba ya chukulizi ambayo huwa na ujumbe wa kijumla kulingana na muktadha wa diskosi. Washiriki katika diskosi huwa na akiba yao ya chukulizi na huwa na mchango wao kutegemea jinsi diskosi inavyoendelea. Mazungumzo yanapoendelea akiba ya chukulizi huwa na kiima kinachorejelewa katika mazungumzo.

uhusiano walio nao, basi hahitaji kulisema jambo kwa ukamilifu kwani anayo hiari ya kuyaacha mambo mengine kwa sababu msikilizaji atunda chukulizi akiini mwake kuhusu mambo ambayo hayakutajwa. Msemaji huzua chukulizi kwa msikilizaji kwa kuwa yeye ndiye hutamka kauli ambazo msikiliza huzitafakari na kupata chukulizi mwafaka akilini mwake. Kwingineko, kuna akiba ya chukulizi ambayo huwa na ujumbe wa kijumla kulingana na muktadha wa diskosi. Washiriki katika diskosi huwa na akiba yao ya chukulizi na huwa na mchango wao kutegemea jinsi diskosi inavyoendelea. Mazungumzo yanapoendelea akiba ya chukulizi huwa na kiima kinachorejelewa katika mazungumzo.

kwa mfano: 3.17:

1) *"Alikwambia nini?"*

2) *"Alisema kuwa tunafaa kumwona kesho."*

Chukulizi katika kauli hizi ni kuwa kuna kiima anayerejelewa kama "A" katika mazungumzo baina ya msemaji na msikilizaji. Vilevile, msemaji anachukulia kuwa msikilizaji anafahamu anayerejelewa bila kumtaja, naye msemaji anapojibu anachukulia vivyo hivyo.

Baadhi ya wanafalsafa wamejihusisha na hadhi ya sentensi kwa mfano: 3.18: '*Mfalme wa Ufaransa ana upara.*' Sentensi 3.18, ina proposisheni kuwa:

1) **Kuna mfalme wa Ufaransa.**

2) **Mfalme huyu wa Ufarasa ana upara.**

Kulingana na maelezo yanayorejelea kauli kama 3.18, msemaji anachukulia kuwa msikilizaji anaweza kumtambua mtu au kitu kinachozungumziwa. Hivyo basi, hadai kuwa mtu au kitu kipo, anachukulia kuwa kipo kwani kuna upara na mtu yupo kwa sababu kuna mfalme ambaye ni wa

Ufaransa. Kama mtu au kitu hakipo, basi lazima chukulizi ifaulu na sentensi itakuwa si ya kweli na wala si ya uongo, bali kuna pengo katika thamani yake.

Matumizi bora ya sentensi katika nyanja fulani yatategemea uchukulizi wa baadhi ya proposisheni. Kwa mfano: 3.19: Mtu akisema. "*Barua haijafika bado*". Kauli yake itakuwa mwafaka kama kuna chukulizi kuwa barua itawasili baada ya muda fulani maalum. Chukulizi yaweza kuwa barua itawasili kabla ya adhuhuri ya siku ambayo kauli hiyo ilitamkwa. Sentensi fulani itakuwa ya kweli ili sentensi nyingine iwe ya kweli au uongo, Kwa mfano: 3.20: *'Virginia anajua kuwa gazeti lake limechelewa.'* Kauli 3.20, ina chukulizi kuwa *'gazeti la Virginia limechelewa'* kwa sababu Virginia anachukulia hivyo na anao uhakika kuwa limechelewa. Kauli kuwa *'gazeti la Virginia limechelewa'* kama ni kauli ya kweli basi, *'Virginia anajua kuwa gazeti lake limechelewa'*, itakuwa ni ya kweli wala si ya uongo. Hivyo basi, katika maeneo ambapo sentensi yapaswa kueleza proposisheni katika muktadha, proposisheni hizo hufahamika kuwa za kweli au uongo, nadharia ya semantiki katika proposisheni yaweza kueleza kuwa sentensi "S" yachukulia proposisheni "P" katika muktadha fulani kama tu proposisheni "P" ni ya uongo basi sentensi "S" itaeleza kuwa hakuna proposisheni katika muktadha huo. Wazo la chukulizi ya msemaji laweza kuhusishwa na proposisheni ambazo msemaji huchukulia kuwa za kimsingi na jambo hili linalomhusu msemaji na chukulizi anazokusudia zifasiriwe na msikilizaji hujulikana kama nadharia ya pragmatiki katika proposisheni. Matumizi makuu ya nadharia hii yahusu kuanisha mambo yaliyopo katika muktadha wa kiproposisheni, ambayo yanaweza kutumika kueleza masharti fulani katika ufaafu wa kutumia sentensi maalum.

Wakati mtu anaposema kitu, huwa tunapata chukulizi za aina kadha kuhusu sababu za kauli zilizotamkwa ambazo twatumaini kuwa zilifahamika kabla ya kauli kutamkwa. Kwa mfano: 3.21: "*Mwambie Maria kuwa nimekwenda kwa maankuli.*" Msemaji alitarajia kuwa Maria anaweza kuwasili wakati wowote. Pia anachukulia kuwa msikilizaji anamfahamu Maria ni nani, na kuwa ananuia kumpa Maria ujumbe huo. Chukulizi kama hii ni ya Kipragmatiki kwani yategemea matumizi yake katika mawasiliano na washiriki katika mazungumzo. Chukulizi ya kipragmatiki yahusishwa na muktadha katika kauli 3.21. Hata hivyo, kuna chukulizi ambayo haihusishwi na muktadha katika kauli 3.21, kuwa kuna mtu kama Maria.

Proposisheni katika kauli hii ni kuwa:

1) **Msemaji anamfahamu Maria.**
2) **Mpokezi ujumbe anamfahamu Maria.**
3) **Msemaji anamtarajia Maria kufika.**
4) **Msikilizaji anapaswa kumpa Maria ujumbe kutoka kwa msemaji.**
5) **Huenda ikawa msemaji hataki kukutana na Maria hivyo basi akaamua kwenda kwa maankuli.**

Chukulizi ni mambo ambayo huchukuliwa kuwepo katika kauli na husalia kuwa na msukumo hata kama kauli itakanushwa.

Kwa mfano:

3.22: '*Yohana aliweza kuuza hisa zake kabla ya soko la hisa kufilisika.*'

3.23: '*Yohana hakuweza kuuza hisa zake kabla ya soko la hisa kufilisika.*'

Kulingana na kauli hizi, Yohana alijaribu iwezekenavyo kuziuza hisa zake. Chukulizi kuwa Yohana alijaribu kufanya jambo halibadilishwi na kinyume cha kauli ya pili 3.22 na 3.23.

Proposisheni katika kauli 3.22 na 3.23 ni kuwa:

1) **Kuna mtu anayejulikana kwa jina Yohana.**
2) **Yohana alikuwa amemiliki hisa.**
3) **Yohana alikuwa na mpango wa kuziuia hisa zake.**
4) **Soko la hisa lilifilisika.**

Vilevile, katika mfano mwingine unaofikiana na huu, kwa mfano: 3.24:

1) *'Yusufu anajuta kuwa alisafiri jana'*.
2) *'Yusufu hajuti kuwa alisafiri jana'*.

Proposisheni katika kauli 3.24, ni kuwa:

1) **Kuna mtu anayejulikana kwa jina Yusufu.**
2) **Yusufu alisafiri jana.**
3) **Yusufu alikuwa na mpango wa kusafiri.**

Hivyo basi, msikilizaji atachukulia kuwa huenda ikawa kuna jambo ambalo lilitokea na kumfanya Yusufu kujuta kusafiri kwake ilhali kama kauli itakanushwa na kuwa kinyume, basi hatakuwa na jambo lolote la kumfanya kujuta. Kwingineko, katika mfano wa hapo awali, Yohana aliweza kubahatika na kuziuza hisa zake lakini, kama kauli hii itakanushwa basi itabidi ajute kwa sababu hakufanikiwa kuziuza hisa zake kabla ya soko la hisa kufungwa.

Chukulizi hurejelea proposisheni ambazo ukweli wake huchukuliwa kuwa wa kawaida katika kueleza kauli za kiisimu na ambazo huwezesha kauli kutathminiwa. Kwa mfano: 3.25: "*Juma kutofaulu katika uchaguzi alioshiriki ni jambo la kuhofisha sana.*" Kauli hii ina proposisheni kuwa: '**Juma hakupata ushindi katika uchaguzi alioushiriki.**' Chukulizi iliyopo pia huelezwa kwa njia iliyo wazi.

Kwa mfano:

3.26: "*Sinema katika idhaa ya "KTN" ni nzuri*".

*3.27: "Nimewafunza watoto wa Farida."*

Kauli 3.26, ina chukulizi kuwa; '**kuna sinema katika idhaa ya "KTN",**' ilhali kauli 3.27, ina chukulizi kuwa; '**Farida ana watoto.**' Chukulizi iliyo na hakika yaweza kuhusishwa na maelezo ambayo huwa na kiima au yambwa. Yambwa ambayo husifu mambo yaliyopo kama; ***fahamu*** na ***tambua***, kiima ambacho husifu kama; ***kumaanisha*** na ***thabiti***. Mambo haya hurejelewa kuwa na chukulizi za kweli kama sifa za mambo yaliyopo kama vile; ***kujuta***, ***kushangaa*** na ***kufurahi*** kwa mfano: 3.28: "*Amina ana gari la kifahari.*"

Kauli 3.28, ina chukulizi kuwa :

1) **Luka anajua kuwa Amina ana gari la kifahari.**
2) **Amina kuwa na gari la kifahari ni jambo la kawaida.**
3) **Luka anajuta kuwa Amina ana gari la kifahari.**
4) **Amina kuwa na gari la kifahari ni jambo ambalo liliwashangaza wazazi wake.**
5) **Huenda ikawa Luka hana furaha kuwa Amina ana gari la kifahari.**

Proposisheni katika kauli 3.28, ni kuwa:

1) **Kuna mtu anayejulikana kwa jina Amina.**

2) **Amina amelimiliki gari fulani.**

3) **Gari la Amina sio la kawaida.**

4) **Huenda ikawa Amina ni tajiri kwa sababu ana uwezo wa kumiliki gari la kifahari.**

Chukulizi huwa na mambo kadha yaliyo muhimu, kwanza chukulizi ni kipengee cha semantiki, jambo ambalo huchukuliwa kuwa ni la kawaida. Vilevile, huwa na mtazamo wa kipragmatiki. Kauli zifuatazo zinaafiki jambo hili.

Kwa mfano: 3.29:

1. a) *Wanafunzi wanajuta kuwa mwalimu Julius alichelewa kufika darasani.*

b) *Mwalimu Julius alipochelewa kufika darasani, wanafunzi walidai kuwa ni lazima aombe msamaha.*

c) *Kama mwalimu Julius hangechelewa wangefanya kazi zao.*

2. *La, hakuchelewa.*

3. .*La, hawajuti kuchelewa kwake, hawakudai msamaha, hawangefanya kazi zao.*

Mtu anapotamka kauli mojawapo kati ya zilizopo katika mfano wa kwanza, huenda atafahamika kuwa anachukulia ni jambo la kawaida kuwa; '*mwalimu Julius alichelewa kufika darasani*' badala ya kufahamika kuwa anadai jambo hilo. Hivyo basi, kukana chukulizi kwa kauli ya pili 3.29, hakutafaa. Hata hivyo, dai hilo laweza kukanwa kwa kauli ya tatu 3.29. Pili, chukulizi

ambazo huhusishwa na neno huwa thabiti wakati ambapo kishazi kilicho na neno hilo hukanushwa au kuulizwa kama swali lenye chukulizi:

'**Mwalimu Julius alichelewa kufika darasani'**, itaunganishwa na vishazi katika mifano 3.29, kauli ya kwanza, ambayo yaweza kukanushwa au kuwa swali kwa mfano: 3.30:

1. *a) Wanafunzi hawajuti kuwa mwalimu Julius alichelewa kufika darasani.*

*b) Je, wanafunzi walifurahia wakati mwalimu Julius alichelewa kufika darasani?*

*c)Kama mwalimu Julius hangechelewa kufika darasani, wanafunzi hawangefanya kazi zao.*

Pia, chukulizi zinaweza kukanushwa kama kuna ushahidi wa kutosha katika kinyume chake. Kwa mfano: 3.31:

1. a) *Watoto wa Jack ni werevu lakini Jack hana watoto.*

*b)Wanafunzi wanajuta kuwa mwalimu Julius alichelewa kufika darasani ingawa mwalimu Julius hakuchelewa.*

*c)Wanafunzi walisherehekea wakati matokeo ya mwisho yalitangazwa, lakini hayakutangazwa kamwe.*

*d)Kama mwalimu Julius angechelewa kufikia darasani, wanafunzi wangesikitika ingawa mwalimu Julius hakuchelewa.*

2. a) *Nina uhakika kuwa watoto wa Jack in werevu, kama ana watoto.*

*b)Wanafunzi watajuta kuwa mwalimu Julius alichelewa kufika darasani kama kwa hakika alichelewa.*

*c)Nilikuwa mle chumbani wakati matokeo ya mwisho yalitangazwa, kama kwa hakika yaliwahi kutangazwa.*

Vilevile, chukulizi huhusishwa na mambo yanayochukuliwa kuwepo katika ulimwengu. Hata hivyo, vitenzi na maneno yanaweza kueleza mambo yaliyo na uhusiano katika kutathmini chukulizi zinazohusu tungo.

Kwa mfano: 3.32:

1. *a) Niliota kuwa dunia ilikuwa tambarare, na kuwa watu wengi walifurahi wakati Columbus alianguka ukingoni.*

*b) Chukulia kwamba Columbus aligundua jinsi ya kupenya hadi India; hakuna mtu ambaye angemkosoa kama angefika eneo hilo.*

*c.)Kama nguruwe wangepaa angani, mabawa ya nyama yake hayangekuwa na ladha sawa na mabawa ya kuku.*

Kauli hizi, zinaeleza ulimwengu kwa *ndoto, chukulizi* na *masharti* hivyo basi, chukulizi zenye uhusiano zinatumika. Chukulizi zifuatazo zahusishwa na ulimwengu halisi na wala sio ndoto au kuchukulia jambo fulani kuwepo.

Kwa mfano: 3.33:

1. *a) Niliota kuwa kila mtu alijuta kuwa Columbus alianguka alipokuwa katika ukingo wa dunia.*

b) *Chukulia kwamba watu walikuwa wamemkosoa Columbus kwa kukosa kutua katika maeneo ya India.*

c) *Kama mabawa ya nguruwe hayana ladha nzuri, usiyale.*

### 3.2.2 PROPOSISHENI KATIKA UMAANISHO

Umaanisho hutumika katika isimu hasa katika muundo wa mazungumzo. Mazungumzo katika umaanisho hurejelea kinachohusishwa na matamshi kwa misingi ya kanuni za ushirikiano ambazo huamua kuhusu ufaafu na ukubalifu uliopo katika mazungumzo. Kwa mfano: 3.34: *"Kuna kipande cha chaki kilicho sakafuni".* Kauli hii yamaanisha kuwa unafaa kukichukua kipande kile cha chaki.

Proposisheni katika kauli 3.34, ni kuwa:

1) **Kuna mtu ambaye amekiona kipande cha chaki sakafuni.**
2) **Mtu aliyekiona kipande cha chaki sakafuni anamweleza mwingine kuhusu kipande cha chaki kilicho sakafuni.**
3) **Anayetoa maelezo haya anatarajia kuwa msikilizaji atakichukua kipande kile cha chaki baada ya kufahamishwa kukihusu.**
4) **Msikilizaji anapaswa kukichukua kipande kile cha chaki.**

Mambo yanayosemwa na yanayomaanishwa huwa tofauti. Kwanza, jambo lililosemwa hurejelea maana ya juu inayomaanishwa na maneno ambayo yanaweza kuelezwa kwa misingi ya masharti ya ukweli. Pili, jambo lililomaanishwa hurejelea athari anazokusudiwa kuwa msikilizaji atazipata

baada ya kutambua jambo hasa alilolilenga msemaji katika kauli yake kwa msikilizaji. Mazungumzo kati ya Yohana na Maria, kwa mfano: 3.35:

*Yohana: "Yuko wapi Anna?"*

*Maria: "Ametembea kuelekea maktabani muda wa kama dakika tano zilizopita".*

Maria anaripoti alichokiona akifanya Anna muda wa takribani dakika tano zilizopita, lakini huenda anamaanisha muda zaidi ya dakika tano. Maria anamaanisha kuwa kama Yohana anataka kumwona Anna, basi ama anaweza kumpata maktabani au maeneo yaliyomo karibu na maktaba. Vilevile, kwa kurejelea *maktaba* Maria anamaanisha kuwa Yohana ana ufahamu wa mahali panapoitwa maktaba. Kwingineko, huenda ikawa umbali wa mahali walipo Maria na Yohana ni karibu na maktaba na mtu hutumia takribani dakika kama tano hivi kufika maktabani.

Umaanisho hutokea wakati ambapo msemaji hutamka sentensi au kauli moja na kurejela jambo fulani. Baada ya kutamka na kuzua maana iliyokusudiwa, basi umaanisho hujitokeza akilini mwa msikilizaji na kulifahamu jambo ambalo msikilizaji alipaswa kulielewa. Unapokuwa na maana iliyokusudiwa katika kauli pamoja na chukulizi ambayo msemaji anataka ifahamike bila kukiuka kanuni yoyote katika mazungumzo, basi utakuwa ni umaanisho katika mazungumzo. Kwa mfano: 3.36: '*Hamisi atakutana na mwanamke leo jioni.*' Umaanisho uliopo katika kauli ni kuwa mwanamke huyu si mkewe Hamisi hii ni kwa sababu mkewe hapaswi kurejelewa kama mwanamke na badala yake ingekuwa, 'Hamisi atakutana na mkewe leo jioni' Proposisheni katika 3.36, ni kuwa:

1) **Kuna mtu anayejulikana kwa jina Hamisi.**

2) **Hamisi ana mpango wa kukutana na mtu fulani jioni.**

3) **Mtu ambaye Hamisi anapanga kukutana naye ni mwanamke.**

4) **Mpango wa Hamisi kukutana na mwanamke huyo ni leo jioni na wala sio kesho au siku nyingine.**

Kwingineko, umaanisho hufahamika kwa kuhusishwa na muktadha wa yaliyasemwa na chukulizi maalumu kuhusu hali ya ushirikiano uliopo baina ya watu wanapotangamana katika mazungumzo. Ufahamu huu hutokea kwa kuulinganisha na uhusiano uliopo baina ya msemaji na msikilizaji na jinsi msemaji anavyochulikwa kuwa ana kanuni za ushirikiano akilini mwake. Msemaji kama atatazama na kuzingatia kanuni hizi moja kwa moja basi, si lazima alitaje jambo kwa njia ya moja kwa moja kwani atachukulia kuwa msikilizaji vilevile anazingatia kanuni hizo. Kwa mfano: 3.37: *Maria : "Petroli kwisha !"*

*Asha : "Kuna gereji pale pembeni."*

Kauli ya Asha huenda inamaanisha kuna uwezekano kuwa Maria anaweza kupata petroli katika gereji hilo, hata kama si kituo cha petroli kwani labda wao hununua na kuhifadhi petroli pale katika gereji lao. Hivyo basi, kama Maria atafika kwenye gereji gari lake litapata petroli.

Proposisheni katika 3.37, ni kuwa:

1) **Maria ana gari.**

2) **Gari la Maria limekwisha petroli kabla ya kukamilisha safari yake.**

3) **Asha anafahamu kuwa kuna gereji karibu na mahali walipo.**

4) **Huenda ikawa Asha pia anafahamu kuwa wanaohudumu katika gereji hilo hununua na kuhifadhi petroli.**

5) **Asha anafahamu anachokimaanisha Maria hata kama hakumfahamisha kila kitu.**

Wales (2001:83-84) anasema kuwa kanuni ya ushirikiano ni ya kimsingi katika mawasiliano ya kawaida. Huhakikisha kuwa kuna uhusiano baina ya washiriki katika mazungumzo. Kanuni hii ya ushirikiano hutawaliwa zaidi na makundi manne makuu ambayo yamejigawa kama visehemu vya kanuni zinazobainishwa kuwa ni zifuatazo:

1)**Kanuni ya ukweli:** Mtu anapaswa kuyasema mambo anayoyafahamu kuwa ni ya kweli na kuwa ana uhakika nayo, kwa mfano: 3.38: '*Alex ana shahada mbili.*" Kauli hii itakuwa na maana kuwa mimi ninaamini kuwa Alex anazo shahada mbili, kisha ninao ushahidi kuwa Alex ana shahada mbili. Hata hivyo, kauli hii yaweza kuwa si ya kweli. Vilevile, katika mfano mwingine huenda nataka kufahamishwa jambo ambalo silijui. Kwa mfano: 3.39: *"Je! shamba lile ni la ekari mia nne?"* Kauli 3.39, ina maana kuwa sijui kama lina ekari mia nne na ninataka nifahamishwe kama ni kweli kuwa lina ekari mia nne. Hivyo basi, sina ushahidi wowote kuwa shamba lile lina ekari mia nne na ni lazima nithibitishiwe na mtu ambaye anaufahamu ukweli huo. Mtu anapouliza swali huwa na tashwishi kuhusu jambo na hutaka hakikisho la jambo hilo. Kwingineko, mtu anapoahidi kufanya jambo, humaanisha kuwa kwa kweli anataka kulifanya jambo hilo. Hata hivyo, kanuni hii ya ukweli si lazima izingatiwe kwa sababu mtu anaweza kuamua kusema uongo kwa kiari au kwa kulazimishwa. Hivyo, anaweza kulilazimisha jambo lisilo la kweli kuwa la kweli na kuwashawishi watu kuliamini.

2) **Kanuni ya idadi:** Mtu anapaswa kuyasema mambo yanayotosheleza katika mazungumzo bila kuyazidisha wala kuyapunguza. Kwa mfano: 3.40: '*Hamisi ana watoto kumi na watano*'. Kauli 3.40, inamaana kuwa watoto wake Hamisi ni kumi na watano, wala sio zaidi au wachache kuliko kumi na watano. Vilevile, katika mazungumzo yafuatayo:

Kwa mfano: 3.41: *Juma: "kesi ya Suleimani iliamuliwa vipi?"*

*Adam: "Alitozwa faini."*

Mazungumzo haya yanamaanisha kuwa Juma alitozwa faini baada ya hakimu kuchunguza shtaka lake na wala sio kufungwa gerezani au kuachiliwa bure. Kanuni hii huipa kauli urejelezi wa kipragmatiki kwani huonyesha kuwa mambo yaliyotamkwa yana ujumbe ulio muhimu zaidi. Umaanisho pia unaweza kuwa na muktadha wa kiproposisheni katika sentensi ili kusisitiza jambo hilo. Kuwa mfano: 3.42: '*Hamisi ana watoto kumi na watano tu.*' Hivyo basi, kwa kutumia neno '*tu*', jambo latiliwa mkazo kuwa halikupunguzwa wala kuzidisha lile tuliloelezwa.

3)**Kanuni ya uhusiano:** Mtu anapaswa kusema jambo ambalo lahusiana na mazungumzo yaliyopo kwa wakati huo na wala sio ambalo haliafikiani kamwe. Kwa mfano: 3.43:

*Eve: "Je, unaweza kuniambia ni saa ngapi sasa?"*

*Jackline: "Dereva ameingia."*

Jibu la Jackline ni tofauti kabisa na jambo aliloulizwa na Eve. Huenda tukahusisha jibu lake na swali, kama labda Eve alikuwa anamngoja dereva wake, kisha akaona amekawia sana na kuamua kuuliza ilikuwa ni saa ngapi wakati huo. Labda Jackline hana uwezo wa kutambua ni saa ngapi, kwani labda hana saa ya mkono na mahali walipokuwa hakuna kifaa cha kutazama saa na kuuhusisha wakati huo na ule ambao dereva huwa anaingia. Kwigineko, huenda ikawa wakati huo huo alipoulizwa, alimwona dereva wa Eve akiingia na kuamua kumpa jibu hilo. Kama dereva wa Eve huwa anawasili wakati kama huo, basi ni jukumu lake kuhusisha jibu la Jackline

kuwa sasa ni wakati ambao dereva huingia kwa kawaida. Huwa muhimu kwa umaanisho kuhusishwa na chukulizi mwafaka ili mazungumzo yaambatane sawasawa, kisha kufasirika ipasavyo.

4)**Kanuni ya namna:** Mtu anapaswa kusema jambo kwa njia iliyowazi, inayoeleweka na kufasirika vyema bila kuficha jambo lolote. Kwa mfano: 3.44: *"Nipe Pesa!"* Kauli kama hii haijafafanua wazi msemaji anataka kiasi gani cha pesa. Labda anataka pesa nyingi ambazo msikilizaji huenda ikawa hana kwa wakati huo. Msemaji basi alipaswa kubainisha wazi anazitaka pesa ngapi, ili msikilizaji aweze kuamua kama inawezekana au la. Mazungumzo pia yanapaswa kuwa yenye uwazi.

Kwa mfano: 3.45: *Joyce: "Tafadhali nipe chakula."*

*Judy: "Twende."*

Jibu la Judy haliafikiani na swali alilouliza Joyce. Judy kujibu "*twende*" hafafanui ni wapi wanakokwenda na ni kwa sababu gani, ilhali Joyce anasema kuwa ana njaa na anaomba kupewa chakula. Pengine Judy alimjibu hivyo kwa sababu hakuwa na chakula chochote na alitaka waende mahali ambapo watapata chakula.

## 3.3 HITIMISHO

Sura hii vilevile, imejihusisha na mjadala kuhusu proposisheni na istilahi nyingine. Imejadili kuhusu vitendo usemi ambavyo huhusisha lokusheni, ilokusheni na palokusheni. Vitendo Usemi ni tendo lolote ambalo hufanywa na binadamu ambao hutenda wakati wanapotumia lugha kuwasiliana, ni uhusiano uliopo baina ya maneno na vifaa vinavyorejelewa. Sura hii yaeleza

kuwa: Kwanza, lokusheni ni kitendo cha kauli ambacho mtu hukitenda kwa kutamka jambo ambalo alitaka lifanywe. Pili, ilokusheni ni kitendo cha utendaji ambacho mtu hukitenda kwa kutambua kusudi la msemaji kwa kutaka jambo fulani litendwe. Tatu, palokusheni ni athari ambazo humpata mpokezi ujumbe baada ya kufahamu na kufasiri ujumbe uliokusudiwa na msemaji. Hivyo basi, kupitia kwa vitendo usemi washiriki katika mawasiliano huwasilisha proposisheni anuwai kwa kuafikiana baina yao wanapoelewana katika mazungumzo yao. Vilevile, vitendo usemi hivi huwapatisha watu walio na mitazamo tofauti na mmoja wao hufahamu vyema kusudi la mwenzake.

Imejadili kuhusu proposisheni katika chukulizi na umaanisho. Chukulizi ni jambo ambalo humpatanisha msemaji na msikilizaji katika mazungumzo. Matumizi bora ya sentensi katika mazungumzo hutegemea uchukulizi wa baadhi ya proposisheni ambazo wanaozungumza hupaswa kuzifahamu ili kufanikisha mawasiliano. Jambo lililolengwa hufahamika vyema na msikilizaji kwa sababu yeye huwa na ujumbe wa hapo awali kuhusu yaliyolengwa kuwasilishwa kwa chukulizi. Umaanisho ni jambo ambalo hutokea wakati ambapo msemaji hutamka kauli moja na kurejelea jambo alilokusudia. Umaanisho hufahamika kwa kuhusisha muktadha wa mambo yaliyosemwa na chukulizi iliyopo na uhusiano baina ya watu wanaoshiriki katika mazungumzo. Pia, sura hii imejihusisha na proposisheni katika miktadha tofauti ambayo husaidia hasa kutatua utata unaozuka kwa kutamka baadhi ya sentensi au kauli. Muktadha hutatua jambo hili kwani ni katika muktadha ambapo watu huzungumza na kufafanua zaidi walioyakusudia kuyawasilisha.

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA DATA

### 4.0 UTANGULIZI

Sura hii, tutajihusisha na uwasilishaji wa data kuhusu proposisheni. Tutatumia dhana kutoka kwa nadharia ya uhusiano ambazo tulizijadili, kisha muhtasari wa uchanganuzi huu kwa kuangazia jinsi dhana hizi hutumika kueleza proposisheni. Proposisheni hutokea mara tu msemaji anapotamka kauli fulani na kuzua mawazo katika akili za msikilizaji na humsababisha kufahamu kisha kufasiri ujumbe kutoka kwa msemaji. Chanzo cha data ya kimsingi ni katika maktaba, ambacho yahusisha mifano mbalimbali ya sentensi kutoka kwa wasomi kadha, na yenye kuonyesha proposisheni tofauti. Mifano kutoka kwa Wilson na Sperber itatumika, kama michoro ya kuonyesha ufasiri ujumbe, uzalizaji proposisheni na jukumu la muktadha.

### 4.1 DATA KUHUSU PROPOSISHENI

Utafiti huu kuhusu proposisheni umeijadili katika misingi ya nadharia ya uhusiano ambayo yadai kuwa uhusiano ni jambo la muhimu sana na huathiri utambuzi wa binadamu. Mambo ambayo mtu hutumaini kuyapata katika uhusiano yaweza kuwa tofauti kutegemea ni nani anayetoa ujumbe.

Kwa mfano: 4.1: '*Mtu akikutana na mwingine na hawafahamiani katika matatu, anatarajia machache kutoka kwake hasa katika mawasiliano na ambao unawahusu. Kwingineko, mtu akikutana na mwenzake ambaye anamfahamu katika matatu, atarajia mengi kutoka kwake hasa*

*katika mawasiliano na uhusiano utakuwa wa juu kwa sababu ni mtu waliyejuana naye tangu awali. kisha wana mengi yanayowahusu.'* Tukizingatia mfano 4.1, tunapata kuwa katika mawasiliano washiriki hutarajia jambo fulani kutoka kwa wanaozungumza nao. Vilevile, washiriki huelewa kwamba kauli huhusisha:

1) Jambo ambalo msemaji alikusudia kusema.

2) Jambo ambalo msemaji alikusudia kumaanisha.

3) Mtazamo wa msemaji kuhusu alilokusudia kulisema na kulimaanisha.

4) Mambo yote aliyoyakusudia msemaji kwa sababu kauli yaweza kulenga mambo kadha.

Kwa mfano: 4.2: *'Kitabu cha Sara kilipouzwa faida ilikuwa ndogo.'*

*4.3: Eunice: "Ungependa kula keki?"*

*Janet: "Nazingatia kwa makini ninachokula siku hizi."*

*4.4: Mercy: "Ni nini kitakachotendeka katika uchumi wetu?"*

*Juliet: "Bill atakuwa Rais wetu mpya.*

Kauli 4.2, yaweza kumaanisha ni:

1)Kitabu ambacho Sara anakimiliki.

2)Kitabu ambacho Sara amekiandika.

3)Kitabu ambacho Sara amekishika.

Ili kuamua proposisheni iliyokusudiwa na msemaji katika kauli hii, msikilizaji anapaswa kuyafasiri mambo haya na kutatua utata ambao ungezuka katika maana hasa iliyokusudiwa na msemaji. Mfano wa 4.3, unaweza kumaanisha kuwa:

1)Janet anatarajia Eunice ataelewa kuwa hataki keki.

2)Janet kulingana naye keki kama italiwa mara kwa mara, si bora kwa watu ambao wanazingatia masharti fulani katika ulaji wao.

3)Eunice anapaswa kulifasiri jambo hili kuwa ulaji wa keki mara kwa mara si njema sana kwa watu wanaozingatia masharti fulani kwa afya bora.


Kauli ya 4.4 yaweza kumaanisha kuwa:

1)Juliet anaposema Bill atakuwa Rais mpya anakusudia kueleza kuwa hakutakuwa na matatizo yoyote katika uchumi.

2).Anatarajia kuwa Mercy atapata chukulizi akilini mwake kuwa Juliet anamaanisha Bill atakapo kuwa Rais mpya matatizo yote ya kiuchumi yatakoma na uchumi huenda ukaimarika.

Kuafikiana na madai haya ya kauli 4.2, 4.3 na 4.4: Mchoro 4.3 kulingana na Sperber na Wilson (1985-2002), unahusu mfanyiko wa jinsi msikilizaji huufasiri ujumbe baada ya kuusikiliza kutoka kwa msemaji. Msemaji huwa na msukumo fulani, kutamka kauli, ujumbe hupelekwa na hupashwa kwa njia ya kuzungumza akitarajia kuwa msikilizaji yu makini kusikiza, kisha msikilizaji katika akili zake tambuzi huupata utaratibu fulani ili aweze kuunda fasiri na kuuelewa ujumbe huo kama ilivyokusudiwa. Mwishowe msikilizaji huamua kama atakubali, kukataa au kuifanya kauli hiyo kuwa bora zaidi kwa kutoa maoni yake.

## 4.2 MFANYIKO WA UFASIRI UJUMBE



ineko, msikilizaji anapaswa kuutambua muktadha unaojitokeza papohapo.

ıfano: 4.5: Kutoka kwa Biblia (Luka 23:1-2)

*5.1) Kisha wanachama wote wakaamka.*

*5.2) Wakamleta mbele ya Pilato.*

*5.3) Walianza kumshutumu wakisema,*

*5.4) Tulimpata Mwanamume huyu akikiuka sheria za nchi.*

wa proposisheni inayoelezwa katika kauli ya kwanza 4.5, ni kuwa msikilizaji anapaswa ımbua wanaorejelewa kama *wanachama* ili kuwahusisha na yaliyosemwa. Kauli ya pili ısikilizaji hatapata urejelezi kuwa; *wakampeleka* katika kauli hii lakini, anapaswa nbua anayerejelewa kuwa ni ***Yesu*** kwa sababu ni jambo lililo katika Biblia. Mfano wa pili tatu 4.5, msikilizaji anapaswa pia kumfasiri ni nani anayerejelewa kwa kusema *ıtumu* na *mwanamume huyu* kuwa vilevile ni ***Yesu***.

le, msikilizaji anapaswa kuunda umaanisho uliokusudiwa na msemaji katika kauli yake.

ıfano: 4.6:


*Jane:* *"Ulikitazama Kipindi cha Vijana katika Runinga?"*

*Michael*: *"Mimi huwa sitazami Runinga."*

lha katika 4.6; ni kuwa Michael hamjibu Jane moja kwa moja. Proposisheni inayorejelewa Jane habari kuwa Michael huwa hana hamu ya kutazama Runinga. Michael naye atapata ıu kuwa Kipindi cha Vijana huonyeshwa katika Runinga na hakukitazama kipindi kile.

Pia. tunafahamu kuwa proposisheni hujengeka katika akili za anayekusudia kuuwasilisha ujumbe na hivyo basi: Mchoro 4.4 kulingana na Sperber na Wilson (1985-2002), unaonyesha jinsi proposisheni huundwa akilini mwa binadamu ambaye huwa ni msemaji baadaye ya kuitamka kauli kwa kumlenga mikilizaji, ambaye naye huunda proposisheni hiyohiyo iliyokusudiwa na msemaji akilini mwake. Ujumbe ulioundwa na kuwa proposisheni hupelekwa kwa mikilizaji kwa mfumo ambao humwezesha msikilizaji kuutathmini ujumbe huo na kuamua kuwa ni wenye mantiki au la. Mambo yaliyotamkwa huambatanishwa na muktadha unaorejelewa katika mazungumzo. Hatimaye maumbo ambayo hujulikana kama proposisheni huundwa.

## 4.3 UZALISHAJI WA PROPOSISHENI




Kuna tofauti iliyopo baina ya mambo yaliyo katika Semantiki na ufasiri wa Kipragmatiki. Kwa mfano: 4.7: *"Sue na Joe wameoana."* Msemaji anapotamka kauli hii huenda anatarajia msikilizaji kufasiri na kupata proposisheni kuwa:

1) **Sue na Joe hutembea pamoja wakati wote.**

2) **Mwanamke na mwanamume hutembea pamoja wakati wote wakiwa wameoana.**

3) **Huenda ikawa Sue na Joe wamefanya harusi.**


Hata hivyo, mfano 4.7, una maana katika semantiki kuwa wao wameoana, kisha kuna ufasiri wa kipragmatiki ambao ni kulingana na watumizi lugha kuwa watahusisha kauli hii na mambo kadhaa, kama yalivyo katika proposisheni za kauli 4.7.

Kwa mfano: '*Watu waliooana mara nyingi hutembea pamoja.*'

'*Watu ambao huoana huwa ni mke na mume.*'

Kwingineko, tunaelezwa kuwa muktadha ni jambo ambalo ni muhimu sana katika uelewa wa proposisheni kwa sababu ndio huzua mazungumzo ambayo huundwa kwa kauli tofauti. Hivyo basi, mchoro 4.5 kulingana na Sperber na Wilson (1985-2002), ni kuhusu umuhimu wa muktadha. Muktadha huwepo katika fahamu za wanaoshiriki kwenye mazungumzo, ambapo ujumbe hupitishwa baina msemaji na msikilizaji kisha kubadilishana mawazo kwa njia ya kupashana kauli na proposisheni huudwa baina yao. Baadaye, mawazo huudwa akilini mwa kila anayeshiriki kisha kuthibitishwa kama yanafaa au hayafai kamwe.

## 4.4 JUKUMU LA MUKTADHA




Kusudi kuu la msemaji ni kwamba msikilizaji atatambua lengo lake la kumwarifu kuhusu hali ya mambo fulani. Binadamu anaouwezo wa kuhusisha mambo yaliyo kusudiwa na uelewa wake.

Kwa mfano: 4.8:

*Peter: "Unataka kunywa kahawa?"*

*Maria: "Kinywaji cha kahawa kitanifanya nikae macho badala ya kulala."*

Maria hana jibu la moja kwa moja kuwa anataka kunywa kahawa au la. Jambo hili linamfanya kukiuka kauli ya uhusiano katika mojawapo wa kanuni za ushirikiano na Grice (1975, 1978). Peter anapaswa kuwa na chukulizi kwamba Maria hataki kunywa kahawa kwa sababu atakaa macho ilhali anataka kulala. Washiriki katika mawasiliano wanapaswa kufahamu mambo kadha kama vile:

1) Ujumbe walio nao washiriki katika mawasiliano.
2) Mitindo inayotumiwa katika kurejelea jambo.
3) Uhusiano ni nini na jinsi ya kuutimiza.
4) Jukumu la uhusiano katika mawasiliano.

Katika mawasiliano kwa njia ya mazungumzo, msemaji huwasilisha maana zilizo anuwai japo huenda akawa hana jambo lolote maalum alilolenga kulirejelea. Jambo ambalo humfanya msikilizaji kutambua alilokusudia kuliwasilisha msemaji ni kuwa, kauli huwa na maumbo yenye mantiki ndani yake. Maumbo haya husawiriwa kiutambuzi na msemaji huyachagua ili kumpa msikilizaji mfumo wa kuweza kuuchanganua ujumbe ipasavyo. Hivyo basi, mawasiliano ya aina hii hutimiza lengo lake kuu la kufahamu ujumbe na kufasiri jambo lililokusudiwa. Utaratibu wa ufahamu katika nadharia ya uhusiano hutumia kiasi kidogo tu cha juhudi katika athari za kiutambuzi, hutathmini mawazo kwa utaratibu na hukoma punde tu matarajio ya uhusiano

yanapotimia. Kwa ujumla msikilizaji anaweza kuwa mwenye uhusiano fulani kwake lakini, akawa na matarajio maalum kuhusu jinsi kauli itakuwa ya kumhusu yeye, kwa kuzingatia athari za kiutambuzi ambazo huenda washiriki katika mazungumzo wakawa nazo.

Kwa mfano: 4.9:

*Paul: "Je, Mark alikulipa pesa zako?"*

*Alex: "La, alisahau kwenda benki."*

Matamshi ya Paul yanaweza kutumia utaratibu wa ufahamu katika uhusiano kuunda mawazo kuhusu kauli ya Alex, '*alisahau kwenda benki'*. Paul anachukulia kuwa kauli ya Alex kwa kuifasiri jinsi inavyomhusu kuwa Mark hakumlipa pesa zake kwani alisahau kwenda benki. Paul hasa anataka kufahamu ni kwa nini Mark hakumlipa Alex deni lake. Hivyo basi, anachukulia kuwa '*kusahau kwenda benki'* ni jambo ambalo laweza kumfanya mtu kukosa kulipa deni alilo nalo. Muktadha kama huu unaweza kuibua mawazo kadha kama vile: Kwanza, msilizaji na msemaji wanafahamu kuwa kuna shirika liitwalo benki ambalo mojawapo wa kazi yake ni kuhifadhi fedha hasa kama mtu ana akaunti pale. Pili, mara tu anapohitaji kiasi fulani cha pesa atapata kutoka kwa akaunti yake. Hivyo basi, mazungumzo baina ya Paul na Alex yanatupa uelewa kuwa Mark hakukataa kumlipa Alex pesa zake lakini ni kwa sababu alisahau kwenda kuzichukua benki, hana budi kumlipa punde tu atakapokumbuka kwenda benki.

Watu ambao hushiriki katika mazungumzo huwa na matarajio ambayo hunuia kuwa yatatimia. Matarajio yao ni kama vile:

1)Msemaji kuuwasilisha ujumbe alioukusudia kwa msikilizaji.

2)Msemaji kuueleza ujumbe wake kwa njia iliyo mwafaka zaidi.

3)Msemaji kuhakikisha kuwa msikilizaji anaufahamu na kuufasiri ujumbe wake barabara.

4)Msikilizaji anapaswa kuwa na hakika kuwa ameuelewa bayana ujumbe uliokusudiwa na msemaji.

5)Msikilizaji anastahili kuzipata athari alizokusudia msemaji baada ya kuupokea ujumbe.

6)Msikilizaji anatarajiwa kulifanya jambo fulani kwa kuzingatia athari alizozipata baada ya kuupokea ujumbe kutoka kwa msemaji.

Hivyo basi, jedwali 4.6 kulingana na Sperber na Wilson (1985-2002), linahusu mambo ambayo washiriki katika mazungumzo huyatarajia kuwa yatatokea. Mambo haya yanahusu jambo ambalo ni lenye uhusiano unaofaa hasa kwa msikilizaji kuwa hulichagua linalomfaa zaidi kutoka kwa msemaji. Msemaji huweza kufahamu kisha kuelewa kusudi la msemaji kutamka kauli maalum, hatimaye hupata athari fulani na kuchukua hatua mwafaka kama kukubali au kulikataa jambo lile.

## 4.5 MATARAJIO KATIKA UHUSIANO

| Athari katika mawasiliano | Matarajio katika mazungumzo |
|---|---|
| 1)Alex amesema kwa Paul, 'Alisahau kwenda *benki*: **A** – kumrejelea Mark. *Benki*-kurejelea; **sekta ya kushughulikia fedha** au **kando ya mto**. | Kuambatisha maumbo ya kiisimu yaliyofasiriwa kuhusu kauli iliyo tamkwa na Alex kuwa ni maelezo kuhusu tabia za Mary. |
| 2)Kauli ya Alex itakuwa yenye uhusiano wa hali ya juu kwa Paul. | Matarajio kutokana na tabia ya Alex na kuafikiana na mawazo ya hapo awali yanayoeleza tarajio lililo na uhusiano na yaliyotamkwa. |
| 3)Kauli ya Alex itakuwa yenye uhusiano kama itaeleza ni kwa nini Mark hajalipa pesa alizo nazo za Alex. | Matarajio kutokana na kauli (2), pamoja na maelezo yake yatakuwa yenye uhusiano wa hali ya juu zaidi kwa Paul. |
| 4)Kusahau kwenda Benki-**sekta ya kushughulikia fedha,** humfanya mtu kukosa uwezo wa kulipa deni analodaiwa. | Wazo la kwanza kumpata Paul, pamoja na mambo mengine yanayofaa yatatimiza matarajio katika kauli (3). Kukubali kuwa kauli ya Alex ni ya kweli. |

| | |
|---|---|
| 5)Mark alisahau kwenda Benki-**sekta ya kushughulikia fedha.** | Hakikisho la kwanza kuhusu maumbo ya kiisimu katika kauli ya Alex, ambayo itatokea akilini mwa Paul na yaweza kuunganishwa na kauli (4) ili kutimiza kauli (3). Kukubalika kama chukulizi ya kauli ya Alex. |
| 6)Mark hakuweza kumlipa Alex deni lake kwa sababu alisahau kwenda Benki-**sekta ya kushughulikia fedha.** | Kurejelewa kauli (4) na kauli (5), ili kutimiza kauli (3) na kukubali kauli ya Alex kama yenye kuthibitisha jambo hilo. |
| 7)Mark ataweza kumlipa Alex deni lake wakati atakapo kwenda Benki-**sekta ya kushughulikia fedha.** | Kutokana na kauli (7) na ufahamu wa hapo awali, ni mojawapo wa chukulizi ya kuwa kauli ya Alex pamoja na kauli (6), ili kutimiza kauli (2). |

## 4.6 KUWALINGANISHA: SPERBER NA WILSON DHIDI YA GRICE

Bali na kuitumia nadharia ya uhusiano katika utafiti wetu ili kuchanganua proposisheni, vilevile kama tulivyotaja katika sura ya kwanza na kuzieleza kanuni hizi za ushirikiano za Grice katika sura ya tatu. Tulizitumia kanuni hizi kwani zinaafikiana kwa kiasi kikubwa na kanuni katika nadharia ya uhusiano ya Sperber na Wilson. Basi, jedwali 4.7.1 na 4.7.2 kulingana na Sperber na Wilson (1985-2002), lahusu dhana za kimsingi na kanuni baina ya Sperber na Wilson dhidi ya Grice. Katika utafiti wetu tumejadili proposisheni kwa kuzingatia sehemu ya nadharia ya uhusiano ambayo ni ya Wilson na Sperber na wala sio dhana zote katika nadharia yenyewe. Hata hivyo, tumezihusisha kanuni za Grice, kwa kuwa ni muhimu katika uchanganuzi wa proposisheni. Hivyo basi ni muhimu kuwalinganisha kwa sababu kuna uhusiano uliopo baina ya dhana zza kimsingi na kanuni zao. Dhana za Wilson na Sperber na zile za Grice, japo zimepewa istilahi tofauti tunapata kuwa zina malengo sawa. Hii ni kwa sababu jukumu lao kuu ni *kuwasiliana*, kisha kuhakikisha kuwa ujumbe kutoka kwa msemaji *utafasiriwa* ipasavyo na msikilizaji. Hata hivyo kuna mambo muhimu ambayo ni lazima yazingatiwe na washiriki katika mazungumzo ili waweze kuafikiana. Mambo haya yanajumlisha hatua zinazofaa kama vile; *dhana za kimsingi* katika mawasiliano pamoja na *kanuni* mwafaka za kuthibitisha kuwa mawasiliano yametimia na kufasiriwa kama ilivyokusudiwa.

### 4.6.1 DHANA ZA KIMSINGI

| GRICE | SPERBER NA WILSON |
|---|---|
| **-KANUNI YA USHIRIKIANO** | **-UHUSIANO** |
| Kanuni ya Ukweli | -Si muhimu kwa sababu ya uhusiano |
| Kanuni ya Idadi | -Athari za kiwango cha juu kiutambuzi |
| Kanuni ya Namna | -Juhudi kiasi cha kiutambuzi |

**4.6.2 KANUNI ZAO**

| GRICE | SPERBER NA WILSON |
|---|---|
| Msikilizaji ndiye muhimu | -Msemaji ndiye muhimu |
| Muktadha wa awali | Muktadha kulingana na Msikilizaji |
| -Kanuni nyingi | -Kanuni chache |
| Jukumu ndogo la ufasiri | Jukumu pana la ufasiri |

## 4.7 PROPOSISHENI KATIKA MIKTADHA TOFAUTI

Bussmann (1996: 100-101) anasema kuwa muktadha hurejelea elementi zote zinazohusiana katika mawasiliano, kama vile muktadha katika mazungumzo au maandishi, muktadha katika mahusiano baina ya msemaji na msikilizaji kwa kuzingatia maarifa yao na mitazamo yao. Tukifafanua maelezo haya ya Bussmann (1996) ni kwamba muktadha huwa tofauti kulingana na mada au suala linalozungumziwa. Vilevile, unaweza kuwa rasmi au usio rasmi, kama; baina ya mwajiri na mwajiriwa utakuwa ni rasmi ihali, baina ya marafiki utakuwa si rasmi.

Msemaji huwa na kusudi fulani wakati wote anapotumia lugha. Kama vile, mwalimu huenda akamwambia mwanafunzi aliyechelewa darasani kwa muda wa takribani dakika thelathini, kwa mfano: 4.8: "*umefika mapema leo.*" Mwalimu amelitamka jambo hili kwa kinaya kwa sababu, mwanafunzi kwa hakika hakufika mapema. Hivyo basi, mwalimu kuwa anatumia kinaya pengine kumtia changamoto ili siku nyingine asichelewe kufika darasani. Pragmatiki hukusudia kufafanua maana halisi iliyopo katika kauli zilizo na maana isiyo ya moja kwa moja, kama iliyotamkwa na mwalimu. Kwingineko, muktadha ni muhimu katika ufasiri na ufafanuzi wa maana ya sentensi. Wazungumzaji hubainisha maana na muktadha uliopo katika kauli tofauti tofauti. Jukumu la muktadha katika ufasiri kwanza, huwa na fasiri maalum iliyokusudiwa na pili, huhimili fasiri, iliyokusudiwa. Hata hivyo, proposisheni huwepo katika muktadha.

Kwa mfano: 4.9:

*a)* *Kuna mwanamume na mwanamke walioketi sebuleni, mwanamke ameketi akisoma kwa furaha, mwanamume amechoka kisha anaelekea dirishani na kutazama nje na mwanamume huyo anajitayarisha na hatimaye anaondoka.*

Muktadha huu utafasirika kuwa; *mwanamke aliyeketi akisoma kwa furaha* kama; mwanamke aliyetajwa hapo mwanzo. Vilevile, *dirisha* ambalo mwanamume alilielekea lapaswa kufasiriwa kuwa ni; *dirisha lililo sebuleni.* Msemaji baadaye anabadilisha mandhari na itabidi tuchukulie kuwa muktadha ujao umo sasa katika mandhari mapya.

*b)* *Mwanamume anaelekea kwenye klabu, anaagiza kinywaji na kuzungumza na mhudumu mmoja wa pale Klabuni, kisha anaanza kucheza densi na msichana mrembo mwenye nywele ndefu nyeusi na anakuwa na wakati mwema.*

Muktadha huu unafasirika kuwa chochote kinachotendeka hapa kinamhusu mwanamume tuliyeelezwa kumhusu hapo awali akiketi sebuleni na sasa yumo katika klabu anapoagiza kinywaji, anazungumza na mhudumu, anacheza densi na kuwa na wakati mwema kwenye klabu, msemaji pia anabadilisha mandhari tena:

*a) Kisha anaenda nyumbani, anampigia msichana yule na mkewe anayasikia mazungumzo yao.*

Tunachukulia kuwa ni mwanamume yule yule ambaye sasa amerudi nyumbani katika mandhari ya hapo awali sebuleni ambapo tulielezwa kumhusu kwa mara ya kwanza. Tunafasiri kumpigia kuwa ni simu na msichana yule kuwa ni yule mrembo aliye na nywele ndefu nyeusi, ambaye alicheza naye densi na akawa na wakati mwema.

Proposisheni katika muktadha "a" ni kuwa:

**1)Kuna mwanamke na mwanamume walio nyumbani na wameketi sebuleni.**

**2)Mwanamke ana furaha.**

**3)Mwanamke huyo anasoma.**

**4)Mwanamume amechoka.**

**5)Huenda ikawa mwanamume huyo amechoshwa na hali ya kuwa mumewe anasoma na labda alitaka walizungumze jambo fulani.**

**6)Mwanamume huyo ameamua kuondoka.**

Proposisheni katika muktadha “b” ni kuwa:

**1)Mwanamume alipoondoka alielekea kwenye klabu.**

**2)Baada ya mwanamume huyo kuagiza kinywaji anazungumza na mhudumu mmoja katika klabu.**

**3)Mwanamume huyo anacheza densi na msichana pale katika klabu.**

**4)Msichana mwenyewe ni mrembo na ana nywele ndefu nyeusi.**

**5)Mwanamume huyo anakuwa na wakati mwema katika klabu.**

Proposisheni katika muktadha “c” ni kuwa:

1) **Baadaye mwanamume huyo anarejea nyumbani.**
2) **Mwanamume alipowasili nyumbani alimpigia simu msichana yule mrembo mwenye nywele ndefu nyeusi ambaye alicheza naye densi kwenye klabu na kuwa na wakati mwema .**

3) **Mkewe aliyasikia mazungumzo baina yake na msichana yule.**

Hivyo basi, kulingana na miktadha hii tunaona kuwa kuna umuhimu wake katika pragmatiki. Hii ni kwa sababu muktadha husaidia katika kufafanua utata ambao unaweza kuwepo kama tungeelezwa tu kumhusu mwanamke na mwanamume wakiwa sebuleni bila ya kufahamishwa matukio yaliyofuata, ingekuwa vigumu kufahamu ni nini kilichotendeka kuwahusu mwanamke na mwanamume huyo.

Muktadha hubainisha maana katika kauli kwa viwango vitatu katika uchanganuzi wa matini au diskosi. Kwanza, hufanya kuwa bayana sentensi iliyotamkwa. Pili, huifanya wazi proposisheni iliyoelezwa. Tatu, huifanya bayana proposisheni iliyopo kwa kuhakikisha kuwa imeelezwa kwa aina moja ya msukumo wa kiilokusheni ambao unafaa zaidi. Viwango hivi vitatu hukusudia kuufanya muktadha kuhusiana na kinachosemwa. Maana katika kauli pia hurejelea chukulizi iliyopo na muktadha hufafanua ujumbe katika kauli hiyo. Kwa mfano: 4.8: "*Walivuka daraja usiku wa manane.*" Kauli kama hii yaweza kusababisha utatu kuielewa na kuifasiri. Muktadha ndio unaoweza kutatua utata kama huu kwa sababu tutaelezwa ni akina nani waliokuwa safarini, waliivuka daraja ipi na vilevile, waliivuka vipi. Hatuwezi kufahamu proposisheni iliyopo katika kauli kama hii ila tu kama itafafanuliwa zaidi kupitia kwa muktadha.

Muktadha katika kauli wapaswa kuhusiana na mambo yanayorejelewa na kuhusishwa na muktadha huo. Lugha ambayo hutumiwa katika mazungumzo huwa na mbinu zake za kimuundo ambazo pia hujulikana kama zenye mitindo tofauti, na humfanya mshiriki katika mazungumzo kuelewa vyema kisha kuhusika vyema zaidi katika mtiririko wa mazungumzo.

Kwa mfano: 4.9: *Musa: "Ni nani aliyemuua mbuzi?"*

*Halima: "Jack. Jack alimuua. Jack alimuua mbuzi.*

*Farida: "Alikuwa mbuzi ambaye jack alimuua."*

*Rukia: "Kitu ambacho Jack alikiua ni mbuzi."*

Kauli ya Musa inamlenga Jack, lakini majibu ya Farida na Rukia yanamlenga mbuzi. Jambo hili laufanya muktadha kuwa mgumu kuufahamu. Proposisheni katika muktadha huu ni kuwa:

1) **Kuna mtu aliyemuua mbuzi.**
2) **Musa anataka kufahamishwa ni nani aliyemuua mbuzi.**
3) **Halima anafahamu kuwa Jack ndiye aliyemuua mbuzi kulingana na jibu analompa Musa.**
4) **Farida na Rukia pia wanafahamu kuwa Jack ndiye aliyemuua mbuzi japo hawataki kulitaja jambo hilo moja kwa moja.**
5) **Farida na Rukia wanakitaja kitu ambacho Jack alikiua kuwa ni mbuzi.**

Hata hivyo, muktadha wenyewe waeleweka kuwa muuaji wa mbuzi ni Jack, hii ni kwa sababu Eric alimtaja Jack kuwa ndiye aliyemuua mbuzi, nao Doris na Ben wanasema kuwa kitu ambacho Jack alikiua ni mbuzi.

Pragmatiki hujihusisha na; Kwanza, uhusiano uliopo baina ya muktadha na maana ya sentensi, na pili, uhusiano uliopo baina ya maana ya sentensi, muktadha na maana ya msemaji. Vipengee fulani katika pragmatiki huwa na muktadha ambao huzua maana katika semantiki. Muktadha unatumia nafsi na hutegemea matumizi yake kwa mfano: 4.10: Nafsi ***Yeye***

*Judy: "Unamwona yule mototo wa kike pale? Yeye ni mrembo."*

*Paulina: "Hakuna msichana yeyote hapa aliye na tashwishi kuwa* yeye *ni mrembo."*

Hivyo basi, '*yeye*' ni nafsi ambayo itamrejelea msichana yule mrembo kulingana na matumizi yake katika muktadha. Proposisheni iliyopo katika muktadha huu ni kuwa:

1) **Judy anafahamu kuwa kuna mtoto wa kike ambaye ni mrembo.**
2) **Judy anamrejelea mrembo mahsusi na kumweleza Pauline kuhusu jambo hilo.**
3) **Paulina vilevile anafahamu kuwa msichana huyo ni mrembo.**
4) **Kulingana na Paulina, wasichana wengine pia wanahakika kuwa msichana yule ni mrembo.**
5) **Judy amemrejelea msichana yule kama mtoto wa kike ili kuusisitiza urembo wake.**

## 4.8 PROPOSISHENI KATIKA SEMANTIKI NA PRAGMATIKI

Tuki (1990:47) wanasema kuwa Pragmatiki ni kitengo cha taaluma ya isimu ambayo huchanganua lugha kwa kutegemea maoni ya mtumizi, hasa uchaguzi wa miundo ya maneno anaoufanya, vikwazo vya kijamii anavyokabiliana navyo katika kutumia lugha na athari za kijamii katika matumizi ya lugha. Kwingineko, Tuki (1990:52) wanaendelea kusema Semantiki ni tawi la isimu ambalo hushughulikia maana katika lugha. Kulingana na maelezo haya, washiriki katika mazungumzo hutumia lugha kulingana na vile msikilizaji anauelewa ujumbe wa kutoka kwa msemaji. Vilevile, tunapata maoni yao kama watumizi lugha huamua kile watakachokitamka katika kauli zao.

Lugha itachukuliwa kuwa ni mfumo wa ujumbe, itahusisha maana na ishara kadha. Ferdinard de Saussure (1916) anarejelea jambo hili kama *kiashiria* na *kiashiriwa*. *Kiashiria* ni kitu ambacho hutumika ili kurejelea au kuonyesha. *Kiashiriwa* ni kitu ambacho hasa kinachorejelewa au kuonyeshwa. Kwa mfano: 4.11: "*Kitabu kile ni changu.*" Kauli hii ina kiashiria ambacho ni *kile* na kinatumika kurejelea kitabu, kisha kiashiriwa ni *kitabu* ambacho ninakirejelea kuwa ni changu. Maana katika semantiki hutegemea msemaji, msikilizaji na muktadha. Hivyo basi, msemaji lazima aafikiane na msikilizaji ili muktadha utakaohusika katika mazungumzo yao uwe na mafanikio. Proposisheni ambayo huwa katika jambo lililosemwa hutegemea uelewa na ufasiri alionao mpokezi ujumbe baada ya msemaji kutamka na kujieleza kupitia kwa kauli. Proposisheni katika 4.11, ni kuwa:

1) **Mimi ninacho kitabu.**
2) **Mimi ninakiona kitabu change.**
3) **Kitabu ambacho ni change ni kile.**
4) **Mimi nina uwezo wa kukifahamu kitabu changu.**

Pragmatiki ni utafiti unaohusu uhusiano uliopo baina ya umbo la Kisiimu na watunzi wa maumbo hayo. Pragmatiki pia huchanganuliwa na binadamu kwa misingi ya *ufahamu* na *ufasiri* wake. Mtu anaweza kuzungumza kuhusu maana iliyokusudiwa na watu wengine, chukulizi zao, malengo yao na matendo yao, kama vile; *kusihi* wanayoyatenda wakati wanapozungumza. Watu katika mazungumzo wanaweza kurejelea mambo fulani na kuzua mambo mengine ambayo hawakuyakusudia.

Kwa mfano: 4.12:

*Jackline: "Ulifanya hivyo?"*

*Maria: "Nani ambaye hangedhubutu kufanya vile?"*

Muktadha huu unaeleweka na mtu ambaye hajahusika katika mazungumzo haya lakini, hana habari kuhusu ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa. Jambo hili litamfanya kuwazia kuhusu muktadha huu na kuufikiria kwa kina kuuhusu ujumbe wake. Hivyo basi, Jackline na Maria wamezua jambo kwa mtu tofauti kuutafakari ujumbe uliolengwa. Pragmatiki basi, ni kuhusu jinsi watu huzua fasili ya dhana akilini baina yao kiisimu lakini ni lazima ufahamu uwepo kuhusu jambo lililo akilini.

Proposisheni katika 4.12, ni kuwa:

1) **Maria alipaswa kufanya jambo.**
2) **Jackline anataka kufahamu kama Maria alilifanya jambo lile.**
3) **Kulingana na Maria ni jambo la kawaida kuwa kila mtu angedhubutu kufanya jambo lile.**
4) **Jambo lenyewe halitajwi ni lipi, japo Jackline na Maria wanalifahamu vyema jambo hilo.**

Vilevile, pragmatiki ni utafiti kuhusu uelewa wa matendo yaliyokusudiwa na binadamu. Huhusisha kufasiri matendo yanayofanywa ili kukamilisha lengo fulani. Pia, maana za aina kadha katika mawasiliano hushughulikiwa. Kwa mfano: 4.13: *"mwokoaji anatakakumsaidia mtu ambaye anaelekea kuzama kwenye kidimbwi anapoogelea, kisha mwokoaji anamtupia mpira wa*

*kuchezea kandanda. Mwokoaji anachukulia kuwa mwogeleaji anafahamu kuwa mpira huo ni mwepesi na hauwezi kuzama majnii, hivyo basi anapaswa kuushika mpira ule ili asizame majini".* Hivyo basi, mwokoaji ameamua kukitumia kitu ambacho kimo karibu naye sana ili kujaribu kumwokoa mtu huyu anayezama. Kifaa anachokitumia ni mpira wa kucheza kandanda. Proposisheni iliyopo katika 4.13, ni kuwa:

1) **Kuna mtu anayeogelea katika kidimbwi.**
2) **Huenda ikawa mwogeleaji huyu hana ujuzi mwingi wa kuogelea kwa sababu anaelekea kuzama.**
3) **Mwokoaji ametambua kuwa kuna mtu anayezama pale kwenye kidimbwi.**
4) **Mwokoaji anafanya juhudi za kujaribu kumwokoa mwogeleaji yule.**
5) **Mwokoaji anamtupia mwogeleaji yule mpira wa kucheza kandanda.**
6) **Mwogeleaji yule anapaswa kujitahidi kuushika mpira ule, ile aelee majini badala ya kuzama.**

## 4.9 HITIMISHO

Sura hii imejihusisha na uchanganuzi wa data kuhusu proposisheni. Hivyo basi, uhusiano ni muhimu kwani:

1) Huhitajika ili kuwa na vichocheo vya kiwango cha juu vitakavyochanganuliwa na mfumo wa kuupeleka ujumbe.
2) Huwezesha watumizi wa mfumo huu wa kuupeleka ujumbe kuchagua muktadha wa kiwango cha juu katika utambuzi ili vichocheo hivyo vieleze vyema mawazo yaliyopo katika mifumo ya kimsingi.

3) Huamua ni dhana zipi za hapo awali zitakazochaguliwa katika mpango wa kuyatathmini mawazo ili kukubali au kukataa rejelezi muhimu katika kumbukizi.

Kwingineko, mikakati ya msikilizaji:

1) Hulenga ujumbe uliokusudiwa na msemaji kwani, huurejelea muktadha wa hapo awali wa msemaji.
2) Hulenga ujumbe ulio na uhusiano wa kiwango cha juu zaidi kwake kwani, anaweza kuamua kuukataa ujumbe uliokusudiwa na msemaji kisha kuutilia maanani ule ambao anaudhani kuwa ni muhimu katika muktadha uliopo.

Jambo la mwisho katika sura hii kujadiliwa ni proposisheni katika Semantiki na Pragmatiki. Tumeona kuwa pragmatiki ni kipengee cha isimu ambacho hutumika kutafiti lugha kulingana na mtazamo wa watumizi lugha. Huhusisha uhusiano uliopo baina ya msemaji na msikilizaji. Hutafiti kanuni zinazohusika katika mazungumzo, kwa upande mwingine Semantiki ni kitengo cha isimu ambacho hutafiti maana katika lugha. Huchanganua na kueleza maana halisi katika lugha, maana ya maneno hasa katika ukuaji wake na mabadiliko ambayo yanaweza kuwepo katika maana zake. Semantiki na Pragmatiki ni dhana mbili zinazohusishwa katika kazi hii kwa sababu ya kubainisha maana iliyopo ndani ya proposisheni imo katika taaluma zote mbili, kwa kurejelea maana iliyopo katika kauli na maana kulingana na watumizi lugha.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 UTANGULIZI

Sura hii itajihusisha na muhtasari kuhusu uchanganuzi wa proposisheni, mahitimisho kurejelea yaliyojadiliwa katika sura zote za utafiti huu, mapendekezo katika tafiti za wakati ujao. Vilevile, sura hii itashughulika na suala la kuthibitisha kama nadharia tete pamoja na madhumuni ya utafiti huu ni mambo ambayo yamekubalika au kukataliwa baada ya utafiti kukamilika.

### 5.1 MUHTASARI NA MAHITIMISHO

Sura ya kwanza tulijadili kuhusu tatizo la utafiti huu ambapo proposisheni imejadiliwa kwa misingi ya kuwa na maana katika pragmatiki, kueleza nadharia itakayotumika katika kuchanganua dhana ya proposisheni, kujadili yaliyoandikwa kuhusiana na proposisheni. Kusudi la utafiti huu ni hasa kutathmini nadharia tete tatu ambazo ni pamoja na; kujadili dhana ya proposisheni kwa kurejelea maana yake katika pragmatiki, kutambua umuhimu wa muktadha katika uelewa wa dhana ya proposisheni na mwishowe kufahamu kuwa proposisheni imo katika pragmatiki na semantiki. Uchanganuzi katika utafiti huu pia unajihusisha na madhumuni tatu ambapo; yameeleza jinsi dhana ya proposisheni ina maana katika pragmatiki, tutaona kuwa muktadha ni muhimu katika uelewa wa dhana ya proposisheni, pia tutabainisha kuwepo kwa proposisheni katika pragmatiki na semantiki kwa pamoja.

Sura ya pili tulijadili dhana ya proposisheni ambayo ni maana iliyopo katika kauli iliyotamkwa, kisha msikilizaji anapaswa kuifasiri na kuibua maana hasa iliyolengwa na msemaji. Ni kipengee hasa cha kipragmatiki kwa sababu hutegemea maana kulingana na watumizi lugha maalum kama vile, ***Kiswahili***. Huhusisha washiriki katika mazungumzo ambao hutamka kauli ili kuwepo na proposisheni. Hivyo basi, proposisheni haiwezi kuwepo kama hakuna watu wanaozungumza. Maana yake hutegemea hasa maafikiano baina ya kauli ya msemaji na ufasiri wa msikilizaji kuwa wote wawili huibuka kuilenga maana moja.

Vilevile, tuliona kuwa proposisheni huwa za aina tatu ambazo ni: Kwanza, *proposisheni ya hakika*. Aina hii ya proposisheni hulenga imani ya msikilizaji. Sharti msemaji awe na uhakika wa jambo analolisema kwani proposisheni yapaswa kuwa ya kweli wala si ya uongo. Msikilizaji huenda akawa na maoni tofauti na ya msemaji na anao uhuru wa kulipinga jambo lililotamkwa, hata kama kauli ya msemaji ilikuwa ya kweli. Pili, *proposisheni ya thamani*. Hulenga maoni ya msikilizaji. Msemaji huwa na mambo kadha ambayo humpa msikilizaji jukumu la kuyalinganisha na kulichagua ni lipi lililo na thamani zaidi. Hata hivyo, maoni ya msikilizaji yanaweza kuwa tofauti na maoni ya watu wengine kwani ana uhuru wa kuchagua alitakalo. Tatu, *proposisheni ya sera*. Aina hii ya proposisheni hutoa mawazo kuhusu jambo fulani kama hatua mwafaka ya kukabiliana na baadhi ya sheria za makubaliano kati ya washiriki katika mazungumzo ambao huwa hasa wamepatanishwa pamoja na kaida fulani. Hivyo basi washiriki hawana budi ila kuzingatia sheria mahsusi bila kuzikiuka.

Kwingineko, tukapata kuwa proposisheni nzuri huwa na ishara zake. Ishara hizi ni mbili na ambazo ni: Kwanza, *ishara ya kujadilika.* Proposisheni hujadiliwa baina ya watu ambao wanajihusisha nayo. Baada ya kuijadili huweza kuamua kama inafaa kukubaliwa au kukataliwa. Ukweli wake ndio hasa jambo ambalo huifanya ikubalike. Hivyo basi, kama ni ya uongo haina budi kukataliwa. Pili, *ishara ya kuthibitika.* Baada ya mjadala kuhusu proposisheni, washiriki katika mazungumzo wataamua na kuafikiana kuwa yafaa au la. Basi, itakuwa proposisheni yenyewe ina misingi yake ya kuidai kuwa ni ya kweli na wala si ya uongo. Pia katika sura hii, tulipata kuwa proposisheni huwa imo katika misingi ya kweli au uongo. Misingi hii ndio huamua kama itazingatiwa au la.

Katika sura hii pia, tuliona kuwa kuna aina mbalimbali za kauli ambazo hutamkwa na kuwa proposisheni. Aina hizi za kauli ni nne ambazo ni: Kwanza, *kauli za kuamuru na mtazamo.* Kauli hizi hutoa amri na kueleza mambo kama yalivyo. Huwa na mtazamo na mwelekeo fulani kuhusu jambo na amri iliyotolewa yapaswa kuzingatiwa. Pili, *kauli chambuzi.* Aina hizi za kauli hutathmini na kuzingatia kanuni kama kauli zahitaji kutiliwa maanani au la, katika kuamua kuhusu mambo yaliyojadiliwa katika proposisheni. Sharti basi, kanuni zilizopo zifuatwe na kila anayeshiriki katika mazungumzo hayo. Tatu, *kauli za thamani.* Hizi ni kauli ambazo hutathmini au kupendekeza jambo fulani ambalo lafaa zaidi ya mambo mengine. Huchunguza kama kauli ni bora au si bora, kisha hupendekeza kama kauli hiyo ni madai yaliyo sawa ili kukubaliana nayo. Nne, *kauli dhanifu.* Kauli hizi ni ambazo uthabiti wake hutegemea mambo yafaayo na yamo akilini mwa mwanadamu. Huwa hasa zimo katika mafikira ya mtu binafsi na si lazima ziwe na madai yoyote kwani zimo katika dhahania tu.

Mwishowe tuliona kuwa katika sura hii, proposisheni huwa na majukumu kadha kama: Kwanza, *kutoa maagizo*. Msemaji humweleza msikilizaji jambo ambalo analitaka alifanye. Msikilizaji naye huyazingatia maagizo ya msemaji na kutenda kama anavyotarajiwa kufanya. Pili, *kuuliza maswali*. Msemaji huwa na tashwishi kuhusu jambo na hutaka hakikisho kutoka kwa msikilizaji hivyo basi, humuuliza maswali ambayo anatarajia kuwa msikilizaji atampa majibu yafaayo na hasa yawe ni ya kweli. Tatu, *kuamrisha jambo*. Msemaji huenda ikawa ana mamlaka dhidi ya msikilizaji na kumwamrisha kulifanya jambo fulani. Hivyo basi, msikilizaji huwa hana budi ila kuzingatia amri iliyotolewa na msemaji. Vilevile, msemaji hutarajia amri yake izingatiwe ipasavyo. Nne, *kuyakinisha jambo*. Msemaji huhakikisha kuwa anakubaliana na kauli fulani aliyoitamka, ambayo pia msikilizaji hukubaliana nayo. Tano, *kukanusha jambo*. Msemaji hufanya kinyume na kukataa kuafikiana na kauli fulani aliyoitamka, ambayo vilevile msikilizaji huikataa na kuikanusha.

Sura ya tatu, tulijadili kuhusu proposisheni katika vitendo usemi ambavyo hujumlisha: Lokusheni, ilokusheni na palokusheni. Lokusheni ni kitendo kinachotokana na kauli iliyotamkwa na msemaji. Ilokusheni ni kitendo kinachotokana na utendaji wa msemaji baada ya kitamka kauli. Ilokusheni huwa na kauli tano ambazo ni; *kauli wakilishi* au *tetezi*, *kauli za maagizo* au *maelezo*, *kauli za kujitolea*, *kauli elezi* na *kauli za kuarifu*. Palokusheni ni kitendo cha utendaji baada ya msikilizaji kuzipata athari fulani kupitia kwa kauli iliyotamkwa na msemaji. Msikilizaji hutarajiwa kulifanya jambo litakalo afikiana na athari alizozipata.

Pia katika sura hii, tulijadili kuhusu proposisheni katika chukulizi na umaanisho. Chukulizi ni jambo ambalo msikilizaji huchukulia kuwepo kwani msemaji hakulitaja. Hivyo basi, msemaji hutaja baadhi ya mambo na kuyaacha mengine ambayo msikilizaji huyaundia mawazo fulani na kufasiri uwezekano wa jambo alilokusudia msemaji. Huwa na maana kisemantiki katika jambo lililokusudiwa na msemaji na vilevile huwa na maana kipragmatiki kwa kuwalenga watumizi na maana wanayoizua. Umaanisho hurejelea hasa jambo lililolengwa na msemaji ili msikilizaji alifahamu kama lilivyokusudiwa bila kupotosha maana. Huhusishwa na muktadha kwa wakati huo katika chukulizi maalum. Huzingatia kanuni za ushirikiano na Grice ambazo ni; kanuni ya ukweli, kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano na kanuni ya namna.

Vilevile, tuliona kuwa proposisheni yaweza kuwa katika miktadha tofauti kama, ***rasmi* au *isiyo rasmi*** na hutegemea jambo lililojadiliwa. Washiriki huwa na kusudi la kuwasiliana na kuelewana. Muktadha hutatua utata katika baadhi ya kauli ambazo si dhahiri kwa kueleza hatua baada ya nyingine kwa jinsi mambo yanavyofuatana kutoka mwanzo hadi mwisho. Mwishowe katika sura hii tulijadili kuwa proposisehni imo katika semantiki na pragmatiki. Semantiki ni maana iliyopo katika kauli kwa kurejelea lugha fulani. Pragmatiki ni maana iliyopo kulingana na watumizi lugha fulani, hutegemea ufahamu na ufasiri baina ya watu wanaoshiriki katika mazungumzo. Pia uelewa wa matendo binadamu anayoyakusudia kuyafanya ni muhimu katika kuifasiri maana kipragmatiki.

Kulingana na data iliyowasilishwa katika utafiti huu pamoja na matokeo ya uchanganuzi, kuna ithibati kuwa dhana ya proposisheni ina maana katika pragmatiki. Maana hii katika pragmatiki ni

ile ambayo huhusisha watumizi lugha katika mazungumzo mbalimbali. Washiriki katika mazungumzo huafikiana baina yao na kuhakikisha kuwa kuna maelewano mwafaka. Jambo hutimia kwa kuzingatia kanuni za nadharia ya uhusiano, kwani yahusu mawasiliano baina ya msemaji na msikilizaji. Muktadha ndio hubainisha utata uliopo katika mazungumzo hasa kama msikilizaji hana ujumbe wa hapo awali kuhusu jambo lililosemwa. Basi, kama msikilizaji hana ujumbe wa hapo awali au hakuna muktadha wowote uliopo, itabidi abuni chukulizi akilini mwake kuhusu alilokusudia msemaji. Hata hivyo, huenda chukulizi yake haiafikiani na kusudi la msemaji, kwa hivyo muktadha ni muhimu.

Pia, utafiti huu unadai kuwa proposisheni ina maana katika pragmatiki na semantiki kwani, kwanza kuna maana katika jambo lililosemwa ambalo ni semantiki na pili kuna maana katika watumizi lugha kuhusu jambo lililosemwa ambayo ni pragmatiki na hubainisha hasa ni upi ufasiri wa msemaji na msikiliza katika kuafikiana wanapozungumza. Kwingineko, utafiti huu uliongozwa na madhumuni ambayo yanaithibati kuwa yapo katika uchanganuzi wa utafiti huu. Maelezo katika utafiti huu ni kuwa proposisheni ni usemi wa msemaji ambao hukubaliwa au kukataliwa. Kuna aina za proposisheni ambazo kila moja huzingatia kanuni zake ili kuweza kubainika. Vilevile, kuna ishara za proposisheni nzuri ambazo huitambulisha kama bora na yenye kufaa. Proposisheni yapaswa kuthibitika katika misingi ya kweli au uongo wake, katika ukweli wake itakubalika na katika uongo wake itakataliwa. Hivyo basi, washiriki katika mazungumzo wataamua kuhusu proposisheni iliyo mwafaka zaidi. Vivyo hivyo, utafiti huu umejadili kuhusu vitendo usemi ambavyo hujumlisha mambo matatu ambayo huwa ni; kwanza, lokusheni-kitendo cha kauli, pili, ilokusheni-kitendo cha utendaji, tatu, palokusheni-kitendo cha utendaji baada ya kusema jambo.

Sura ya nne, tuliichanganua data yetu. Tulipata kuwa uhusiano huathiri utambuzi wa binadamu kwa sababu jambo ambalo halimhusu mtu kwa vyovyote vile huwa ni vigumu kulifahamu. Ujumbe kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji hufasiriwa kupitia kwa njia ya mfanyiko, tangu wakati wa kutamkwa hadi wakati itakapo tathminiwa ili aidha ithibitike, ikataliwe au ifanywe kuwa bora zaidi. Msikilizaji pia anapaswa kuuhusisha muktadha na mambo yanayohusiana na ambayo yanaafikiana na suala linalozungumziwa. Vilevile, proposisheni huundwa baada ya msemaji kuwa na kichocheo fulani, kisha kutamka kauli. Msikilizaji huufasiri na kuutathmini ujumbe huo.

Kwingincko, maumbo ya semantiki hupewa ufasiri wa kiisimu kwani msemaji huibua maana kulingana na vile anavyoitumia lugha. Muktadha nao huwa na jukumu la kuunda proposisheni baina ya washiriki katika muktadha. Msemaji hukusudia kuwa msikilizaji atatambua lengo lake. Huenda akakusudia maana anuwai katika kauli zake. Vilevile, msikilizaji huwa na matarajio yake katika mazungumzo baina yake na msemaji. Hutaka kupata jambo ambalo lamhusu katika mazungumzo. Pia katika sura hii tulipata kuwa Wilson na Sperber wanauhusiano baina yao na Grice. Hii ni kwa sababu kanuni za ushirikiano na Grice huchanganua na kueleza proposisheni vyema. Dhana na kanuni zao pia zinaafikiana kwa kiasi fulani.

## 5.2 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umejikita tu katika uchanganuzi wa proposisheni katika nyanja ya kiisimi ambayo yahusu pragmatiki kisha kuhusisha semantiki. Hivyo basi, ni bora katika utafiti wa nyakati za usoni kuitafiti proposisheni katika nyanja ya kifasihi kwa kuhusisha proposisheni katika methali, semi na hadithi. Vilevile, proposisheni inaweza kutafitiwa katika nyanja ya kiisimu ambayo yahusu sintaksia kwa kuichanganua katika sehemu mbalimbali zilizomo katika sentensi tofautitofauti kama virai na vishazi. Pia proposisheni kama itatafitiwa katika nyanja ya isimu ambayo yahusu mofolojia kwa kuihusisha na maumbo mbalimbali ya maneno kama nomino, vitenzi na vivumishi.

Vilevile, utafiti huu pia unapendekeza kuwa proposisheni inaweza kutafitiwa katika lugha mbalimbali za kiafrika. Lugha hizi ni kama zile zilizomo nchini Kenya. Hii ni kwa sababu kila lugha huwa na mtindo wake wa kuunda maana. Baadhi yao huunda maana kulingana na matumizi ya kitu, wengine huunda maana kwa kuzingatia umbo la kitu fulani na hata wengine pia huunda maana zao kwa kutazama umaarufu wa kitu hicho. Watumizi lugha pia wanaweza kuafikiana kuhusu njia mwafaka za kuifasiri na kuieleza maana iliyopo katika proposisheni vyema bila kuzua utata. Kwa vile nyanja ya proposisheni ni pana sana, basi huenda kukawa na uwezekano kuwa proposisheni yaweza kuwa ni somo ambalo litakuwa huru na kusomwa kivyake bila kuhusishwa ndani ya semantiki na pragmatiki.

## MAREJELEO


Abraham, S. (1996). *A Theory of Structural Semantics*: Mouton and Company Publishers.

Akmajian, A. na Wenzake. (2004) *Linguistics. An Introdution to Language and Communication.* Fifth Edition: MIT Press, Cambridge.

Atichi, A.R. (2004) The Semantic Distinctiveness of Kenyan English: UON. Unpublished MA Thesis.

Atoh, F.O. (2001) Semantics Analysis of Dholuo Nowns: The Semantics Field Approach. UON. Unpublished MA Thesis.

Blass, R. (1990) *Relevance Relations in Discource*. A Study in Special Reference to Sissala: Cambidge University Press.

Brown, G. na Yule, G. (1983) *Discource Analysis*: Cambridge University Press.

Bussman, H. (1996) *Route*ledge *Dictionary of Language and Linguistics*: International Thompson Publishing Company.

Cambridge (2008) *Cambridge Advanced Learners Dictionary.* Cambridge University.

Carston, R. (2002) *Thoughts and Utterances.* The Pragmatics of Explicit Communication. MA: Blackwell Publishers Ltd.

Cornford, F. M. (1957) *Platos Theory of Knowledge*: Routeledge and Kegan Paul Ltd.

Crystal, D. (2003) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics.* Fifth Edition. Oxford: Blackwell Publishers.

Falsod, R. W. (2002) *An Introdution to Language and Linguistics.* Cambridge University Press.

Fleming, (1998) Google Search. Powered by The Ultimate Programming Weblog. Sil Internatinal: http:// worldnet Princeton. Edu/Pert/Webwn.

Fodor, J. D. (1997) *Semantics: Theories of Meaning in Generative in Generative Grammar*: Harper and Row , Publishers.

Fretheim, A. (2000) *Pragmatic Markers and Propositional Attitude*: John Benjamin Publishing Company.

Green, G. M (1996) *Pragmatics and Natural Language Understanding.* Second Edition: Lawrence Erlbaum Associates Publishers.

Greenbaum, S. na Wenzake. (1985) *A comprehensive Grammar of English Language:* Longman Group UK Ltd.

Griffin, E. M (1991) *A First look at Communication Theory.* Wheaton College: Mc Graw- Hill, Inc. Company.

Hofmann, T. R. (1993) *Realms of Meaning*: An Introduction to Semantics: Longman Group UK Ltd.

Ifantidou, E. (2001) *Evidentials and Relevance.* Volume 86: John Benjamin Publishing Company.

Kamau, S. K. (2008) An Analysis of Truth Conditions in Pragmatics: Relevance Theory Approach. UON. Unpublished MA Thesis.

Kasher, A. (1998) *Pragmatics.* Critical Concepts. Volume V: Communication, Interaction and Discourse: Routeledge Publishers.

Katie, W. (2001) *A Dictionary of Stylistics*: Longman Group UK Ltd.

Katz, J.J. (1977) *Propositional Structure and Illocutionary Force*. A Study of the contribution of Sentence meaning and Speech Acts: The Harvest Press.

Kempson, R. M. (1975) *Pressuposition and The Delimination of Semantics*: Cambridge University Press.

Larson, M. L. (1984) *Meaning-Based Translation*: A Guide to Cross–Language Eqivalence: University Press of America, Inc.

Leech, G. (1974) *Semantics:* Penguin Books Limited.

Leech, G. N. (1971) *Towards a Semantic Description of English*: Longman Group Ltd.

Linsky, L. (1952) *Semantics and the Philosophy of Language*: University of Illinois Press.

Longmans (1968) *Longmans English Larousse*: Longmans, Green and Co. Ltd.

Munga, C. M. (2009) Sence Relations in Gikuyu: A Lexical Pragmatics Approach. UON Unpublished MA Thesis.

Ndug'u, M. N. (2009) Mada na Fokasi katika Kiswahili: Mtazamo wa Muundo wa Taarifa. UON. Unpublished MA Thesis.

Ogola, C. A. (2006) A Pragmatic Analysis of Intercultural Communication Failures. UON, Unpublished MA Thesis.

Palmer, F. R. (2006) *An Introduction to Language and Linguistics*: Cambridge University Press.

Rouchota, V, na Jucker, H. (1998) Current Issues in Relevance Theory: John Benjamin Publishing Company.

Saeed, J. L. (2003) *Semantics.* Second Edition: Blackwell Publishing Ltd.

Schroeder, H. (2005) *Do we Speak the same Language*? A cognitive Pragmatic Explanation of Cultural Misunderstanding. In Across Borders: Benefiting from Cultural Differences. Conference Proceedings. 17th-18th March: 2005.

Sperber, D na Wilson, D. (1995) Communication and Cognition, 2nd Edition: Blackwell Publishers.

Sperber, D na Wilson, D. (2004) A Handout on Relevance Theory (1985-2002): Blackwell Publishers.

Tuki (1990). *Kamusi ya Isimu na Lugha.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Educational Publishers and Distributors Ltd.

Tuki (2006) English-Swahili Dictionary. Third Edition: Book Printing Services Ltd.